JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA AFYA

## HOTUBA YA WAZIRI WA AFYA MHE. MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA BAJETI YA WIZARA YA AFYA KWA MWAKA 2026/2027



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akimjulia hali mtoto aliyelazwa katika wodi ya watoto iliyopo katika jengo jipya la huduma za afya ya mama na mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Katavi*

**Mei, 2026** **Dodoma**



*Makamu wa Rais Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi akimjulia hali mgonjwa ambaye amelazwa kwa ajili ya matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila, jijini Dar Es Salaam.*



*Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba akimjulia hali mama aliyejifungua wakati alipofanya ziara katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma.*



*Waziri wa Afya **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)** akizungumza na wananchi Mbashara kupitia mfumo wa Ongea na Waziri mara baada ya kuuzindua rasmi mfumo huo mwezi Februari 26, 2026 katika Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru Jijini Arusha.*



*Naibu Waziri wa Afya, **Mhe. Dkt. Florence George Samizi (Mb)**, akishuhudia huduma ya "Kangaroo Mother Care" kwa mama na mtoto katika Hospitali ya Meta iliyopo Mkoani Mbeya.*




*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, ikiongozwa na Mwenyekiti wake **Mhe. Dkt. Johannes Lukumay** katika picha ya pamoja na viongozi wa Wizara, ilipokagua maendeleo ya huduma za uchunguzi wa saratani katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road.*




*Waziri wa Afya, **Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)** akiwa na Menejimenti ya Wizara wakati wa Kikao cha Baraza la Wafanyakazi kilichofanyika Jijini Mwanza, Mei 2026.*

# YALIYOMO

**SEHEMU YA I: UTANGULIZI .......................................... 1**

**SEHEMU YA II: MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2026. ................................................................ 17**

**SEHEMU YA III: MAENEO MAHSUSI YA MSISITIZO ... 40**

**SEHEMU YA IV: MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026 ................................. 48**

**SEHEMU YA V: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA ................................................................ 54**

Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza ........................... 54

Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza ............................. 70

Utoaji wa Huduma za Kinga ............................................ 87

Huduma za Dharura na Majanga .................................. 108

Utoaji wa Huduma za Tiba ............................................ 117

Huduma za Uuguzi na Ukunga ...................................... 171

Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya ............................... 175

Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa ............................ 179

Huduma za Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi ............... 191

Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ................... 210

Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya ............................ 216

Ufuatiliaji na Tathmini ..................................................... 224

Ugharamiaji wa Huduma za Afya .................................. 226

Utekelezaji wa Majukumu ya Mabaraza na Bodi za Kitaaluma ...................................................................... 237

Miradi ya Maendeleo ....................................................258

**SEHEMU YA VI: VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI, MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO VYA WIZARA YA AFYA, KWA MWAKA 2026/2027. ....................................................266**

**SEHEMU YA VII: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA** 2026/2027 ....................................................280

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| API | – | Application Programming Interface |
| CPAP | – | Continuous Positive Air Way Pressure |
| ECG | – | Electrocardiography |
| ECHO | – | Echodardiography |
| GBV | – | Gender Based Violence |
| HBV | – | Hepatitis B Virus |
| HCV | – | Hepatitis C Virus |
| HDU | – | Health Data Universal |
| IQC | – | Internal Quality Control |
| MRI | – | Magnetic Resonance Imaging |
| NCU | – | Neonatal Care Unit |
| NEMS | – | National Emergency Medical Service |
| PET CT-Scan | – | Positron Emission Tomography and Computed Tomography |
| PHEOC | – | Public Health Emergency Operation Center |
| SADCAS | – | Southern African Development Community |

| | | |
|---|---|---|
| | | Accreditation Service |
| STBF | – | Susan Thompson Buffet Foundation |
| TAEC | – | Tanzania Atomic Energy Commission |
| TIRA | – | Tanzania Insurance Regulatory Authority |
| UVIDA | – | Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa |

## SEHEMU YA I: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya Bunge lako tukufu kupokea taarifa iliyochambua bajeti ya Wizara kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI, naomba kwa mujibu wa **vifungu namba 118 hadi 123 vya kanuni za kudumu za Bunge toleo la mwaka 2023**, kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026 na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2026/2027.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu na kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Kwa namna ya kipekee kabisa nachukua fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuniamini na

kuniteua kuwa Waziri wa Afya. Wizara hii sio tu inagusa afya za kila mtanzania bali inagusa uhai wa watanzania wote bila kujali jinsi, umri, dini, kabila, tajiri au maskini. Ninatambua kuwa, nina deni na dhima kubwa kwa nchi yangu katika kutekeleza jukumu hili muhimu na ninamuahidi Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu pamoja na watanzania wote kuwa sitawaangusha.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru pia Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia kwa nchi, mashirika ya kimataifa, wadau mbalimbali wa maendeleo wa ndani na nje ya nchi licha ya changamoto za ugharamiaji wa huduma za afya zilizotokana na kubadilika kwa sera za nje. Katika kuhakikisha kuwa nchi inavuka salama katika kipindi hiki, Mheshimiwa Rais ameendelea kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha huduma za afya nchini zinaendelea kutolewa bila kuathiri uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na wadau mbalimbali uliodumu kwa muda mrefu tangu tulipopata uhuru. Mheshimiwa Rais amekuwa

kinara wa kuimarisha uhusiano wa diplomasia ya kimataifa na kutetea maslahi ya Taifa ili kujenga Tanzania yenye amani na uchumi imara.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue nafasi hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Rais** kwa kuchaguliwa kwa awamu ya pili kupitia uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Ushindi huo wa kishindo ni ishara kuwa wananchi wana imani na Mheshimiwa Rais na Serikali kwa ujumla. Nami namuahidi kuwa, kwa imani ile ile iliyooneshwa na watanzania, nitaibeba agenda yake ya kuimarisha huduma za afya nchini na kuwa chachu ya kukuza uchumi hasa ikizingatiwa kuwa Afya ni Mali na Afya ni Mtaji.

***"Baba wa Taifa aliwahi kusema kuwa afya ya wananchi ni msingi wa maendeleo na Taifa haliwezi kuendelea ikiwa watu wake ni wagonjwa au dhaifu". "na kwa mafunzo ya Nelson Mandela, heshima ya binadamu ni kiini cha taifa huru. Hivyo, huduma ya afya tunayojenga ni huduma ya utu, haki na maendeleo" Nami nitaendelea***

***kusimamia utekelezaji wa maono hayo ili kufikia azma na maono ya sekta ya afya ya kujenga jamii yenye afya bora na ustawi itakayochangia katika kukuza uchumi wa nchi na mtu mmoja mmoja".***

5. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,** kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuiongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Imani waliyopewa na wananchi kwa kuwachagua, ni ishara kuwa wananchi wana imani kubwa kwao katika kuendelea kuleta mabadiliko makubwa ya kimahusiano, kiuchumi na kijamii katika nchi yetu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)**, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri

Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni matumaini yangu kuwa miongozo, maelekezo, hekima na busara zake katika kusimamia shughuli za Serikali, zitanisaidia katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku ya usimamizi wa Sekta ya afya kwa ufanisi mkubwa.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri na uongozi thabiti unaozingatia kanuni bila upendeleo katika kusimamia majadiliano na kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu. Aidha, nampongeza **Naibu Spika, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)**, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge. Nitumie fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa ili kusimamia na kuishauri Serikali kwa maslahi mapana ya Taifa.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Johannes Lukumay (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI na **Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid (Mb)** kuwa Makamu Mwenyekiti. Hakika miongozo yenu na ushauri kwa kushirikiana na wajumbe wa Kamati ni nguzo muhimu katika kuwezesha kuboresha utendaji wa majukumu ya Wizara ya Afya. Aidha, ninawapongeza Waheshimiwa wabunge wote kwa kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa wawakilishi wa wananchi katika Bunge hili tukufu. Ninawaahidi waheshimiwa Wabunge wote kwamba, Wizara ya Afya itaendelea kutoa ushirikiano kwa kuzingatia ushauri wenu katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini. Vilevile, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa **Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard** na watumishi wa Bunge kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia. Niwahakikishie kuwa viongozi na watumishi wa Sekta ya Afya nchini tutaendelea kutekeleza wajibu wetu wa kutoa huduma

bora za afya kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utoaji wa huduma za afya.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Florence George Samizi (Mb)**, kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri wa Afya. Ninaamini kuwa, taaluma na uzoefu wake katika Sekta ya Afya utasaidia kuleta mapinduzi yenye tija. Vilevile, nachukua nafasi hii kumpongeza **Ndugu. Emmanuel Tayari** kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya anayeshughulikia masuala ya dawa na vifaa tiba.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee nachukua fursa hii kuwashukuru **Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe**, Katibu Mkuu, **Ndugu. Ismail Hassan Rumatila**, Naibu Katibu Mkuu na **Dkt. Grace Elias Magembe**, Mganga Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Afya. Vilevile, naishukuru **Menejimenti ya Wizara ya Afya na**

**watumishi wote wa Sekta ya Afya** kwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, moyo wa uzalendo na imani thabiti kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita. Hakika mmekuwa nguzo muhimu kwa kipindi kifupi ambacho nimehudumu katika Wizara.

11. ***Mheshimiwa Spika*****,** natoa shukrani kwa Wizara zote kwa namna tunavyoshirikiana kwa pamoja kuimarisha huduma za afya nchini. Kipekee naishukuru Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali watu, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kuwezesha utekelezaji wa afua za afya mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu kwa uratibu wa sekta mtambuka, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, kwa usimamizi wa huduma za afya ngazi ya msingi, Wizara ya Fedha kwa kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kushirikiana na Wizara katika masuala mbalimbali ya kisheria na Wizara ya Maji

katika kuimarisha afua mbalimbali za afya kupitia upatikanaji wa maji safi na salama.

***12. Mheshimiwa Spika*****,** kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote zilizo chini ya Wizara ambao ni **Bw. Mavere Tukai** (MSD), **Dkt. Irene Isaka** (NHIF), **Dkt. Adam Fimbo** (TMDA), **Prof. Said Shehe Aboud** (NIMR), **Dkt. Fidelice Mafumiko** (Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali), **Dkt. Germana Leyna** (Taasisi ya Chakula na Lishe). Pia, nichukue fursa hii kuwashukuru Wakurugenzi wa Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda ambao ni **Dkt. Delillah Kimambo** (Hospitali ya Taifa Muhimbili), **Mheshimiwa. Balozi Dkt. Mpoki Ulisubisya** (Taasisi ya Mifupa MOI), **Dkt. Peter Kisenge** (Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete), **Dkt. Diwani Msemo** (Taasisi ya Saratani ya Ocean Road), **Dkt. Leonard Subi** (Hospitali ya magonjwa ambukizi Kibong'oto), **Dkt. Innocent Mwombeki** (Hospitali ya Afya ya Akili Mirembe) na Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa za Kanda **Dkt. Godlove Mbwanji**

(Hospitali ya Rufaa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya), **Prof. Abel Makubi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Benjamin Mkapa), **Dkt. Brian Mawalla** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato), **Dkt. Herbert Massigati** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mtwara), **Dkt. Sr. Alicia Massenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando), **Prof. Gileard Masenga** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC) na **Bi. Brenda Msangi** (Hospitali ya Rufaa ya Kanda CCBRT).

13. ***Mheshimiwa Spika,*** pia napenda kuwashukuru Waganga Wakuu wa Mikoa na Halmashauri, Waganga Wafawidhi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa zote 28, Hospitali za Halmashauri, vituo vya afya, zahanati, wakuu wa vyuo vya mafunzo vilivyo chini ya Wizara, wasajili wa bodi na mabaraza ya kitaaluma. Aidha, kipekee nawashukuru watumishi na watendaji wa Sekta ya Afya wa ngazi zote kwa mchango wao katika kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa bidii, weledi na kujitoa usiku na mchana kuokoa maisha ya watanzania.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kushirikiana na nchi rafiki na mashirika ya kimataifa yanayochangia katika uboreshaji na utoaji wa huduma za afya nchini. Hivyo basi, nitumie wasaa huu kuzishukuru nchi za Canada, Denmark, Uingereza, Ireland, Uswisi, Korea Kusini na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, UNFPA na UNICEF kwa kuchangia katika Mfuko wa Afya wa Pamoja (Health Basket Fund), ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya nchini hususan afya ya msingi. Aidha, napenda kuzishukuru nchi za Ujerumani, Japan, India, Sweden, Umoja wa Falme za Kiarabu, Uturuki, Marekani, Ufaransa, China, Cuba, Italia, Misri na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Sekta ya Afya kwa njia mbalimbali ikiwemo kufadhili miradi inayotekelelezwa na Serikali ili kuboresha huduma za afya nchini.

15. ***Mheshimiwa Spika***, kwa dhati kabisa, napenda kutoa shukrani zangu kwa Sekta binafsi, mashirika ya dini, asasi za kiraia, vyama vya kitaaluma na mashirika yasiyo ya

kiserikali kwa mchango wao mkubwa katika kuimarisha huduma za afya nchini. Wadau hao wamekuwa mstari wa mbele katika kushirikiana na Serikali kuleta maendeleo ya sekta ya afya. Baadhi ya wadau hao ni, Benjamin Mkapa Foundation, APHFTA, AMREF, AGOTA, AGPAHI, APT, BAKWATA, CSSC, CCT, Foundation for Cancer Care in Tanzania, LHL International, MDM, COUNSENUTH, ELCT, Ifakara Health Institute, Lions Club, MAT, PST, TAPHATA, Good Samaritan Foundation, Aga Khan Foundation, NEST 360, EGPAF, JHPIEGO, JSI, FHI, AFRICARE, Abbott Fund Tanzania, Shirika la Msalaba Mwekundu, Plan International, MEHATA, TAMWA, TAWLA, TGNP, MDH, Pathfinder, PATH, CHAI, AMERICARES, MELSAT, TARA, TAWOPHA, PASADA, NACOPHA, PAT, PSI, PRINMAT, Rotary Club International, SIKIKA, MKUTA, Shree Hindu Mandal, TANNA, TPHA, Tanzania Surgical Association, SATA, Tanzania Diabetic Association, TANESA, THPS, Tunajali, Tanzania Midwives Association, TAYOA, NACONGO, TDA, TISS, TEC, UMATI,

USADEFU, White Ribbon Alliance, LSF, CIHEB TANZANIA, Starlink Gulf Trading LTD, KIVULINI, WILDAF, Haydom Lutheran Hospital, GSM Foundation, MO Foundation, VODACOM Foundation, TCRF, FSDT, JAI, Touch Foundation pamoja na asasi nyingine zinazoshirikiana na Sekta ya Afya kwa namna moja au nyingine. Ushirikiano wao ni wa kupongezwa na unaendelea kuwa chachu ya maendeleo katika sekta ya afya nchini.

16. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani za dhati kwa vyuo vya elimu ya juu vinavyoshirikiana na Sekta ya Afya katika kuimarisha huduma za afya nchini. Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Kairuki, Chuo Kikuu cha Katoliki cha Afya na Sayansi Shirikishi, Chuo Kikuu cha KCMC, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph, Chuo Kikuu cha Aga Khan, Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro, Chuo Kikuu cha

Kimataifa cha Kampala, Vyuo Vikuu vya Sayansi na Teknolojia Mbeya na Arusha, Taasisi ya Teknolojia ya Nelson Mandela, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Mtakatifu Franscisco pamoja na wadau wote wa vyuo vya kati vinavyotoa mafunzo ya afya na sayansi shirikishi.

17. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa, nitumie fursa hii mbele ya Bunge lako tukufu kuwashukuru kwa moyo wa dhati wananchi wote wa jimbo langu pendwa la Rufiji kwa namna wanavyoniamini na kunipa ushirikiano wa kiwango cha juu katika kipindi chote ninachowatumikia kama Mbunge wao. Kila ninapokumbuka imani waliyonayo kwangu, ninajikuta mwenye nguvu na ari kubwa ya kuwatumikia wananchi wa jimbo langu. Ninawaahidi kuwa nitafanya kazi bila kuchoka ili kuhakikisha ahadi zangu kwao na vipaumbele tulivyopanga kwa pamoja jimboni ninavitekeleza sio tu kwa maslahi mapana ya wana Rufiji bali kwa maslahi ya Taifa kwa

ujumla. Natambua imani yao ni deni kubwa kwangu na nimedhamiria kuzitekeleza ahadi zangu kwa uadilifu kama ilivyo desturi yetu wana Rufiji kuweka mbele uadilifu na uzalendo katika kuijenga Rufiji na Taifa letu kwa ujumla.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** mwisho japo sio kwa umuhimu, nichukue nafasi hii kipekee kuishukuru familia yangu kwa upendo, uvumilivu, ushirikiano, dua na maombi yao wakati wote ninapokuwa natekeleza majukumu yangu. Hakika wamekuwa wa msaada na faraja kubwa kwangu wakati wote ninapokuwa katika wajibu wangu wa kuwatumikia watanzania.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwako binafsi na Bunge lako tukufu, wanafamilia wote, ndugu, jamaa, marafiki, na wananchi wote kwa ujumla kwa kuondokewa na wapendwa wetu; Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge,

Uratibu na Wenye Ulemavu. Vilevile, nitoe pole kwa kifo cha Mheshimiwa Halima Idd Nassor aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (Wafanyakazi), Muadhama Polycarp Kardinali Pengo, Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es salaam, Mhashamu Bernadin Francis Mfumbusa aliyekuwa Askofu Mkuu wa Jimbo Katoliki la Kondoa na viongozi wengine wa dini na madhehebu mbalimbali waliopoteza maisha.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** natoa pole kwa watumishi wa Sekta ya Afya kwa kuwapoteza watumishi wenzao katika kipindi hiki na watanzania wote waliopoteza ndugu zao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na magonjwa, ajali na majanga. Kipekee nitoe salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma na wananchi wote walioguswa kwa ajali ya boti iliyotokea tarehe 13 Machi, 2026 na kusababisha Sekta ya Afya kupoteza watumishi saba (7) wa kada za afya waliokuwa kazini wakitekeleza majukumu yao. Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

## SEHEMU YA II: MAFANIKIO YA SEKTA YA AFYA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KUANZIA MWAKA 2021 HADI 2026.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo yangu ya awali, naomba sasa kutambua mafanikio ya Sekta ya Afya yaliyotokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu alipoingia madarakani kama ifuatavyo:-

### Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya

22. ***Mheshimiwa Spika,*** vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 10,153 mwaka 2021/22 na kufikia vituo 13,683 mwezi Machi 2026 sawa na ongezeko la vituo 3,530 vilivyojengwa katika kipindi cha Awamu ya Sita. Ongezeko hili linahusisha Zahanati 8,706 kutoka 7,189; Vituo vya Afya 1,359 kutoka 956; Hospitali 475 kutoka 404 na Vituo vinginevyo 3,143 kutoka 1,604. Aidha,

kuna ongezeko la majengo mapya katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Mbeya, Hospitali ya Kanda Benjamin Mkapa, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda Kusini Mtwara na Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imejenga hospitali kumi (10) mpya za rufaa za mikoa ambapo hospitali tano (5) za mikoa ya Katavi, Njombe, Geita, Simiyu na Songwe hazikuwa na hospitali hizo na hospitali tano (5) za mikoa ya Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi zilihamishwa kutoka majengo ya zamani kwenda kwenye majengo yaliyojengwa katika maeneo mapya. Vilevile, Serikali imeongeza majengo katika hospitali za rufaa za mkoa za Ligula (Mtwara), Sekou Toure (Mwanza), Maweni (Kigoma), Sumbawanga (Rukwa) na Kitete (Tabora). Hivyo, kwa sasa mikoa yote nchini ina hospitali za rufaa za mikoa na Wilaya zote zina hospitali katika ngazi ya

halmashauri. Pia, Serikali imefanya ukarabati wa majengo ya zamani katika hospitali kongwe 50 za Halmashauri, ukamilishaji wa maboma ya zahanati 980, ujenzi wa vituo vya afya 390, ujenzi wa mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na wagonjwa wa dharura kutoka 25 hadi 61 na ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya zenye uwezo wa kuhudumia kaya 540.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utoaji wa huduma za dharura nchini, idadi ya majengo maalum ya kutolea huduma za dharura (Emergency Medicine Department – EMD) imeongezeka kutoka saba (7) yaliyokuwepo mwaka 2021/2022 katika ngazi ya rufaa pekee hadi kufikia 125 mwezi Machi 2026, yakijumuisha ngazi ya rufaa na msingi, sawa na ongezeko la majengo 118. Hii ni hatua ya kihistoria, kwani kwa mara ya kwanza huduma hizi zimefikishwa hadi ngazi ya afya ya msingi, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania hupata huduma. Uwekezaji huu umeimarisha upatikanaji wa huduma za dharura ndani ya muda muhimu wa saa moja ya kwanza

(Golden Hour), ambao kitaalamu ni kipindi muhimu cha kuokoa maisha na kuzuia madhara makubwa kama ulemavu au kifo. Aidha, Wizara inaendelea kusimamia ubora wa huduma hizi, kwa kuwa ushahidi unaonesha kuwa huduma bora za dharura zinaweza kupunguza vifo kwa wastani wa asilimia 40 na hivyo kuokoa maisha ya wagonjwa wa dharura, ajali na majanga.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya vitanda vya wagonjwa imeongezeka kutoka 86,131 mwaka 2021/2022 hadi 156,932 mwezi Machi 2026 ikiwa ni ongezeko la vitanda 70,801 sawa na asilimia 82. Aidha, idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka 258 mwaka 2021/2022 hadi 1,647 mwezi Machi 2026 ikiwa ni ongezeko la vitanda 1,389. Ongezeko la vitanda hivyo limeboresha huduma kwa wagonjwa mahututi, wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalum na wagonjwa wote wa kulazwa na kuwezesha kupunguza vifo vinavyoweza kuzuilika.

## Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika miaka mitano iliyopita Serikali imeimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kupitia diplomasia ya afya na kuwezesha kutekeleza miradi mbalimbali iliyogharimu kiasi cha Shilingi Trilioni 1.2 zilizowezesha kuongezeka kwa wodi maalum za watoto wachanga kutoka 49 mwaka 2021/2022 hadi 438 mwezi Machi 2026 na vituo vya uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi katika ngazi ya msingi kutoka 732 mwaka 2021/2022 hadi 1,700 mwezi Machi 2026. Aidha, katika kipindi hicho kupitia mpango wa madaktari wa Dkt Samia, mafunzo kazini kwa watumishi 29,129 yametolewa na jumla ya watu 286,381 wamehudumiwa. Vilevile, Serikali imehakikisha upatikanaji wa dawa muhimu za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa asilimia 85 zikiwemo bidhaa za uzazi wa mpango, dawa za kuzuia damu kuvuja kwa wingi wakati wa kujifungua (oxytocin na misoprostol), dawa za kutibu kifafa cha mimba (magnesium sulfate), dawa za kutibu kuharisha kwa watoto

(ORS/Zinc) na vidonge vya myeyuko vya kutibu nimonia kwa watoto (amoxycilline).

27. ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio hayo yamechangia kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104 mwaka 2022. Kushuka kwa vifo hivyo kumesababisha **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kuchaguliwa kuwa kinara wa huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto katika bara la Afrika. Kutokana na heshima kubwa iliyopewa Tanzania, Serikali imedhamiria kwa dhati kuendelea kuwekeza katika afua za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza kwa asilimia 50 ya vifo 104 kwa takwimu za sasa ifikapo 2030. Lengo ni kuvuka Malengo Endelevu ya Dunia ya vifo vitokanavyo na uzazi kufikia chini ya 70 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo 2030.

***"Nichukue fursa hii kuwafahamisha waheshimiwa wabunge na wananchi kuwa, Mheshimiwa Rais ameendelea***

***kutambuliwa kama Rais wa mfano aliyefanya vizuri katika kupunguza kwa kiasi kikubwa vifo vitokanavyo na uzazi kwa kipindi cha muda mfupi tangu kuingia madarakani. Mafanikio hayo yametokana na dhamira yake ya dhati ya kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na kuboresha huduma za afya nchini kwa lengo la kuhakikisha hakuna mwanamke anapoteza maisha wakati analeta uhai duniani”.***

**Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa**

***28. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa mionzi kwa wagonjwa, Serikali imenunua na kusimika vifaa tiba vya uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya Shilingi bilioni 241.6 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya hospitali ya Taifa hadi ngazi ya afya ya msingi. Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, MRI zimeongezeka kutoka saba (7) hadi 13, CT Scan 12 hadi 45, Mini Angio Suite tano (5), kipimo cha uchunguzi na tiba ya magonjwa ya mfumo wa chakula na mfumo

wa uzazi (Fluoroscopy) 14, Digital X-ray 147 hadi 559, Ultrasound 476 hadi 970, huduma ya kutibu matatizo ya moyo ya dharura (CathLab) moja (1) hadi nne (4) na matibabu ya hali ya juu ya magonjwa ya saratani (PET CT SCAN) ambayo haikuwepo awali na sasa ipo moja (1). Aidha, kuongezeka kwa vifaa na vifaa tiba vya uchunguzi kumepunguza rufaa za ndani na nje ya nchi, kumewezesha kusogeza huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu na kusaidia kutoa matibabu sahihi zaidi na kupunguza muda wa kupata huduma. Tumeshuhudia siku za karibuni wananchi wengi wakijiuliza kwa nini magonjwa yameongezeka, pamoja na sababu nyingine za mtindo wa maisha na mabadiliko ya tabia nchi, uwezo wetu wa kugundua na kutambua magonjwa umeongezeka sana kufuatia uwekezaji huu mkubwa.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha huduma bora za maabara zinapatikana nchini kwa kuendelea kuijengea uwezo Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii ambapo mwaka 2025 Maabara hiyo imepata

ithibati ya kimataifa ISO 17043:2022 ya kuandaa, kusambaza, kusimamia na kupima ubora wa vipimo vya maabara ndani na nje ya nchi. Hatua hiyo imeongeza uwezo wa ndani wa usimamizi wa maabara, kupunguza utegemezi kwa maabara za nchi za nje katika uthibiti ubora wa maabara, kupunguza gharama, kulinda usalama wa nchi na kuongeza upatikanaji wa huduma kwa wakati.

30. ***Mheshimiwa spika,*** katika kuendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa maabara nchini, Serikali imefanikiwa kuongeza maabara zilizopata ithibati ya ubora wa kimataifa kutoka Maabara 49 mwaka 2021/2022 hadi 102 Machi 2026. Aidha, Serikali imenunua na kusimika mashine za uchunguzi wa maabara 3,238 ambapo mashine 1,081 ni za hematolojia, mashine 1,334 za uchunguzi wa kemia, mashine 792 za uchunguzi wa mkojo na mashine 31 za kuotesha vimelea na kutambua dawa sahihi ya kuua vimelea husika. Mashine hizo zimesimikwa kwenye vituo 900 vya kutolea huduma katika ngazi mbalimbali zikiwemo

zahanati nane (8), vituo vya afya 686, hospitali za wilaya 121, hospitali teule za wilaya 39, hospitali za kijeshi 29 na hospitali 64 za ngazi ya rufaa. Vilevile, Serikali imefanikiwa kununua jumla ya makabati 15 ya usalama wa vimelea vya magonjwa ambayo hutumika kulinda afya za wataalam wa maabara dhidi ya vimelea hatarishi wakati wa kutimiza majukumu yao.

## Huduma za Ubingwa na Ubingwa Bobezi

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika ngazi ya rufaa ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana ndani ya nchi. Baadhi ya huduma za ubingwa bobezi zilizotolewa kwa wagonjwa kuanzia mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026 ni pamoja na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 170, upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa 57, upandikizaji wa vifaa vya usikivu kwa wagonjwa 102, uwekaji wa puto tumboni kwa wagonjwa 200, kuondoa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa kutumia mawimbi

mshtuko kwa wagonjwa 510, upandikizaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 1,791, upasuaji wa mgongo kwa wagonjwa 1,688, upasuaji wa kibiongo kwa wagonjwa 98, upasuaji na urekebishaji wa mifupa ya kiuno kwa wagonjwa 647, upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi kwa wagonjwa 2,095, na upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu kwa wagonjwa 1,246.

32. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma nyingine za ubobezi zilizotolewa katika miaka mitano ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ni pamoja na upasuaji wa ubongo kwa kufungua kichwa kwa wagonjwa 1,208, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 785, uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 1,347, upasuaji wa moyo (kwa kufungua kifua) kwa wagonjwa 73, kuzibua mishipa ya moyo kwa wagonjwa 2,074, upandikizaji wa kurekebisha mapigo ya moyo kwa wagonjwa 34, upasuaji wa macho kwa kutumia matundu madogo kwa wagonjwa 1,078, upasuaji wa ubongo kwa kutumia teknolojia ya mawimbi kwa wagonjwa 13,

matibabu ya radiolojia kwa wagonjwa 1,680, matibabu ya mfumo wa chakula na ini wagonjwa 9,666, tiba mionzi bobezi kwa wagonjwa 1,651, tiba ya mionzi ya ndani kwa wagonjwa 10,056, tiba ya *immunotherapy* wagonjwa 4,024, huduma za upasuaji wa magonjwa ya saratani kwa wagonjwa 6,097 na wagonjwa 731 wa saratani walifanyiwa uchunguzi kwa kutumia PET-CT scan.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji katika huduma za ubingwa na ubingwa bobezi umewezesha watanzania wengi kupata huduma hizo ndani ya nchi na karibu na maeneo wanapoishi kwa gharama nafuu ambapo awali walikuwa wakizifuata huduma hizo nje ya nchi. Aidha, uwekezaji huo haujawanufaisha watanzania pekee bali wagonjwa kutoka nchi za jirani nao wamevutiwa na huduma nzuri zinazotolewa na hospitali na taasisi zetu hali iliyopelekea kuhudumia jumla ya wagonjwa 26,770 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia, Malawi, Msumbiji, Kenya,

Burundi, Angola, Rwanda, Sudani ya Kusini, Somalia na Uganda.

**Hali ya Upatikanaji wa Chanjo Nchini**

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo nchini ambapo idadi ya watoto waliopata chanjo ya *Pentavalent* dozi ya 3 imeongezeka kutoka watoto 2,093,412 hadi 2,361,701 na kufanya wastani wa watoto waliopata chanjo kuongezeka kutoka asilimia 93 mwaka 2021/2022 hadi 94.3 Machi 2026 na hivyo kuendelea kuvuka lengo la kimataifa la asilimia 90. Vilevile, katika kipindi hicho Wizara imeratibu ununuzi wa dozi 161,499,930 za chanjo zenye thamani ya Shilingi 439,889,990,420 zilizosambazwa nchi nzima na hadi kufikia Machi 2026 kulikuwa na jumla ya dozi 20,268,820 za chanjo mbalimbali katika maghala ya kuhifadhia chanjo. Hii inaonesha kuwa upatikanaji wa chanjo nchini ni wa kutosheleza na huduma za kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa 13

yanayozuilika kwa chanjo zimeendelea kupatikana bila malipo kwa wananchi kulingana na mahitaji.

***35. Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za chanjo ili kuhakikisha chanjo zinafika kwa walengwa kwa ubora unaostahili kwa kununua majokofu 3,980 yenye thamani ya Shilingi 31,486,129,515, boti saba (7) zenye thamani ya Shilingi 1,184,312,500 kwa ajili ya huduma za chanjo kwa halmashauri za Wilaya ya Kibiti, Kigoma, Muleba, Ukerewe, Nkasi na Zanzibar. Vilevile, magari 68 aina ya Hilux pickup double cabin, malori 28 na pikipiki 300 zimenunuliwa kwa ajili ya kusaidia kutoa huduma za chanjo nchini. Aidha, Serikali imesambaza mfumo wa rejista ya kielektroniki kwenye vituo 1,487 vilivyopo katika halmashauri 33 za mikoa sita (6) pamoja na ugawaji wa vishikwambi 1,603 kwenye vituo vya serikali na binafsi kwa ajili ya huduma za chanjo.

## Hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi, 2026, jumla ya Shilingi trilioni 1.4 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa bidhaa za afya kupitia Bohari ya Dawa (MSD). Aidha, kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi bilioni 150 zilitolewa kulipa madeni ya MSD na Shilingi bilioni 141.9 zilitolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa za UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu na Shilingi trilioni 1.1 zilitumika kwa manunuzi ya bidhaa za afya kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya. Pia, katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 11 vya dawa na vifaa tiba ambavyo ni viwanda viwili (2) vya kuzalisha maji tiba, viwanda vitatu (3) vya kuzalisha vitendanishi vya maabara, viwanda vitatu (3) vya kuzalisha dawa za vidonge na maji na viwanda vitatu (3) vya kuzalisha vifaa tiba. Viwanda hivyo vitawezesha uwepo endelevu wa maji tiba,

vitendanishi vya maabara, dawa za maji na za vidonge.

37. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeanza kufufua na kuwezesha kiwanda cha Tanzania Pharmacetical Industry (TPI) kilichopo Arusha ili kuzalisha dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI. Aidha, katika kuimarisha utendaji na uendelevu wa kiwanda cha viuadudu Kibaha, Serikali imenunua lita milioni 1.45 za viua dudu zenye thamani ya Shilingi bilioni 17.5 zilizosambazwa kwenye halmashauri 184 nchini kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa malaria.

38. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi, 2026 hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu za kipaumbele 382 ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeimarika kutoka asilimia 58 mwaka 2021/2022 mpaka asilimia 88.8 Machi 2026 sawa na ongezeko la asilimia 30. Mchanganuo wa ongezeko hilo katika ngazi mbalimbali za utoaji wa huduma ni kama

ifuatavyo: zahanati kutoka asilimia 69 hadi 88, vituo vya afya asilimia 68 hadi 88, hospitali za wilaya asilimia 72 hadi 90, hospitali za rufaa za mikoa asilimia 83 hadi 91, hospitali za kanda, maalum na taifa asilimia 58 hadi 91.

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti na Usimamizi wa Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imeendelea kuimarisha utendaji na ubora wa huduma hivyo kuwezesha kuendelea kushikilia cheti cha utambuzi wa umahiri katika mifumo ya udhibiti ubora wa dawa kwa vigezo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa ngazi ya tatu (Maturity Level 3). Hii inamaanisha kuwa, wananchi wameendelea kupata bidhaa za afya kwa ubora unaokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa.

## Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuajiri wataalam katika Sekta ya Afya ambapo jumla ya wataalam 53,633 wa kada mbalimbali wameajiriwa na kusambazwa

katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini katika kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi Machi 2026 na hivyo kufanya idadi ya watumishi katika Sekta ya Afya kufikia 182,430. Aidha, watumishi 9,039 waliajiriwa kwa mikataba ya muda mfupi kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato vya vituo husika vya kutolea huduma.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa wataalam bingwa na bingwa bobezi kwa ajili ya utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuanzisha **Programu ya Samia Health Super Specialization Scholarship** ambapo katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi Machi 2026, jumla ya wataalam 2,982 wamepata mafunzo katika fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ikilinganishwa na wataalam 961 waliofadhiliwa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 sawa na ongezeko la wataalam 2,021.

**Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote**

42. ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ilileta mapendekezo ya kutungwa kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote mbele ya Bunge lako Tukufu na kupitishwa mwezi Novemba, 2023. Kupitishwa kwa sheria hiyo kunawahakikishia wananchi kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha pindi watakapougua.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** masuala muhimu yaliyokamilishwa baada ya sheria hiyo kupitishwa ni pamoja na kanuni za utekelezaji wa sheria, mwongozo wa usimamizi na uendeshaji wa mfuko wa kugharamia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo, mwongozo wa utambuzi wa kaya maskini zitakazogharamiwa na Serikali, mwongozo wa rufaa wa huduma za afya na kitita cha mafao cha huduma muhimu kinachojumuisha huduma 372 kwa

kiwango cha uchangiaji cha Shilingi 150,000 kwa kaya ya watu wasiozidi sita kwa mwaka. Vilevile, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima nchini (TIRA) na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) zimefanya mapitio ya muundo na sheria zilizoanzisha taasisi hizo ili kuendana na utekelezaji wa sheria ya Bima ya Afya kwa Wote.

44. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ilianza rasmi usajili wa wanufaika wa Bima ya Afya kwa Wote kwa awamu ya kwanza mnamo tarehe 26 Januari, 2026 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ndani ya siku 100 tangu kuingia madarakani katika kipindi cha pili cha awamu ya sita. Hadi kufikia Machi 2026 Serikali imetoa kiasi cha **Shilingi bilioni 48.8** kwa ajili ya kugharamia kaya zisizo na uwezo kwa awamu ya kwanza. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji, kaya 172,297 zimefikiwa sawa na asilimia 62 ya lengo la kaya 276,004 na kufanya jumla ya wananchi waliosajiliwa kufikia 463,228 sawa na asilimia 38 ya lengo

la kufikia wananchi 1,206,319 na zoezi hilo linaendelea.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inakamilisha maboresho ya mfumo utakaowezesha usimamizi wa bima ya afya kwa ufanisi, udhibiti wa gharama katika ngazi zote na kuwezesha kuanza usajili wa awamu ya pili utakaohusisha wananchi kutoka katika kaya 589,772 zisizo na uwezo pamoja na wananchi wenye uwezo wa kujigharamia. Aidha, kabla ya kuanza uandikishaji wa wananchi kwa awamu ya pili kwenye kitita cha bima ya afya kwa wote, wananchi wenye uwezo kutoka sekta rasmi, binafsi na sekta isiyo rasmi wanaendelea kujiunga kwa utaratibu uliokuwepo

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali inaendelea kutoa elimu kwa umma na kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya, kwa kutumia mkakati na nyenzo za mawasiliano zilizoandaliwa kufikia makundi yote. Jukumu hili endelevu linatekelezwa kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi zote, hususan Mikoa na

Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambao ni kiungo muhimu katika kufikisha ujumbe sahihi, kubadilisha mitazamo ya jamii, kuhamasisha ushiriki, na kuhakikisha hakuna anayebaki nyuma. *Nipende kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2026, Serikali kupitia Wizara imefanya mikutano na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri zote, Wahariri na Waandishi wa Vyombo vya Habari vyote nchini ili kuwawezesha kuelewa kwa kina malengo ya Serikali, mwelekeo wa kisera na dhana ya bima ya afya kwa wote ili wawe washirika wa maendeleo katika kuifikisha dhana hii kwa wananchi.*

***"Ifahamike kuwa, Mafanikio haya ya Sekta ya Afya katika kipindi cha Awamu ya Sita si takwimu tu za majengo, vitanda, vifaa na huduma zilizoongezeka; ni simulizi ya maisha yaliyookolewa, matumaini yaliyorejeshwa na utu wa Mtanzania uliolindwa. Kama ambavyo Mwalimu***

***Nyerere aliamini kuwa maendeleo ya kweli ni maendeleo ya watu, kama Nelson Mandela alivyotufundisha kuwa heshima ya binadamu ndiyo msingi wa taifa huru, na kama Kwame Nkrumah alivyosisitiza kuwa uhuru lazima uambatane na uwezo wa kujijenga, Serikali imeonesha kwa vitendo kuwa afya bora ndiyo msingi wa maendeleo ya kweli. Hivyo, kila zahanati iliyojengwa, kila hospitali iliyoboreshwa, kila mama aliyepata huduma salama, na kila maisha yaliyookolewa ni ushahidi kwamba Tanzania inaendelea kujenga taifa lenye afya, usawa, utu na matumaini kwa vizazi vya sasa na vijavyo.***

## SEHEMU YA III: MAENEO MAHSUSI YA MSISITIZO

47. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuzingatia maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** wakati wa hotuba yake ya kuzindua Bunge hili, Wizara inaendelea kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini kwa kuweka mkazo katika maeneo mahsusi ambayo ni: kuboresha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya; kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili iweze kusomana na kupunguza muda mrefu ambao mteja anatumia kupata huduma.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kusaini Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote na usajili wa wanachama kuanza rasmi Januari 2026, hatua inayoendelea ni maboresho ya mifumo ya utoaji huduma, kuendelea kusajili wananchi wasio na uwezo

kupitia kaya na kuendelea kutoa elimu ya Bima ya Afya kwa wananchi ili kuwa na uelewa wa dhana ya bima ya afya na kujiunga na mifumo ya Bima ya Afya iliyopo nchini. Hatua hii ni ya mageuzi makubwa ya kihistoria ambayo yanaweka bayana ukweli kuwa afya si fadhila, si bahati, si upendeleo bali ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. ***Napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Bima ya Afya kwa Wote si mradi wa Wizara pekee bali ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kwa taifa na wananchi wote.***

***49. Mheshimiwa Spika,*** kufuatia agizo la **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** la kuimarisha uwezo wa nchi katika kuzalisha bidhaa za afya ili kufikia azma ya kujitosheleza kwa asilimia 80 ifikapo mwaka 2030, Wizara itaendelea kukiwezesha kikosi kazi maalum *cha Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce* (PIAT) kwa ajili ya kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vipya vya bidhaa za

afya nchini. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi pamoja na kuwawekea mazingira rafiki na wezeshi ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ardhi na miundombinu muhimu ili kuwavutia kuwekeza katika ujenzi wa viwanda kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha suala la kuimarisha viwanda vya ndani na suala la uwezeshaji wazalishaji wa ndani si maneno tu bali ni dhamira thabiti ya Serikali, Wizara imejipanga kuhakikisha MSD inanunua kwanza dawa zinazozalishwa ndani zilizokidhi vigezo vya TMDA kabla ya kwenda kununua nje ya nchi. Hatutarajii kuona dawa kama Paracetamol, metronidazole, ciprofloxacini, erythromycin za maji na vidonge, maji tiba na nyingine zinazozalishwa kwa utoshelevu nchini zinaagizwa kutoka nje. Lazima tuchukue hatua za ukweli na uwazi ili kuhamasisha na kulinda uzalishaji wa dawa nchini.

***"Nitumie nafasi hii kuwaalika wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa hii ya kuwekeza katika viwanda vya bidhaa za afya ili kuunga mkono juhudi na maono ya Mheshimiwa Rais ya kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya kutoka nje ya nchi kwani dawa ni tiba, dawa ni ulinzi na dawa ni usalama kwa wananchi na Taifa kwa ujumla".***

***51. Mheshimiwa Spika,*** tunafahamu kuwa mifumo ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha huduma bora zinatolewa kwa wananchi. Ili kuhakikisha hilo, Wizara itaendelea kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika Sekta ya Afya inasomana na kubadilishana taarifa pamoja na kuwezesha kutuma, kupokea, kutunza taarifa za wagonjwa katika hospitali za umma na binafsi, kutoa rufaa kidigitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo mingine inayohitaji taarifa mbalimbali. Kusimamia matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kuleta ufanisi ni kutafsiri kwa vitendo

maelekezo ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** ya kutaka mifumo ya Serikali kuwa michache na yenye kusomana.

***52. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ipo kwenye hatua za awali za uanzishaji wa chombo cha kutoa **ithibati ya ubora wa huduma** katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma na vya binafisi. Hatua hii itaimarisha ubora wa huduma za Afya nchini kwa kuzingatia uwekezaji uliofanywa na Serikali kwenye vituo na hivyo kuwezesha huduma zinazotolewa katika vituo vyetu kutambulika kikanda na kimataifa. Kupitia chombo hiki, Wizara imedhamiria kutoa huduma bora za afya kwa wananchi ikiwemo kuwapunguzia muda wa mgonjwa kusubiri huduma kwenye vituo pamoja na kuhakikisha matumizi ya lugha zenye staha kwa wagonjwa. Vilevile, kupitia ithibati zitakazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya zitawezesha kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi na hivyo kuimarisha utekelezaji wa dhana ya tiba utalii.

Malengo yetu kama Wizara ni kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya rufaa ya Mkoa hadi Taifa vinapata ithibati ya ubora ifikapo 2030.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuhitimisha eneo hili, maeneo mahsusi ya msisitizo yanaonesha wazi kuwa safari ya Sekta ya Afya katika kipindi kijacho haitajengwa tena kwa kuongeza huduma pekee, bali kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa endelevu, zenye ubora, zinazofikiwa na kila mwananchi na zinazolinda utu wa kila mgonjwa. Bima ya Afya kwa Wote inaleta usawa na inalinda familia dhidi ya umaskini unaotokana na gharama za matibabu. Aidha, uzalishaji wa dawa na bidhaa za afya nchini unapelekea kujitegemea, kuongeza ajira na kuimarisha usalama wa Taifa. Vilevile, mifumo ya TEHAMA inaongeza ufanisi katika utendaji, inapunguza urasimu na inaharakisha maamuzi ya kitabibu. Pia, ithibati ya ubora inaleta heshima, uwajibikaji na ushindani wa huduma zetu kitaifa, kikanda na kimataifa. Falsafa

inayotuongoza ni rahisi lakini yenye maana kubwa.

***"Napenda kusisitiza kuwa, Afya ya mwananchi si gharama, ni uwekezaji; dawa si bidhaa ya kawaida, ni tiba, ulinzi na usalama; taarifa za mgonjwa si makaratasi, ni maisha yanayohitaji uamuzi wa haraka; na ubora wa huduma si anasa, ni haki ya msingi ya Mtanzania. Hivyo, tunaposema tunaboresha sekta ya afya, tunamaanisha tunajenga mfumo unaolinda maisha, unaozuia umaskini, unaotumia teknolojia kuongeza ufanisi, unaoweka heshima ya mgonjwa katikati ya huduma, na unaoimarisha uwezo wa Taifa kujitegemea. Kwa maneno machache, haya ndiyo mageuzi tunayoyasimamia: afya iwe haki, dawa zizalishwe ndani ya nchi, huduma ziwe za kidigitali, vituo viwe na ubora unaotambulika, na kila mgonjwa ahudumiwe kwa heshima. Huu si mpango wa kawaida wa kisekta; ni ahadi ya Taifa kwa watu wake kwamba***

***hakuna Mtanzania atakayeachwa nyuma katika kupata huduma bora za afya, na kwamba Tanzania yenye afya bora ndiyo msingi wa Tanzania yenye uchumi imara, utu, matumaini na maendeleo endelevu."***

## SEHEMU YA IV: MWENENDO WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake, Wizara imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2050), Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa Taifa (2021/2022– 2025/2026), Sera ya Afya ya Mwaka 2007, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya 2025, Mpango Mkakati wa Tano wa Sekta ya Afya - HSSP V (2021/2022 – 2025/2026), Mpango Mkakati wa muda wa kati wa Wizara wa mwaka (2021/2022 – 2025/2026), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs - 2030) pamoja na makubaliano ya kimataifa na kikanda yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika bajeti ya mwaka 2025/2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara nyingine, Idara na Taasisi za Serikali, Wakala za Serikali na Wadau wa Maendeleo ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye

lengo la kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe;
ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa;
iii. Kuimarisha mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote;
iv. Kuendelea kufanya tafiti na kuhimiza matumizi ya matokeo ya tafiti hizo kwa maeneo ya kimkakati;
v. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga;
vi. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;

vii. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini;
viii. Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;
ix. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko; na
x. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu.

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026**

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara na Taasisi zilizo chini yake ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 819,977,862,602.14** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 74,207,303,307.00** ni kutoka Makao Makuu ya Wizara (ikiwemo Hospitali za Kanda, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma), **Shilingi 153,792,696,693.00** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na **Shilingi**

**591,977,862,602.14** ni kutoka Hospitali Maalum, Hospitali ya Taifa pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekusanya jumla ya kiasi cha **Shilingi 593,852,818,278.97** sawa na asilimia **72.42** ya lengo la kukusanya maduhuli ya **Shilingi 819,977,862,602.14**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 55,433,495,972.85** sawa na asilimia **74.70** ya makadirio kimekusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, kiasi cha **Shilingi 111,089,490,230.85** sawa na asilimia **72.23** kimekusanywa kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha **Shilingi 427,329,832,075.27** sawa na asilimia **72.19** kimekusanywa kutoka katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

## Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha

**Shilingi 1,763,541,235,000.00** ili kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 626,433,136,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida (mishahara ni **Shilingi 475,418,119,000.00** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 151,015,017,000.00)** na **Shilingi 1,137,108,099,000.00** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (fedha za ndani ni **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 347,649,490,000.00**).

**Mapokezi ya Fedha**

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha **Shilingi 1,107,155,251,269.36** kimepokelewa sawa na asilimia **63** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 473,128,037,804.21** ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia **76** (mishahara ni **Shilingi 368,072,592,445.00** sawa na asilimia **77** na matumizi mengineyo ni **Shilingi 105,055,445,359.21** sawa na asilimia **70**) na kiasi cha **Shilingi**

**634,027,213,465.15** sawa na asilimia **56** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo (fedha za ndani ni **Shilingi 403,278,048,926.28** sawa na asilimia **51** na fedha za nje ni **Shilingi 230,749,164,538.87** sawa na asilimia **66**).

***60. Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, fedha za nje zilizopokelewa ni kutoka Mfuko wa Dunia (Global Fund) kwa ajili ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria, GAVI kwa ajili ya huduma za utoaji chanjo nchini, Susan Thompson Buffet Foundation na Benki ya Dunia, kwa ajili ya uwekezaji wa afya ya mama na mtoto, Mfuko wa Afya wa Pamoja (HBF) kwa ajili ya uimarishaji huduma za afya ikiwemo huduma za damu salama, Shirika la Kimataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF), Nutrition International na UNFPA kwa ajili ya huduma za lishe pamoja na huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, asasi zisizo za kiraia na wadau wengine.

## SEHEMU YA V: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA

### Udhibiti wa Magonjwa Yasiyoambukiza

61. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI na wadau mbalimbali inaendelea kuimarisha huduma za afya nchini ikiwemo udhibiti wa magonjwa yasiyoambukiza ambapo takwimu za magonjwa hayo zinaonesha kuwa kuna ongezeko la mzigo wa magonjwa yasiyoambukiza nchini, hali inayoendelea kuiweka Sekta ya Afya katika hitaji la kuimarisha afua za kinga, uchunguzi na matibabu. Kwa mujibu wa taarifa ya tathmini ya National Health Accounts (NHA) ya mwaka 2024 imeonesha kuwa ugharamiaji wa magonjwa yasiyoambukiza umeongezeka kwa asilimia 38 kutoka **shilingi trilioni 1.3** mwaka 2023 hadi **shilingi trilioni 1.8** mwaka 2024.

## Huduma za Kisukari na Shinikizo la Damu

62. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha uratibu na utekelezaji wa afua za magonjwa ya kisukari, shinikizo la damu na magonjwa sugu ya mfumo wa upumuaji. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kumeanzishwa kliniki mpya 130 za huduma za kisukari na shinikizo la damu na hivyo kufanya jumla ya kliniki hizo kufikia 168 kutoka 38 zilizokuwepo katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Kliniki hizo zilipatiwa dawa, vifaa tiba na mafunzo kwa watumishi ili kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma. Aidha, huduma za kinga na uchunguzi ziliboreshwa kupitia upimaji wa magonjwa yasiyoambukiza mahali pa kazi, utoaji wa elimu kwa jamii, matembezi ya Kitaifa ya kuhamasisha mazoezi, pamoja na kampeni za uelimishaji kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini.

63. ***Mheshimiwa Spika***, uwezo wa rasilimali watu umeimarishwa kupitia mafunzo kazini kwa watoa huduma katika vituo vya afya na

Hospitali za Wilaya, pamoja na mafunzo ya kitaalamu kwa madaktari bingwa na wauguzi kuhusu huduma za kisukari, ikiwemo matibabu ya vidonda vitokanavyo na ugonjwa wa kisukari. Watoa huduma wa ngazi ya jamii na watu wanaoishi na magonjwa yasiyoambukiza pia walijengewa uwezo katika maeneo ya udhibiti wa magonjwa, lishe, mazoezi na kupunguza unyanyapaa. Katika kuimarisha matumizi ya takwimu, Wizara imeendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa taarifa za magonjwa ya kisukari na shinikizo la damu katika ngazi ya jamii.

**Huduma za Figo**

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za figo nchini kwa kupanua upatikanaji wa huduma za kuchuja damu ambapo jumla ya wagonjwa 3,342 wamehudumiwa. Aidha, katika kipindi hicho, hospitali tatu (3) zimeanza kutoa huduma ya kuchuja damu; hospitali hizo ni hospitali ya rufaa ya mkoa Mawenzi, hospitali ya rufaa ya

kanda ya kusini Mtwara na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete na kufanya jumla ya vituo vinavyotoa huduma hiyo kufikia 74. Kati ya vituo hivyo, vituo 28 ni vya umma na 46 ni vituo binafsi. Vituo vya umma vinavyotoa huduma za kuchuja damu ni Hospitali ya Taifa Muhimbili Upanga na Mloganzila, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, hospitali 16 za Rufaa za Mikoa, Kituo cha Afya UDOM, Hospitali ya Jeshi Lugalo na Hospitali ya Emilio Mzena.

65. ***Mheshimiwa Spika***, uwezo wa kiufundi umeimarishwa kupitia mafunzo maalum kwa wahandisi wa vifaa tiba kutoka Hospitali 13. Mafunzo hayo yalilenga kuboresha matumizi, matengenezo na uendeshaji wa mashine za kusafisha damu, hivyo kuchangia katika kuboresha huduma. Vilevile, Wizara imekamilisha na kuwasilisha waraka wa mapendekezo ya sheria ya huduma za damu na upandikizaji wa viungo vya binadamu katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, ikiwa ni hatua muhimu katika kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi wa huduma za figo nchini.

**Huduma za Saratani**

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ubora wa **huduma za saratani**, Wizara imeandaa mwongozo wa Kitaifa wa taratibu sanifu za uendeshaji wa bodi za kitaalamu za saratani, hatua iliyolenga kuboresha maamuzi ya kitabibu na usimamizi wa wagonjwa. Aidha, Wizara imepanua huduma za matibabu ya saratani ikijumuisha uchunguzi wa saratani kwenye hospitali zote za rufaa za mikoa, tiba dawa kwenye hospitali ya rufaa ya mkoa Mount Meru na kuendelea kutoa huduma za tiba mionzi na upasuaji katika hospitali za kanda pamoja na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya kitaifa ya matibabu ya saratani.

67. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara inaendelea kupanua huduma za Saratani nchini kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma hizo katika kanda za nyanda za juu kusini Mbeya, Kaskazini – KCMC, kanda ya ziwa Bugando na kanda ya Kusini – Mtwara ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi. Kupitia mtambo maalum wa kisasa ujulikanao

kama Cyclotron, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road imeanza uzalishaji wa dawa za uchunguzi na kutibu saratani nchini. Aidha, uwepo wa mtambo huo na uzalishaji wa dawa nchini umewapunguzia wagonjwa muda wa kusubiri huduma.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeimarisha uratibu na usimamizi wa rejesta za saratani katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza, Dodoma na Mbeya kwa kufanya mafunzo ya ukusanyaji, uchakataji na uhakiki wa ubora wa takwimu, usahihishaji wa makosa ya usajili, pamoja na kuendelea na zoezi la kuoanisha mifumo ya CanReg5 na DHIS2. Uwezo wa wataalam wa rejesta umeimarishwa kupitia programu ya kimataifa ya GICR e-learning ambapo wasajili watano (5) walipata vyeti vya kitaalam vya kimataifa.

**Huduma za Afya ya Akili**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia na kijamii ziliendelea kutolewa katika vituo vya kutolea

huduma za afya ngazi ya msingi nchini, ambapo jumla ya wateja 254,932 walihudumiwa katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026. Huduma hizo zilijumuisha matibabu ya kifafa, skizofrenia, matatizo ya tabia, pamoja na utegemezi wa pombe na dawa za kulevya. Aidha, katika kipindi hiki, vituo 16 vya matibabu ya waraibu wa dawa za kulevya vilitoa huduma kwa wateja 17,807 na upatikanaji wa dawa za afya ya akili katika vituo umefikia wastani wa asilimia 75.

**70.** ***Mheshimiwa Spika*****,** mafunzo pia yalitolewa kwa wataalam wa afya ngazi ya jamii, yakihusisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii 50 na wahudumu wa Afya 10 kwa lengo la kuwawezesha kutambua na kutoa huduma kwa watu wenye changamoto za msongo wa mawazo na sonona katika jamii husika ambapo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, wanajamii 1,709 wamepimwa na 1,362 wamegundulika kuwa na sonona na wapo kwenye tiba. Vilevile, elimu kuhusu ugonjwa wa kifafa ilitolewa kwa jamii kupitia maadhimisho ya Siku ya kifafa Duniani pamoja

na mkutano wa EpiNA na kufikia watu 150. Mafunzo kwa watoa huduma za afya kuhusu tiba na usimamizi wa wagonjwa wa kifafa yalitolewa kwa washiriki 22 pamoja na kutumia vyombo vya habari mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu kifafa na magonjwa ya afya ya akili kwa ujumla. Hali kadhalika elimu ya afya ya akili kuhusu usonji imetolewa katika kilele cha siku ya usonji duniani ambapo watu 247 walifikiwa.

***"Nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi na kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya kupima magonjwa ya afya ya akili hususan hali ya msongo wa mawazo na sonona inayoonekana kuongezeka ili kuepusha madhara zaidi kwani hali hii inatibika".***

**Huduma za Sikoseli na Himofilia**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kupanua huduma za uchunguzi na matibabu ya ugonjwa wa sikoseli kutoka hospitali ya taifa hadi katika ngazi ya mkoa. Katika kipindi

cha Julai 2025 hadi Machi 2026, watoto 17,245 walipimwa. Kati yao 369 waligundulika kuwa na ugonjwa wasikoseli na 2,500 walibainika kuwa na vinasaba vya ugonjwa huo. Aidha, jumla ya wagonjwa 42,564 walihudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Vilevile, elimu ya sikoseli ilitolewa kwa wananchi zaidi ya 29,000 wakiwemo vijana, walimu, viongozi wa dini, waandishi wa habari na makundi maalum kama vijana waliopo kambini, hatua iliyochangia kuongeza uelewa na kupunguza unyanyapaa. Pia, usimamizi shirikishi ulifanyika katika mkoa wa Mwanza na Tabora kwa ajili ya kuangalia upimaji wa watoto chini ya miaka mitano kuhusu ya ugonjwa wa sikoseli ambapo jumla ya vituo 25 vilitembelewa.

**Afya ya Kinywa na Meno**

72. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuboresha huduma za afya za kinywa na meno kwa kuratibu ununuzi na usambazaji wa viti maalum vya matibabu ya kinywa na meno

26 na kufanya jumla ya viti maalum vya matibabu ya kinywa na meno kufikia 900. Aidha, Wizara imenunua mashine kubwa za mionzi (2D-OPG) saba (7) na mashine ndogo za mionzi (Periapical X-ray) tisa (9) na kufanya jumla ya mashine ndogo za mionzi kufikia 396. Mashine hizo zilipelekwa katika hospitali ya kanda ya Benjamin Mkapa, hospitali za rufaa za mikoa za Mawenzi na Amana, Hospitali za Halmashauri za Itigi, Dodoma Jiji, Sengerema na Msalala, Vituo vya Afya vya Ilazo, Ihumwa, Ilolangulu na Uhuru, Muriet, Magugu, Hospitali ya Manispaa ya Shinyanga, Hospitali ya Wilaya ya Itilima na Nanyumbu.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Wagonjwa 680,995 walihudhuria kwenye vituo vinavyotoa matibabu ya kinywa na meno. Wagonjwa 459,238 walikuwa na tatizo la kuoza meno, wagonjwa 68,474 walikuwa na tatizo la magonjwa ya fizi, wagonjwa 17,294 walikuwa na tatizo la jino gego kunasa kwenye mfupa, wagonjwa 17,035 waligundulika na uvimbe wa kinywa na meno, wagonjwa 175

waligundulika na saratani ya kinywa na wagonjwa 118,779 waligundulika kuwa na matatizo mengine ya kinywa na meno. Aidha, wagonjwa 172,494 walizibwa meno, wagonjwa 284,691 waling'olewa meno, wagonjwa 35,829 walifanyiwa matibabu ya kusafishwa meno, wagonjwa 14,946 walifanyiwa upasuaji mdogo wa magonjwa ya kinywa na meno, wagonjwa 914 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa magonjwa ya kinywa na 172,121 walipatiwa matibabu mengine.

**74. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa mafunzo ya afya ya kinywa na meno kwa watoa huduma za afya 1,289 ambapo kati yao, wauguzi 140, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,010 na tabibu meno 139 katika mikoa ya Morogoro, Kagera, Ruvuma na Mwanza.

***"Nitumie fursa hii kuwajulisha waheshimiwa wabunge wenzangu pamoja na wananchi wote kuwa,***

***huduma za kinywa na meno zimeboreshwa sana nchini. Hivyo niwaombe kuwahi mapema katika vituo vinavyotoa huduma za afya ili kupata huduma inayostahili kwani dawa ya jino sio kung'oa pekee".***

**Huduma za Macho**

***75. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za macho nchini kupitia kambi za huduma za macho na huduma za upasuaji katika mikoa 15 na kutoa elimu kwa umma. Jumla ya watu 51,940 walifanyiwa uchunguzi wa afya ya macho, kati yao watu 17,697 walifanyiwa upasuaji, 17,715 walipatiwa tiba dawa na 10,239 walipewa miwani na 6,289 walipatiwa huduma nyingine za macho. Aidha, huduma hizo zimechangia kupunguza mzigo wa upofu unaozuilika na matatizo ya kuona yanayorekebishika kwa miwani. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilinunua kifaa maalum kwa ajili ya uchunguzi wa mapema wa saratani ya macho kwa watoto chini ya miaka mitano, hatua iliyoboresha uwezo wa

uchunguzi na rufaa kwa watoto chini ya miaka mitano. Aidha, Wizara iliratibu maadhimisho ya Siku ya Macho Duniani kitaifa yaliyoambatana na kampeni za uelimishaji zilizofanyika kupitia hospitali, shule na kambi za macho na kufikia zaidi ya watu milioni mbili.

**Huduma za Utengamao, Wazee na Tiba Shufaa.**

76. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imekamilisha orodha ya kitaifa ya msingi ya kiteknolojia saidizi. Wizara imekamilisha ujumuishwaji wa mfumo wa ukusanyaji takwimu za utengamao (Rehab HMIS) na viashiria 17 vya kufuatilia utoaji wa huduma za afya kwa wazee kwenye mifumo ya kieletroniki ya Afya-eHMIS na GoTHOMIS inayotumika kukusanyia takwimu kwenye hospitali za rufaa za Mikoa na vituo vya afya ngazi ya msingi. Aidha, Wizara inaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za tiba shufaa nchini, ambapo watumishi nane (8), wafamasia wawili (2), wauguzi wawili (2),

madaktari wawili (2) na maafisa ustawi wa jamii wawili (2) kutoka hospitali mbili (2) za rufaa za mikoa wamepata mafunzo ya msingi ya utoaji wa huduma za tiba shufaa.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watalaam ili kutoa huduma zinazokidhi mahitaji ya afya kwa wazee ambapo jumla ya watalaam 80 katika vituo vya afya ngazi ya msingi wamepata mafunzo namna ya kutoa huduma za afya kwa wazee. Aidha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, imeongeza klabu za afya za wazee kutoka 32 hadi 263; Tanga (64); Mwanza (40); Morogoro (128); Kigoma (18) na Shinyanga (13).

78. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeweza kupima usikivu kwa watoto wachanga 2,112. Kati yao, watoto 350 sikio moja au yote mawili yalikuwa na changamoto ya kupoteza usikivu. Aidha, katika Siku ya Kimataifa ya Masikio na Usikivu mwaka 2026, Wizara kwa kushirikiana

na Wadau iliweza kuwafikia wananchi 8,500 na kutoa elimu kuhusu masikio na usikivu. Jumla ya mashine za kutibia masikio 23 zimenunuliwa na kusambazwa katika hospitali 23 za mikoa za Tumbi, Mt. Meru, Manyara, Mawenzi, Morogoro, Amana, Mwananyamala, Dodoma, Songwe, Mbeya, Sumbawanga, Singida, Maweni, Katavi, Kitete, Songea, Njombe, Ligula, Sokoine, Bukoba, Tanga na Hospitali za Kanda za Chato na Mbeya. Aidha, mashine 15 za kupima usikivu zimenunuliwa na kusambazwa katika hospitali za rufaa za mikoa za Ligula, Sokoine, Morogoro, Amana, Mwananyamala, Mt. Meru, Manyara, Mawenzi, Songwe, Mbeya, Sumbawanga, Njombe, Katavi, Kitete pamoja na hospitali ya kanda ya Chato. Vilevile, jumla ya watalaam 50 kutoka vituo vya afya ya msingi wamepata mafunzo namna ya kuhudumia watoto wachanga na watoto wadogo wenye maambukizi ya masikio kwa kutumia uwiano kwa njia ya masafa.

***"Mheshimiwa Spika, mapambano dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza yanahitaji si tiba tu, bali kinga, mabadiliko ya***

***mtindo wa maisha na uelewa wa pamoja kwa jamii. Serikali itaendelea kuwekeza katika afua za kinga na uchunguzi wa mapema katika kudhibiti ukuaji wa magonjwa yasiyoambukiza ili kuepuka gharama kubwa za matibabu kwa wananchi na Serikali".***

## Udhibiti wa Magonjwa ya Kuambukiza

### Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI, Homa ya Ini na Magonjwa ya Ngono.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mpango Jumuishi wa kudhibiti UKIMWI, Magonjwa ya Ngono na Homa ya Ini, imeendelea kutoa huduma za tiba na matunzo kwa magonjwa ya VVU/UKIMWI, homa ya ini na magonjwa ya ngono pamoja na kuhamasisha wananchi kupima na kutambua hali zao za maambukizi.

### Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Takwimu zinazokusanywa kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya vinavyotoa huduma za matunzo na matibabu kwa Watu Wanaoishi

na Virusi vya UKIMWI (WAVIU) zinaonesha kuwa, hadi kufikia Machi 2026, watu 1,624,907 kati ya 1,700,000 wanaokadiriwa kuishi na maambukizi ya VVU walikuwa wanatambua hali zao za maambukizi ikiwa ni sawa na asilimia 95.7 ya watu wanaokadiriwa kuishi na Virusi vya UKIMWI nchini (95 ya kwanza). Watu 1,609,078 kati ya waliopima na kutambua hali zao za maambukizi ya VVU walikuwa wameanza kutumia dawa za kufubaza Virusi vya UKIMWI, hii ikiwa ni sawa na asilimia 94.7 (95 ya pili). Aidha, jumla ya WAVIU 1,343,112 wanaotumia dawa za ARV walifanya vipimo vya kujua wingi wa Virusi vya UKIMWI, ambapo WAVIU 1,317,593 sawa na asilimia 98.1 walifubaza makali ya Virusi vya UKIMWI (95 ya tatu). *Jedwali Na 1* linaonesha ufafanuzi huo.

### ***Jedwali Na. 1: Mafanikio Kuelekea Kufikisha Malengo ya 95-95-95***

| **Na.** | **Kiashiria** | **Julai 2024 hadi Machi 2025** | **Julai 2025 hadi Machi 2026** | **Hali ya 95-95-95** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanaokadiriwa kuwa na maambukizi (People Living with HIV/AIDS -PLHIV) | 1,700,000 | 1,700,000 | **95 ya kwanza** |
| | Wanaotambua hali zao za maambukizi | 1,530,227 | 1,624,907 | |
| | Asilimia ya wanaotambua hali zao (on care) | **90** | **95.7** | |
| 2 | Wenye maambukizi na wameanza dawa | 1,500,212 | 1,609,078 | **95 ya pili** |
| | Asilimia ya walioanza dawa (on ART) | **98** | **94.7** | |
| 3 | Idadi ya WAVIU waliofanya vipimo (VL test) | 874,944 | 1,343,112 | **95 ya tatu** |
| | Idadi WAVIU ambao makali ya VVU yamefubazwa | 858,272 | 1,317,593 | |
| | Asilimia ya waliofubazwa makali (VL<1000) | **98** | **98.1** | |

***81. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa huduma kwa WAVIU zinasogezwa karibu na jamii, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, imeendelea kuhakikisha kila kituo cha kutolea huduma za

afya kina uwezo wa kutoa huduma kwa watu wanaoishi na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya vituo vinavyotoa huduma ya tiba na matunzo vimeongezeka kutoka 7,994 hadi 8,203 sawa na asilimia 74.4 ya vituo 11,030 vyenye huduma ya utambuzi wa VVU. Lengo ni kufikia asilimia 95 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya utambuzi kwa WAVIU ifikapo mwaka 2030.

**Huduma ya Dawa Kinga kwa Makundi yaliyo kwenye Mazingira Hatarishi**

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa kinga kwa makundi yaliyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa au kuambukiza VVU ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya watu 121,957 walipewa dawa kinga. Makundi lengwa ni wanaume na vijana wa kike na kiume walio katika hatari zaidi ya maambukizi ikijumuisha wachimbaji madini, madereva wa masafa marefu, wavuvi, wanaojidunga, vijana walio katika mazingira

hatarishi na wanaojihusisha na biashara haramu ya ngono. Aidha, mikakati mahsusi imepangwa kutekelezwa katika Mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya ambayo ina kiwango cha juu cha maambukizi ya VVU. Baadhi ya mikakati hiyo ni; kuhakikisha uimarishaji wa afua ya tohara kwa wanaume, utoaji wa elimu ya kinga na maambukizi kwa vijana balehe na wajawazito.

**Kuzuia Maambukizi ya Magonjwa ya Ngono na VVU kutoka kwa Mama kwenda kwa Mtoto**

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali ili kuhakikisha wajawazito wanapimwa maambukizi ya VVU wanapohudhuria kliniki na hata baada ya kujifungua, lengo likiwa ni kuhakikisha mtoto aliyeko tumboni anakingwa dhidi ya maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto, ikiwa mama atakuwa ameambukizwa. Huduma hizo huenda sambamba na kupima na kutibu maambukizi ya Kaswende na Virusi vya Homa ya Ini aina B

kwa wajawazito ili kuwakinga watoto dhidi ya maambukizi hayo kabla ya kuzaliwa.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wajawazito 2,218,640 walihudhuria kliniki na kati yao 2,080,819 walipimwa maambukizi ya VVU kwa mara ya kwanza wakati wa hudhurio la kliniki na wajawazito 11,445 sawa na asilimia 0.6 walibainika kuwa na maambukizi. Aidha, watoto 23,023 wenye umri wa miezi 18 kati ya watoto 24,998 waliotarajiwa, walipimwa maambukizi ya VVU na kati yao 1,197 walithibitika kuwa na maambukizi. Aidha, jumla ya wajawazito 1,995,822 sawa na asilimia 90 ya waliohudhuria kliniki walifanyiwa kipimo cha kaswende. Kati yao wajawazito 8,684 sawa na asilimia 0.4 walibainika kuwa na maambukizi ya kaswende na 8,598 sawa na asilimia 99 walianzishiwa matibabu.

***"Kwa takwimu hizo nichukue nafasi hii kuwasihi wananchi kuhakikisha wajawazito wanahudhuria kliniki mara***

***wanapojigundua kuwa wajawazito na kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kupata huduma stahiki za kinga dhidi ya magonjwa ya ngono na maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto na kupata matibabu mapema".***

**Huduma za Magonjwa ya Homa ya Ini**

***85. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa huduma za kinga na tiba dhidi ya homa ya ini aina ya B kwa kuhakikisha huduma hizo zinakuwa jumuishi na kutolewa katika ngazi ya afya ya msingi na rufaa. Huduma za chanjo zilianza kutolewa kwa watoto wote waliozaliwa mwaka 2002, hivyo nguvu kubwa imekuwa ikielekezwa kwa wananchi waliozaliwa kabla ya mwaka 2002 kwa kufanyiwa uchunguzi na kutoa chanjo kwa wanaokidhi vigezo na matibabu kwa wanaobainika kuwa na maambukizi.

***86. Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa watumishi wa afya ni sehemu ya kundi lililopo katika

hatari kubwa ya kupata maambukizi ya virusi vya homa ya ini aina ya B, Serikali imendelelea kuhakikisha watumishi wa afya wanapata chanjo hiyo ili kuwakinga. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya watumishi wa afya 13,646 sawa na asilimia 39.7 wamekamilisha chanjo zote tatu za homa ya ini aina ya B.

***"Nitoe rai kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kufanya uchunguzi na kupata chanjo ya homa ya ini aina ya B pamoja na kuwaomba waheshimiwa wabunge kujitokeza na kuwahamasisha wananchi kupima, kupata chanjo kwa wanaokidhi vigezo na matibabu kwa watakaobainika kuwa na maambukizi".***

***87. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imepokea maoni na michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge na kamati ya kudumu ya afya na masuala ya UKIMWI kuhusu mapambano dhidi ya homa ya ini. Katika eneo hili, Mheshimiwa Erick Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa amekuwa mstari wa mbele

kwenye kuhamasisha utoaji wa chanjo na tiba dhidi ya ugonjwa huu na Wizara inatambua jitihada na mchango wake na tunamhakikishia ushirikiano katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini.

## Mapambano dhidi ya Kifua Kikuu na Ukoma

88. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanikisha kuibua jumla ya visa 41,473 vya kifua kikuu, ikiwa ni sawa na asilimia 85 ya lengo la kuibua visa 48,792 kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ambapo visa 125 vilikuwa vya kifua kikuu sugu. Aidha, Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Arusha, Kilimanjaro, Mwanza, Manyara na Tabora imechangia wagonjwa wa Kifua Kikuu kwa asilimia 50 ya wagonjwa wote walioibuliwa nchini. Mikoa ya Katavi, Rukwa, Unguja, Kigoma na Pemba ilikuwa na idadi ndogo zaidi ya wagonjwa walioibuliwa. Kwa upande wa kifua kikuu sugu, Mikoa ya Dar es Salaam, Lindi, Tabora, Mbeya, Mwanza, Arusha, Kagera na Morogoro ilichangia asilimia 63 ya wagonjwa na Mikoa

ya Songwe, Singida, Pemba, Rukwa na Pwani hawakuwa na wagonjwa wa kifua kikuu sugu.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuchukua hatua za dhati ili kuongeza kasi ya uibuaji wa wagonjwa wa kifua kikuu nchini kwa mikoa ambayo imeonesha kiwango kidogo cha kuibua wagonjwa ikilinganishwa na malengo ya uibuaji wa wagonjwa uliowekwa katika mikoa hiyo. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na; kuongeza hamasa ya uelewa na uthubutu wa wananchi kuchunguzwa na kupimwa vimelea vya ugonjwa huo katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na jamii kwa kutumia huduma mkoba za kifua kikuu na kupitia kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na huduma mkoba za kliniki tembezi zenye uwezo wa kutoa huduma za uchunguzi na ugunduzi kwa magonjwa ya kifua kikuu na magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa katika maeneo yenye makundi hatarishi ya kuambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu.

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wagonjwa 77 waliibuliwa kupitia huduma za mkoba za kliniki tembezi.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya visa 755 vya ukoma viliibuliwa nchini sawa na asilimia 95.3 ya lengo la kuibua wagonjwa 792. Mikoa iliyoibua visa vingi ni pamoja na Morogoro, Lindi, Tanga, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Kigoma na Geita. Mikoa ambayo haikuwa na visa vipya vya wagonjwa ni Arusha, Iringa, Manyara na Njombe. Wizara imeendelea kuimarisha mikakati ya kutoa elimu kuhusu ugonjwa wa ukoma kwa kushirikisha jamii na wadau katika kuibua visa vipya na kutoa matibabu kwa wakati.

## Mapambano Dhidi ya Malaria

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kufanya ugawaji wa vyandarua kwa awamu kwenye kaya kupitia kampeni katika mikoa yenye maambukizi ya juu na ya kati. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara

imesambaza jumla ya vyandarua 4,567,179 vyenye viuatilifu ambapo vyandarua 1,236,294 vimesambazwa kwenye kaya 454,595 za halmashauri saba (7) za Mkoa wa Pwani (Chalinze DC, Kibaha DC, Kibiti DC, Kisarawe DC, Rufiji DC, Mafia DC, na Mkuranga DC) na vyandarua 3,330,885 vilisambazwa kwa wajawazito na watoto wa umri chini ya mwaka mmoja kupitia vituo vya kutolea huduma za afya kwenye halmashauri zote 184 nchini.

**93. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa jumla ya Shilingi bilioni 5.5 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 1.5 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa lita 125,000 za viuadudu vya kibaiolojia kutoka katika kiwanda cha Tanzania Biotech Product Limited (TBPL) kilichopo wilayani Kibaha mkoani Pwani na Shilingi bilioni 4 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa pampu 16,000 kwa ajili ya kuziwezesha halmashauri kunyunyizia viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ili kuua mbu waenezao malaria na magonjwa mengine yaenezwayo na mbu. Wizara

imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya mikoa na halmashauri ili kuwajengea uwezo wataalam wa ngazi hizo katika kutekeleza afua ya unyunyiziaji wa viuadudu vya kibaiolojia kwenye mazalia ya mbu.

94. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha malengo ya "Zero Malaria ifikapo 2030" yanafikiwa, Wizara imenunua jumla ya dozi 1,262,490 za dawa mseto (ALu), vitepe 15,015,250 vya kupimia malaria, vichupa 1,063,327 vya dawa ya sindano ya Artesunate, vyandarua 2,089,473, vidonge 1,460,700 vya SP na vidonge 26,600 vya primaquine. Usambazaji wa bidhaa hizo unaendelea kufanyika kulingana na mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya na kwa kuzingatia afua zilizokusudiwa katika maeneo mbalimbali. Katika kuboresha uagizaji wa bidhaa za malaria kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, Wizara imeendelea kufuatilia na kutatua changamoto za kimfumo na kuwawezesha watoa huduma kufanya uagizaji wa bidhaa hizo kwa kuzingatia idadi halisi ya watumiaji wa bidhaa. Aidha, katika kipindi hiki

Serikali imeagiza jumla ya dozi 2,470,260 za ALu zitakazotosheleza matumizi ya miezi 7 na vichupa 500,000 vitakavyotosheleza matumizi ya miezi 17.

***95. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya utafiti wa kuangalia kiwango cha maambukizi ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano na wanafunzi wa shule za msingi wa miaka mitano (5) hadi 16. Utafiti huo umefanyika katika halmashauri zote 184 nchini ambapo, jumla ya watoto 66,801 wa shule za msingi na watoto 8,828 wa umri chini ya miaka mitano walipimwa malaria kwa kutumia kipimo cha haraka cha malaria ili kubaini kiwango cha maambukizi na wale waliokutwa na maambukizi walipatiwa matibabu kwa kutumia dawa ya ALu. Malengo ya utafiti huo ni kupima hali ya utekelezaji wa afua za malaria katika jamii na kujipima kama tumeweza kushusha kiwango cha maambukizi ya malaria kwa watoto chini ya miaka mitano. Taarifa ya awali ya utafiti huo inaonesha kupungua kwa maambukizi ya ugonjwa wa malaria kwa watoto wa umri chini ya miaka

mitano kutoka asilimia 8.1 ya mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 5.5 mwaka 2025.

**Udhibiti wa Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele**

96. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika kutekeleza afua za kutokomeza Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele (NTDs) kama vile matende, mabusha, trakoma, usubi, kichocho, na minyoo ya tumbo. Jitihada hizo zinalenga kufikia lengo la kimataifa na kitaifa la kutokomeza magonjwa hayo ifikapo 2030 kupitia ugawaji wa kinga tiba huduma za upasuaji na uimarishaji wa mifumo ya kidijitali.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utoaji wa huduma za kingatiba na tiba dhidi ya magonjwa hayo, Wizara imetekeleza afua za moja kwa moja kwa wananchi kama ifuatavyo: Wananchi wapatao 3,331,925 (sawa na asilimia 69 ya walengwa) katika halmashauri 25 wamefikiwa na huduma ya kingatiba dhidi ya ugonjwa usubi. Aidha,

watoto wenye umri wa kwenda shule (miaka 5 – 14) 10,414,632 kati ya 11,916,055 sawa na asilimia 87.4 katika halmashauri 119 wamepatiwa kingatiba dhidi ya ugonjwa wa minyoo. Vilevile, watoto 6,176,203 kati ya 6,832,084 sawa na asilimia 90.4 ya walengwa katika halmashauri 147 wamepatiwa kingatiba dhidi ya kichocho. Huduma za upasuaji zimetolewa kwa wagonjwa 1,775 wa mabusha kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, na Mbeya. Wagonjwa 3,125 wa trakoma walifanyiwa upasuaji mdogo wa kusawazisha kope ili kuzuia upofu wa kudumu kwa wananchi hao kutoka Halmashauri za Nanyumbu, Nanyamba, Ngorongoro, Nachingwea, Ruangwa, Masasi DC, Masasi MC, Newala TC, Newala DC, Momba, Bagamoyo na Kibaha.

***98. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo ilifanya tathmini ya kiwango cha maambukizi kwa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele. Matokeo ya tathmini

hiyo yanaonesha kuwa halmashauri za Njombe TC, Njombe DC, Mufindi, na Morogoro DC maambukizi ya ugonjwa wa usubi yameshuka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2018 hadi asilimia 1.6 kwa mwaka 2026, isipokuwa halmashauri ya Morogoro DC ambapo kiwango cha maambukizi kimeongezeka kutoka asilimia 0.6 mwaka 2013 hadi asilimia 17.1 mwaka 2026. Kwa ugonjwa wa matende na mabusha, tathmini iliyofanyika katika halmashauri za Lindi MC, Mtwara Mikindani, na Mtama inaonesha kupungua kwa maambukizi mapya kutoka asilimia 7.5 mwaka 2023 hadi asilimia 0.2 Machi 2026.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo, tathmini katika halmashauri za Mbeya CC, Rungwe, Songwe, Ileje, na Sumbawanga inaonesha maambukizi ya minyoo yamepungua kutoka asilimia 50 kwa mwaka 2004 hadi kufikia asilimia 5 Machi 2026; kadhalika maambukizi ya kichocho yameshuka kwenye halmashauri tajwa kutoka asilimia 50.3 hadi asilimia 10 isipokuwa halmashauri

ya Sumbawanga DC ambapo maambukizi yamesalia kuwa asilimia 50. Kwa ugonjwa wa trakoma, tathmini iliyofanyika katika halmashauri za Kiteto, Simanjiro, Mpwapwa, na Kalambo ilionesha kupungua kwa maambukizi kutoka asilimia 14.6 kwa mwaka 2021 hadi kufikia asilimia 5.6 Machi 2026, isipokuwa katika halmashauri ya Kiteto ambapo kiwango cha maambukizi ni asilimia 9.9.

## Utoaji wa Huduma za Kinga

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma bora za kinga kwa kuhakikisha huduma za chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinapatikana muda wote kulingana na mahitaji. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri chini ya mwaka mmoja, umri chini ya miaka mitano, wajawazito, wasichana wenye umri wa miaka tisa (9), na makundi mengine yaliyo katika hatari ya magonjwa yanayozuilika kwa chanjo wanapata huduma hizo kwa wakati.

***101. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na uratibu wa ununuzi na usambazaji wa chanjo za watoto kwa magonjwa 13 yanayozuilika kwa chanjo. Chanjo hizo ni: Rota kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kuhara dozi 8,910,655; PCV - 13 kwa ajili ya kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Nimonia dozi 8,532,600; chanjo za Surua Rubella 8,295,000; bOPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio) dozi 19,204,560; Pentavalenti kwa ajili ya kukinga Donda Koo Kifaduro, Pepopunda, Homa ya Ini, na Mafua ya Influenza dozi 11,943,100; Td kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Pepo Punda dozi 5,600,000; BCG za kukinga watoto dhidi ya ugonjwa wa Kifua Kikuu dozi 12,700,000; HPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa Saratani ya mlango wa kizazi dozi 588,740 na IPV kwa ajili ya kukinga ugonjwa wa kupooza (Polio) dozi 6,838,400. Aidha, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kulikuwa na jumla ya dozi za chanjo 17,239,640 nchi nzima katika maghala ya kuhifadhia chanjo na zinatosheleza mahitaji ya nchi kwa muda wa miezi mitatu (3) mpaka sita (6).

**102. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilitoa chanjo ya Penta -3 ambayo hutumika kama kipimo kikuu cha utoaji wa chanjo nchini kwa watoto chini ya umri wa mwaka mmoja kwa watoto 2,361,701 sawa na asilimia 94.3 ya lengo la watoto 2,504,130. Aidha, katika kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka tisa (9) hadi 14 dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi, wasichana 866,299 wamepatiwa chanjo ya HPV sawa na asilimia 98 ya walengwa.

**103. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo, Wizara imenunua Boti saba (7) ambazo zimepelekwa katika maeneo ya Kigoma DC (1), Kibiti (1), Nkasi (1), Ukerewe (1), Muleba (1) na Zanzibar (2). Vilevile, Wizara imenunua Majokofu 237 ya kutunzia chanjo na vifaa 4,363 (RTM) na *Fridge Tags* 10,000 kwa ajili ya kufuatilia jotoridi la jokofu la chanjo kwa matumizi ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

**Huduma za Lishe**

***104. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha afua za lishe nchini, Wizara imeratibu utoaji wa matone ya vitamini A kwa watoto 9,115,501 walio chini ya umri wa miaka mitano sawa na asilimia 96.9 ya watoto 9,408,384 waliolengwa kupatiwa huduma hiyo. Aidha, Tanzania iliungana na mataifa mengine kuadhimisha wiki ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama duniani ambayo hufanyika kila mwaka kuanzia tarehe 1 hadi 7 Agosti na kaulimbiu ilikuwa "*Thamini unyonyeshaji, weka mazingira wezeshi kwa mama na mtoto*". Kupitia maadhimisho hayo, watoa huduma za afya 4,027 kutoka mikoa ya Mara, Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Dodoma, Katavi, Dar es Salaam, Manyara, Njombe, Rukwa, Songwe na Kigoma walijengewa uwezo wa kutoa huduma za lishe kwa makundi mbalimbali hususan kwa kina mama na watoto wachanga, watoto chini ya umri ya miaka mitano na vijana balehe.

***105. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa kanuni za uongezaji wa virutubishi kwenye chakula ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026 imenunua vifaa (I-check iron Machine) 12 vya kufuatilia kiwango vya madini chuma kwenye unga wa ngano na mahindi ambavyo vimesambazwa katika Mikoa ya Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Rukwa, Katavi, Kigoma, Geita, Tabora, Arusha na Tanga.

***106. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutoa elimu kuhusu ulaji unaofaa kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo; maadhimisho ya Siku ya Lishe Kitaifa yaliyofanyika tarehe 21 Novemba 2025 mkoani Ruvuma. Wizara ilitumia fursa hiyo kutoa elimu kwa wadau mbalimbali kwa kauli mbiu isemayo: "*Afya ni mtaji wako*, *Zingatia Unachokula*." Katika maadhimisho hayo shughuli mbalimbali zilifanyika katika halmashauri zote ikiwemo uelimishaji na uhamasishaji jamii kuhusu ulaji unaofaa. Jumla ya wananchi 5,650,002 walifikiwa, na

vipindi 970 vya elimu ya lishe vilitolewa kupitia redio, luninga na mitandao ya kijamii. Jumla ya mabango 3,624 ya hamasa ya lishe yaliwekwa shuleni na vyuoni ili kuongeza uelewa. Aidha, jumla ya miche 118,546 ya matunda ilipandwa kama hatua ya kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi.

## Taasisi ya Chakula na Lishe

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imekamilisha utafiti unaobainisha gharama za athari za utapiamlo hasa lishe pungufu hapa nchini. Utafiti huo ulianzishwa na Umoja wa Afrika kupitia mpango wa "The Cost of Hunger Study in Africa – COHA" na umeshafanyika pia katika nchi nyingi za Afrika. Utafiti huo umebainisha kuwa nchi yetu inapoteza hadi asilimia 2.03 ya pato ghafi la taifa (GDP) ambayo ni sawa na takribani Shilingi trilioni 3.47 (Dola za Marekani bilioni 1.5) kwa mwaka. Kiwango hiki kimetokana na uchambuzi wa athari za utapiamlo katika sekta ya afya, elimu na

uzalishaji mali. Kiwango hiki ni kikwazo kwa taifa kuweza kufikia lengo la Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 ya pato ghafi la Dola za Marekani trilioni 1. Mikakati madhubuti ya kukabiliana na lishe duni inahitaji kuendelea kutekelezwa ili kupunguza/kuondoa upotevu huu kwa kujenga raslimali watu ambayo itashiriki kikamilifu katika kazi za ujenzi wa taifa na kuleta tija.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa damu kwa vijana balehe, Taasisi imetengeneza asusa (snack bar) kwa kutumia maharage yaliyoongezwa virutubishi kibaiolojia (bio fortified beans). Bidhaa hii inatarajiwa kuzalishwa kwa wingi na kampuni ya BIVAC inayoongozwa na mjasiriamali Mtanzania kutoka Arusha kwa kushirikiana na taasisi, lengo likiwa ni kuzalisha tani 200,000 ili kuwafikia vijana balehe 2,000,000 kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano ijayo. Sambamba na hili, taasisi imetengeneza pia unga mchanganyiko kwa lengo la kukabiliana na tatizo la utapiamlo

wa kadiri. Unga huu umethibitishwa kisayansi kuwa na uwezo wa kupunguza utapimlo wa kadiri kwa asilimia 66 na upungufu wa damu kwa asilimia 59 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa maabara ya chakula, taasisi imefanya vipimo 18,000 kupitia maabara yake kwenye sampuli za damu, mkojo na vyakula zilizopokelewa kutoka katika nchi za Kenya, Ethiopia, Malawi, katika tafiti mbalimbali za lishe zinazoendelea nchini Tanzania kwa kushirikiana na taasisi zingine kama vile IITA, NI, Technoserve, GAIN na TARI. Maabara imeweza pia kufanya uchambuzi wa viashiria vya madini chuma, vitamin A, vitamin B12, madini joto na viashiria vya maambukizi ya magonjwa katika sampuli za utafiti wa Kitaifa wa Demorgraphic Health Survey (DHS). Idadi hii ya vipimo ni nyongeza ya asilimia 80 ya uchambuzi uliopangwa kufanyika katika kipindi hiki. Aidha, idadi hii ya watumiaji inapelekea nchi ambazo zinapata huduma katika Maabara ya

Taasisi kufikia 18 kutoka katika ukanda wa Afrika, Mashariki ya Kati, na Ulaya Mashariki. Katika kipindi hiki pia, maabara imeweza kuongeza idadi ya viashiria vinavyoweza kufanyiwa uchambuzi kutoka 9 hadi 12 pamoja na kununua mashine mpya ya kisasa yenye uwezo wa kupima vinasaba vinavyosababisha matatizo ya lishe.

***"Taifa letu haliwezi kuwa na askari imara au wakulima wenye nguvu kama wanawake hawajui thamani ya chakula wanachopika. Jiko la mwanamke ndilo kiwanda cha kwanza cha kutengeneza afya ya watanzania". Bibi Titi Mohamed***

**Afya Mazingira na Usafi**

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za usafi wa mazingira na usafi binafsi kwa kuhamasisha na kusimamia ujenzi na matumizi ya vyoo bora katika ngazi ya kaya, taasisi na maeneo ya umma kwa lengo la kudhibiti magonjwa ya mlipuko hususan kipindupindu na magonjwa ya kuhara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi

Machi 2026, jumla ya kaya zilizojenga vyoo bora zimeongezeka kutoka 8,504,503 hadi 9,165,833 sawa na ongezeko la kaya 661,330 na kufanya nchi kuwa na asilimia 78.4 ya kaya zenye vyoo bora. Vilevile, kaya zenye vifaa vya maji tiririka na sabuni vya kunawia mikono zimeongezeka kutoka asilimia 45.6 hadi 47.6 katika kipindi hicho. Mafanikio hayo yametokana na utekelezaji wa kampeni ya Taifa ya Mtu ni Afya kwa kuzingatia afua saba (7) ikiwemo ujenzi na matumizi ya vyoo bora na unawaji wa mikono, pamoja na kuimarisha uhamasishaji kupitia mbinu ya mabadiliko ya tabia na ushiriki wa vyombo vya habari.

**111. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhuisha miongozo inayolenga kuendelea kuimarisha usimamizi wa afua za usafi nchini ili kulinda jamii dhidi ya magonjwa ikiwemo Mwongozo wa Ujenzi wa Vyoo Bora ngazi ya Kaya yaani "The National Guideline for Household Sanitation Options & Catalogue on Sanitation Options" na Mwongozo wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

wakati wa majanga "National Guidelines on WASH During Emergency". Miongozo hii inalenga kutoa maelekezo kwa wataalam katika kusimamia na kuwezesha ujenzi wa aina mbalimbali za vyoo bora ngazi ya kaya kwa usahihi. Aidha, Mwongozo wa *WASH During Emergency* unatoa maelezo ya hatua sahihi za kufuata wakati wa majanga.

**112. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM TAMISEMI imeendelea kuratibu utekelezaji wa programu ya huduma endelevu za maji na usafi wa Mazingira kwa Sekta ya Afya inayotekelezwa katika Halmashauri 137 za Mikoa 25 ya Tanzania Bara. Programu hii inahusisha ujenzi wa miundombinu ya maji, udhibiti wa taka hatarishi, ujenzi wa vyoo bora, vifaa vya kunawia mikono na maboresho ya vyumba vya kujifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya, ambapo kwa awamu ya kwanza (2019 - 2025) jumla ya vituo 3,483 vimenufaika, ikiwa ni ongezeko la vituo 847 zaidi ya lengo la vituo 2,636.

**113. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutoa miongozo ya namna ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi ili kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa malengo ya kitaifa ya kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuimarisha utayari wa pamoja katika ngazi zote. Aidha, Wizara ilikamilisha uandaaji wa mchango wa taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa Sekta ya Afya inayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile, Wizara imefanya mapitio ya Mpango wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Sekta ya Afya wa mwaka 2018 - 2023, kwa lengo la kujumuisha masuala mapya ya kimkakati ya kukabiliana na athari za afya zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi. Mapitio hayo yamezingatia tathmini ya athari za kiafya zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi hususan kuongezeka kwa magonjwa ya milipuko. Tathmini hiyo imesaidia kuboresha nyenzo za kutathmini ubora wa huduma za afya ili kujumuisha viashiria vya ustahimilivu wa mabadiliko ya tabia nchi.

**114. *Mheshimiwa Spika,*** katika udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, Wizara ilitekeleza afua mbalimbali za udhibiti wa mazingira na taka. Wizara, ilikagua maeneo 145,566 yenye viashiria vya kelele na kubaini maeneo 41,456 kuwa na kelele na kati ya maeneo hayo, 4,632 yalibainika kuzidi kiwango kinachokubalika cha *decibel* 85 cha kelele. Vilevile, malalamiko 3,146 ya kelele yalipokelewa na kushughulikiwa, na hatua za kisheria zilichukuliwa ikiwemo tozo ya faini na mashitaka kwa malalamiko 568. Aidha, katika udhibiti wa taka zitokanazo na huduma za afya, jumla ya kilo 1,873,824 za taka ziliripotiwa kuzalishwa katika vituo vya kutolea huduma, ikiwemo taka hatarishi na zisizo hatarishi, hali inayoendelea kuhitaji uimarishaji wa mifumo ya usimamizi wa taka. Katika kutekeleza hili, jumla ya watumishi 120 wanaosimamia masuala ya afya mazingira kutoka katika Hospitali za Rufaa za Mikoa yote 26 na vituo 80 vya kutolea huduma ngazi ya msingi walipatiwa mafunzo ya usimamizi na uendeshaji shughuli za udhibiti taka zitokanazo na

huduma za afya na matumizi sahihi ya viteketezi taka.

***"Bila mazingira bora na afya imara, binadamu hawezi kuwa na tija" Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akizindua kampeni ya Kitaifa ya Elimu ya Afya kwa umma mwaka 1973.***

**Huduma za Afya na Usalama Kazini**

***115. Mheshimiwa Spika,*** Huduma za Afya na Usalama Kazini zina lengo la kuwajengea watumishi uwezo wa kutambua na kujikinga dhidi ya hatari za kiafya na kiusalama katika mazingira ya kazi, jambo linalochangia kuimarisha ufanisi wao na kuboresha utoaji wa huduma kwa jamii. Kupitia huduma hizo, watumishi huwezeshwa kufanya kazi katika mazingira salama, bora na yenye afya.

***116. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imekamilisha mwongozo wa kitaifa wa kulinda afya, usalama na utu wa wafanyakazi wa usafi wa mazingira na

kuandaa nyenzo za mafunzo. Hatua inayoendelea sasa ni kusambaza na kutoa mafunzo ya mwongozo katika mamlaka mbalimbali nchini.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza mpango wa kimataifa wa "Beat the Heat", unaolenga kulinda afya ya jamii dhidi ya madhara ya joto kali yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kutekeleza mpango huo kwa ngazi ya kitaifa kati ya nchi tatu wenyeji katika mashindano ya AFCON 2027. Moja ya utekelezaji wa afua ya mpango huo ni pamoja na tathmini ya awali ya hatari na utayari wa kukabiliana na joto kali, ikiwemo tathmini ya miundombinu ya michezo iliyofanyika katika uwanja wa Benjamin Mkapa wakati wa mashindano ya CHAN mwezi Agosti 2025. Maeneo yenye hatari yalibainishwa na mapendekezo yaliwasilishwa katika kamati ya maandalizi ya AFCON 2027 kwa hatua za maboresho.

## Elimu ya Afya Kwa Umma na Huduma za Afya Ngazi ya Jamii

***118. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeendelea kutoa elimu ya afya kwa umma na hamasa kwa jamii kuhusu njia mbalimbali za kujikinga na magonjwa yanayoambukiza, na yale yasiyoambukiza hususan katika lishe bora, ulaji unaofaa, afya ya uzazi, mama na mtoto na wazee. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara ilitayarisha na kusambaza vielelezo mbalimbali vya elimu ya afya ambapo jumla ya video 518, vipeperushi vya mtandaoni 987, matangazo ya redio 53, matangazo ya televisheni 26, vipindi vya redio 512, na vipindi vya televisheni 172 vimerushwa kuwafikia wananchi. Vilevile, elimu ya afya kuhusu kinga dhidi ya magonjwa ya mlipuko ilitolewa kwa kufanya uhamasishaji kupitia magari ya matangazo na vipaza sauti katika maeneo yenye mikusanyiko ambapo jumla ya kata 108, na maeneo ya mikusanyiko 3,900 yalifikiwa. Juhudi hizo kupitia magari

ya matangazo na huduma ya nyumba kwa nyumba inayofanywa na wahudumu wa afya ngazi ya jamii zimewezesha kuwafikia wananchi 7,570,000.

**119.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha huduma ya utoaji elimu ya msingi katika tiba, kinga, lishe na ustawi wa jamii ngazi ya jamii inaimarika, Wizara imeendelea kutekeleza Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa Afya Ngazi ya Jamii ambapo kupitia mpango huo jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii 1,832 walipata mafunzo ya miezi 6 na kuwezeshwa vitendea kazi ikiwemo vishikwambi kutoka katika mikoa 12 ambayo ni Pwani, Mbeya, Kagera, Njombe, Songwe, Lindi, Geita, Kigoma, Tabora, Dodoma, Tanga na Ruvuma. Hadi sasa jumla ya wahudumu wa afya ngazi ya jamii waliohitimu mafunzo hayo na kurejea kwenye jamii waliyotoka na kuanza kutekeleza majukumu yao ni 9,870 kutoka halmashauri 25.

***120. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha matumizi ya teknolojia za kidijitali ili kuboresha huduma za afya, Wizara imeendelea kuboresha kituo cha mawasiliano ya afya kwa umma (Afya Call Center) kwa kuanzisha jukwaa la "Ongea na Waziri". Kituo hicho kinatoa huduma za elimu, ushauri na mwongozo wa afya kwa njia ya simu namba 199 bila malipo kama hatua ya kimkakati inayotafsiri dhamira ya Serikali kwa vitendo na kuifanya Sekta ya Afya kuwa karibu na wananchi kwa kupokea maoni, pongezi, kusikiliza kero, malalamiko na kutatua kwa wakati. Katika kipindi hiki, jumla ya wananchi 4,269,045 walipiga simu na kuhudumiwa. Miongoni mwa masuala yaliyoulizwa kwa wingi ni Bima ya Afya asilimia 31, magonjwa ya mlipuko asilimia 21, magonjwa yasiyoambukiza asilimia 11, magonjwa ya kuambukiza asilimia 11 na afya ya akili asilimia 10. Kituo hiki kimeiwezesha Wizara kupata tuzo ya umahiri katika utoaji wa huduma za afya kidijitali iliyotolewa mwezi Agosti, 2025 katika kongamano la East Africa Youth Business

and Investment Expo Zanzibar. Vilevile, Wizara imetumia fursa ya majukwaa mbalimbali ya kidijitali ambapo jukwaa la "Tukutane TikTok Live", limeanzishwa na kuwafikia wananchi zaidi ya 100,000 kupitia vipindi 39 vilivyoandaliwa.

***121. Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, Serikali kupitia Wizara ya Afya imezindua kampeni maalum na endelevu ijulikanayo kama **"Zijue Namba Zako."** Kampeni hiyo niliyoizindua mwezi Mei 2026 mkoani Mwanza, ina lengo la kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii na kuwapa fursa ya kufanya uchunguzi wa afya ili kubaini hali ya magonjwa ya shinikizo la juu la damu, kisukari, ongezeko la mafuta mwilini na uzito uliokithiri. Aidha, kampeni hiyo itawawezesha wananchi kuchukua hatua stahiki mapema ikiwa ni pamoja na kupata matibabu kwa wale watakaobainika kuwa na magonjwa yasiyoakuambukiza au kuchukua hatua za kinga kwa wale ambao hawatakuwa na magonjwa hayo kwa

kuzingatia ulaji unaofaa, kufanya mazoezi, kujiepusha na tabiabwete, kuepuka matumizi ya vilevi kama vile pombe na tumbaku.

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa elimu na hamasa katika masuala mbalimbali ya afya na lishe katika shule za msingi 4,800 na kuwafikia wanafunzi 279,000. Aidha, moduli za kufundishia walimu kuhusu afya na lishe zimeandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Taasisi ya Elimu Tanzania, na kuwekwa katika mfumo wa kidijitali ili kuwezesha matumizi kwa walimu. Hii itasaidia kuimarisha uelewa kwa walimu kuhusu afya na lishe na kutoa elimu kwa wanafunzi kwa usahihi hivyo kusaidia kudumisha na kuboresha afya ya mtu mmoja mmoja, familia na jamii kwa ujumla.

## Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 23 ya mwaka 1979 ikiwa na jukumu la kuratibu, kudhibiti na kusimamia utekelezaji wa tafiti mbalimbali za afya hapa nchini, Taasisi imekuwa ikipokea maombi kutoka kwa watafiti mbalimbali kutoka katika Taasisi za tafiti ndani na nje ya nchi, wanataaluma kutoka katika vyuo vikuu na watu wengine wenye nia ya kufanya utafiti katika eneo la afya. Taasisi kupitia *Medical Research Coordination Committee* imekuwa ikipitia maombi yote yanayowasilishwa, baada ya kuyapitia na kujiridhisha, yale yanayokidhi vigezo hupatiwa kibali kwa ajili ya kuanza kufanya tafiti husika. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 Taasisi ilitoa vibali 513 kati ya maombi 600 yaliyowasilishwa sawa na asilimia 86.

***124. Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa utafiti, Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazolenga magonjwa ya kuambukiza yanayojitokeza (emerging and reemerging diseases) na magonjwa yasiyoambukiza, uimarishaji wa mifumo ya afya, kuelewa viashiria vya kijamii na mazingira vya afya, tiba asili na tafiti mtambuka za mabadiliko ya tabianchi. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imetekeleza miradi ya tafiti 119 kati ya 150 iliyopangwa kwa mwaka 2025/2026 ambayo ni sawa na asilimia 79.3.

**Huduma za Dharura na Majanga**

***125. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko kupitia matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa *Electronic Infectious Disease Surveillance and Response* (eIDSR), ambao unawezesha ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa kwa wakati ili kuchukua hatua za haraka za

kudhibiti kusambaa kwa magonjwa. Tangu tarehe 25 Februari, 2026 Wizara imefanikiwa kudhibiti ugonjwa wa kipindupindu na jitihada za kuzuia mlipuko mwingine zinaendelea. Aidha, katika kipindi hicho visa 153 vya Surua katika mikoa 14 na visa 253 vya Mpox katika mikoa 18 viliripotiwa bila vifo.

**126.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imekamilisha kituo maalum cha kisasa cha kitaifa kilichopo katika jengo la Wizara ya Afya (Public Health Emergency Operations Center-PHEOC), ambacho kinaratibu taarifa mbalimbali za matukio ya dharura za afya na tetesi za magonjwa zinazoibuliwa katika jamii, vituo vinavyofuatilia afya mipakani na vituo vya kutoa huduma za afya nchini. Kituo hiki kimeboresha uratibu wa vituo vingine kama hivi vilivyoko ndani ya mikoa 20 nchini vinavyosaidia kuchakata taarifa hizo na kuchukua hatua na kutekeleza afua za kujilinda dhidi ya magonjwa ya mlipuko au majanga pamoja na kujiandaa, kukabiliana na kudhibiti milipuko

hiyo endapo itatokea. Wizara inaendelea kuboresha uendeshaji wa vituo hivyo kwa kuwajengea uwezo wasimamizi wote kwa kupitia dhana ya afya moja kwa kushirikiana na sekta zingine.

***127. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imejenga uwezo wa rasilimali watu kwa kutoa mafunzo kwa watumishi 548 katika Halmashauri 11 za mikoa ya Katavi na Ruvuma iliyo katika hatari zaidi ya kupata magonjwa ya mlipuko. Mafunzo hayo yalilenga kuimarisha utambuzi, utoaji wa taarifa na udhibiti wa magonjwa hayo. Vilevile, wahudumu wa afya ngazi ya jamii 5,070 katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Mwanza, Geita na Ruvuma walipatiwa mafunzo ya kutambua na kuripoti tetesi za magonjwa kwa kutumia simu za mkononi.

***128. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya usimamizi shirikishi kuhusu ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za tetesi za magonjwa na matukio yenye athari za kiafya ya jamii kwa kutumia mfumo wa kidigitali wa kutoa

taarifa za matukio ili waweze kutoa taarifa za tetesi za magonjwa kwa wakati. Aidha, Wizara imefanya mafunzo kwa timu za utayari kwa wataalam 195 kutoka katika mikoa saba (7) ya kimkakati ambayo ni Kigoma, Katavi, Songwe, Dodoma, Kagera, Dar es salaam na Mwanza. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo wa namna ya kushiriki kikamilifu katika kushughulikia dharura na kuibua matukio katika jamii kwa kushirikiana na watoa huduma ngazi ya jamii pamoja na wananchi.

**129.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara iliendelea kutekeleza afua za udhibiti wa magonjwa ya mlipuko ikiwemo Mpox, Ebola na Homa ya Manjano katika viwanja vya ndege, bandari na mipaka ya nchi kavu kwa kufanya uchunguzi wa awali wa afya kwa wasafiri wanaoingia na kutoka nchini. Jumla ya wasafiri 10,829,772 walifanyiwa uchunguzi, wakiwemo wasafiri wa kimataifa 2,840,876 na wasafiri wa ndani 7,988,896. Kati yao, wasafiri 233 walihisiwa kuwa na dalili za magonjwa ya mlipuko na kupelekwa katika

vituo vya kutolea huduma za afya kwa uchunguzi zaidi.

**130.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za chanjo ya homa ya manjano kwa wasafiri wa kimataifa, ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya wasafiri 17,734 walipatiwa chanjo hiyo. Ili kuboresha utoaji wa huduma hizo, magari manne (4), pikipiki 10, majokofu 20 na vibebea chanjo 20 vilinunuliwa na kusambazwa katika ofisi za Afya Mipakani. Aidha, ofisi mpya tatu (3) za afya mipakani zilianzishwa katika bandari ya Wampembe na viwanja vya ndege vya Iringa na Tabora na watumishi wapya 56 waliajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi.

**131.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imefanya tathmini ya vihatarishi vya matukio ya dharura na kuandaa kalenda maalum ya dharura za afya na milipuko inayoweza kutokea kwa kipindi cha mwaka 2025 - 2027 kwa ngazi ya taifa na katika baadhi ya mikoa ya Kagera, Dodoma na Tanga iliyopewa kipaumbele. Kalenda hiyo

inatumika kupanga mipango na kujiandaa kuzuia na kukabiliana na dharura za afya. Utambuzi wa vihatarishi vya matukio ya dharura katika mkoa husika utawezesha kujiandaa na kukabiliana na hatari ya matukio husika yasitokee na endapo yakitokea yasilete madhara makubwa katika jamii.

**132.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imefanya tathmini ya utayari wa mikoa 11 ya Kigoma, Mwanza, Dar es salaam, Tanga, Ruvuma, Songwe, Katavi, Arusha, Kilimanjaro, Tabora na Rukwa iliyo katika hatari kubwa ya kupata mlipuko wa Ebola na Marburg. Lengo ni kuangalia utayari wa timu za maafa na dharura pamoja na vituo vya dharura na maafa kwa ngazi za mikoa na kuwajengea uwezo wa namna ya kujiandaa kukabiliana na Ebola na Marburg. Aidha, katika kukabiliana na shambulio la ugonjwa wa Ebola na Marburg ulioripotiwa nchini Kongo mwezi Agosti 2025, Wizara iliandaa mpango kazi na mwongozo wa kukabiliana

na Ebola na Marburg na kufanikiwa kuzuia ugonjwa huo kuingia nchini.

**133. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya mafunzo kwa vitendo na usimamizi shirikishi katika utoaji wa huduma za tiba za dharura na wagonjwa mahututi kwa mikoa 12 ya Pwani, Dar es salaam, Mwanza, Morogoro, Manyara, Arusha, Ruvuma, Mtwara, Dodoma, Simiyu Mbeya na Mara katika idara za dharura zaidi ya 125 zilizojengwa katika ngazi ya msingi (86) na ngazi ya rufaa (39). Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo watoa huduma kuhusu namna bora ya kuhudumia wagonjwa wa dharura pindi wafikapo katika vituo vya kutolea huduma.

**134. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara imejenga vituo maalum na kuweka vifaa vya kisasa vya mafunzo ya huduma za dharura kwa vitendo vyenye thamani ya Shilingi 3,059,979,959 katika hospitali za kanda za Bugando na Mbeya, na kufanya idadi kuongezeka kutoka vituo vinne (4) hadi

vituo sita (6) katika hospitali za Kanda nchini ambazo zinasaidia sana kuongeza ujuzi wa watoa huduma na kuwawezesha kutoa huduma bora katika maeneo ya wodi za wagonjwa mahututi, idara za dharura, wodi za uangalizi maalum na wodi za uangalizi maalum kwa watoto. Vituo vingine vimejengwa katika hospitali ya Benjamin Mkapa, hospitali ya taifa Muhimbili Upanga na Mloganzila na hospitali ya kanda ya kaskazini KCMC. Vituo hivyo pia vinatumika kutoa mafunzo ya huduma ya kwanza kwa makundi maalum ikiwemo jeshi la polisi, jeshi la zimamoto na uokoaji na madereva ili kusaidia katika kutoa huduma kwa majeruhi wakati wa ajali. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya watu 7,396 wamepata mafunzo ya huduma ya tiba ya dharura na huduma ya kwanza katika mikoa mbalimbali nchini.

**135.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kuendelea kuimarisha huduma za magari ya kubebea wagonjwa nchini, Wizara imefanya tathmini katika Mikoa 11 ya Tanga, Pwani, Dar es salaam, Morogoro, Dodoma, Lindi, Mtwara,

Arusha, Kilimanjaro, Kigoma na Manyara kwa lengo la kuangalia ubora wa magari hayo ili yenye mapungufu kuandaliwa mpango wa maboresho. Jumla ya magari 80 kati ya 473 sawa na asilimia 17 ya magari yaliyofanyiwa tathmini hayakuwa katika hali nzuri ya kutoa huduma ambapo mkoa wa Lindi uliongoza kwa kuwa na asilimia 33 ya magari ya kubebea wagonjwa yasiyo na hali ya kuridhisha. Hivyo, Serikali inaendelea kuelekeza vituo vya kutolea huduma kote nchini kuimarisha utunzaji wa magari hayo na kuyafanyia matengenezo kinga, kutoa mafunzo kwa madereva na watoa huduma wakati wa usafiri wa dharura.

***"Mheshimiwa Spika, nasisitiza kwamba uwekezaji katika kinga na utayari dhidi ya dharura na majanga ni nafuu kuliko gharama itakayotumika wakati wa kupambana na dharura au majanga yanapotokea. Hivyo, Serikali itaendelea kuwekeza katika kujikinga na kuimarisha utayari katika kudhibiti magonjwa ya mlipuko yanayovuka mipaka".***

## Utoaji wa Huduma za Tiba

### Miundombinu na Huduma kwa Wagonjwa

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma bora za afya nchini, Wizara imeendelea kuratibu ujenzi wa miundombinu ya utoaji wa huduma mbalimbali za tiba. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 12,846 hadi 13,683 sawa na ongezeko la vituo 837. Aidha, vituo vinavyomilikiwa na Sekta binafsi ni 4,368 sawa na asilimia 32, mashirika ya dini 1,092 sawa na asilimia 8 na Serikali ni 8,223 sawa na asilimia 60. Kati ya Vituo vinavyomilikiwa na Serikali hospitali ni 248, vituo vya afya 1,042, zahanati 6,722, na vituo vingine 211. Ongezeko la vituo vya kutolea huduma za afya nchini limewezesha kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi ambapo wastani wa asilimia 85 wanapata huduma za afya ndani ya kilometa tano (5) na hivyo kupunguza changamoto ya

kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya.

## Utoaji wa Huduma za Tiba kwa Wagonjwa

***137. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya kutolea huduma za afya kwa wananchi katika vituo vya kutolea huduma za afya ambapo vitanda vimeongezeka kutoka 153,683 hadi kufikia vitanda 156,932. Hivyo kufanya uwiano wa vitanda 2.3 kwa kila watu 1,000 ukilinganisha na Mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaoelekeza kuwa na uwiano wa vitanda 2.5 kwa kila watu 1,000. Aidha, kati ya vitanda 156,932 vitanda 65,938 vipo katika ngazi ya Hospitali, 41,491 vipo katika Vituo vya Afya, 46,282 vipo katika Zahanati na vitanda 3,221 vinapatikana ngazi ya kliniki, kama inavyoonekana katika jedwali Na. 2 hapa chini.

***Jedwali Na.2 Mchanganuo wa Idadi ya Vitanda.***

| Vituo | Vinavyohitajika | Vilivyopo wodini | Vitanda vya kujifungulia | Vitanda vya uchunguzi | Jumla ya Vitanda |
|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali | 74,654 | 58,589 | 2,019 | 5,330 | 65,938 |
| Vituo vya Afya | 42,136 | 32,261 | 3,766 | 5,456 | 41,491 |
| Zahanati | 43,531 | 23,506 | 8,986 | 13,790 | 46,282 |
| Kliniki | 3,329 | 1,534 | 189 | 1,498 | 3,221 |
| Jumla | 163,650 | 115,890 | 14,960 | 26,074 | 156,932 |

***138. Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi, ambapo jumla ya wagonjwa 36,996,862 walihudumiwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Kati yao, wagonjwa wa nje walikuwa 35,260,883 na wagonjwa wa kulazwa walikuwa 1,735,979. Aidha, wagonjwa 6,736,126 sawa na asilimia 18 walipata huduma katika hospitali za rufaa ngazi ya mkoa, kanda, maalum na taifa na wagonjwa 30,260,736 sawa na asilimia 82 walipata huduma katika ngazi ya msingi.

***Jedwali Na.3: Idadi ya Wagonjwa waliohudhuria katika matibabu ya Wagonjwa wa nje (OPD) na Wagonjwa wa kulazwa (IPD) katika Vituo vya kutolea huduma kwa kipindi Julai 2025 hadi Machi 2026***.

| AINA YA KITUO | Jumla OPD | % | Jumla IPD | % | Jumla Kuu | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Hospitali ngazi ya Taifa, Hospitali Maalum, Kanda | 1,989,698 | 5.6% | 194,986 | 11.2% | 2,184,684 | 5.9% |
| Hospitali ngazi ya za Rufaa za Mikoa | 4,059,150 | 11.5 | 492,292 | 28.4% | 4,551,442 | 12.3% |
| Hospitali ngazi ya Halmashauri | 5,585,976 | 15.8% | 551,869 | 31.8% | 6,137,845 | 16.6% |
| Vituo vya Afya | 7,573,559 | 21.5% | 474,674 | 27.3 | 8,048,233 | 21.8% |
| Zahanati | 14,577,396 | 41.3% | 15,158 | 0.9% | 14,592,554 | 39.4% |
| Kliniki | 1,418,370 | 4.0% | 1,251 | 0.1% | 1,419,621 | 3.8% |
| Maternity and Nursing Home | 34,770 | 0.1% | - | 0.0% | 34,770 | 0.1% |
| Nyinginezo | 21,964 | 0.1% | 5,749 | 0.3% | 27,713 | 0.1% |
| **JUMLA** | **35,260,883** | | **1,735,979** | | **36,996,862** | |

## Magonjwa Yaliyoongoza Kuwaathiri Wananchi – Wagonjwa wa Nje

***139. Mheshimiwa Spika,*** Magonjwa yaliyoongoza katika kuwaathiri zaidi wananchi na kuwasababishia kwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu kwa wagonjwa wa nje chini ya miaka mitano (5) ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 36.8, kuharisha asilimia 8.2, malaria ni asilimia 7.2 na maambukizi katika njia ya

mkojo ni asilimia 6.2. Katika kipindi hicho magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje kwa wagonjwa wenye umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 16.2, maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 15.4 na shinikizo la juu la damu asilimia 7.1.

**140. *Mheshimiwa Spika*,** takwimu zinaonesha kuwa magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la juu la damu, kisukari, magonjwa ya viungo (arthritis) na upungufu wa damu yanaongezeka kwa kasi hadi kufikia kuwemo katika orodha ya magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha watu kuhudhuria katika vituo vya kutolea huduma za afya. Magonjwa hayo yanaweza kuzuilika kwa wananchi kubadili mitindo ya maisha isiyofaa kama kula kusikozingatia ulaji bora, unywaji wa pombe uliopitiliza, uvutaji wa sigara, tabia bwete na kutopumzika vya kutosha.

***Jedwali Na. 4: Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje; katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026***

| | **WAGONJWA WA NJE - CHINI YA MIAKA MITANO** | | | **WAGONJWA WA NJE - ZAIDI YA MIAKA MITANO** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **AINA YA UGONJWA** | **IDADI** | **%** | **AINA YA UGONJWA** | **IDADI** | **%** |
| 1 | Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 4,465,725 | 36.8 | Maambukizi katika mfumo wa hewa | 3,465,266 | 16.2 |
| 2 | Kuharisha pasipo kupungukiwa maji | 993,626 | 8.2 | Maambukizi katika njia ya mkojo | 3,296,017 | 15.4 |
| 3 | Malaria (BS +Ve, mRDT +Ve & Clinical) | 870,330 | 7.2 | Shinikizo la Juu la damu | 1,519,187 | 7.1 |
| 4 | Maambukizi katika Njia ya Mkojo | 756,955 | 6.2 | Malaria (BS+Ve, mRDT+Ve & Clinical) | 1,032,952 | 4.8 |
| 5 | Homa ya mapafu | 726,628 | 6.0 | Vidonda vya tumbo | 942,630 | 4.4 |
| 6 | Maambukizi kwenye damu | 497,217 | 4.1 | Kisukari | 704,316 | 3.3 |
| 7 | Kuoza kwa meno | 459,020 | 3.8 | Magonjwa ya mfumo wa chakula | 615,652 | 2.9 |
| 8 | Magonjwa yasiyo ya mfumo wa chakula | 361,677 | 3.0 | Homa ya mapafu | 502,408 | 2.3 |
| 9 | Kuharisha | 296,282 | 2.4 | Maambukizi kwenye damu | 457,639 | 2.1 |
| 10 | Maambukizi ya Ngozi - fungal | 249,336 | 2.1 | kuchanika kwa misuli/ mishipa | 447,329 | 2.1 |

***Chanzo: DHIS2***

## Magonjwa Yaliyoongoza Kuwaathiri Wananchi – Wagonjwa wa Kulazwa

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa ndani kwa wagonjwa wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa

hewa asilimia 55.5, maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 9.4 na maambukizi ya ngozi asilimia 3.1. Aidha, magonjwa yaliyoongoza kwa umri wa miaka mitano na zaidi yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa asilimia 19.7, maambukizi katika njia ya mkojo asilimia 18.7 na shinikizo la juu la damu asilimia 8.6.

***Jedwali Na. 5: Magonjwa 10 yaliyoongoza kwa wagonjwa wa ndani; katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026***

| | **WAGONJWA WA NDANI - CHINI YA MIAKA MITANO** | | | **WAGONJWA WA NDANI - ZAIDI YA MIAKA MITANO** | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **NA** | **AINA YA UGONJWA** | **IDADI** | **%** | **AINA YA UGONJWA** | **IDADI** | **%** |
| 1 | Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 4,465,725 | 55.5 | Maambukizi katika Mfumo wa Hewa | 3,465,266 | 19.7 |
| 2 | Maambukizi katika Njia ya Mkojo | 756,955 | 9.4 | Maambukizi katika Njia ya Mkojo | 3,296,017 | 18.7 |
| 3 | Maambukizi ya ngozi yasiyotokana na fangasi | 451,947 | 5.6 | Shinikizo la Juu la damu | 1,519,187 | 8.6 |
| 4 | Maambukizi ya ngozi ya fangasi | 249,336 | 3.1 | Vidonda vya tumbo | 942,630 | 5.4 |
| 5 | Minyoo ya tumbo | 183,623 | 2.3 | Kisukari | 704,316 | 4.0 |
| 6 | Magonjwa mengine ya mfumo wa upumuaji | 180,027 | 2.2 | kuchanika kwa misuli/ mishipa | 447,329 | 2.5 |
| 7 | Upungufu wa damu wa kiwango kidogo | 173,319 | 2.2 | Upungufu wa damu wa kiwango kidogo | 389,981 | 2.2 |
| 8 | Magonjwa ya ngozi yasiyo ya maambukizi | 130,860 | 1.6 | Maumivu ya viungo | 357,822 | 2.0 |
| 9 | Maambukizi ya sikio | 116,785 | 1.5 | Maambukizi ya ngozi ya fangasi | 337,606 | 1.9 |
| 10 | Maambukizi ya mirija ya hewa | 114,523 | 1.4 | Maambukizi ya ngozi yasiyotokana na fangasi | 303,791 | 1.7 |

***Chanzo: DHIS2***

## Huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala

142. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini, Wizara ilikutana na wadau wote nchini kwa lengo la kuweka mikakati ya pamoja na kutatua changamoto zinazokabili utoaji wa huduma hizo. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu huduma za tiba asili na tiba mbadala ikiwa ni pamoja na huduma jumuishi za tiba asili zinazoendelea kutolewa katika hospitali za rufaa za mikoa 14 (Mbeya, Bombo, Sekou Toure, Singida, Simiyu,Temeke, Mwananyamala, Morogoro, Dodoma, Mt. Meru, Kitete, Bukoba, Sumbawanga na Njombe). Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya dawa 48 zimesajiliwa ambapo dawa sita (6) zimepelekwa kwenye utafiti wa usalama wa awali na kati ya hizo dawa mbili (2) za kisukari zinafanyiwa utafiti wa ufanisi ili ziweze kujumuishwa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Vilevile, jumla ya wagonjwa 648 wamehudumiwa kwa dawa za tiba asili katika hospitali zote zinazotoa huduma

jumuishi. Magonjwa yaliyotibiwa zaidi ni vidonda vya tumbo, pumu, mfumo wa upumuaji, homa ya matumbo, mvurugiko wa homoni kwa wanawake, maambukizi ya mfumo wa mkojo, bawasili, baridi yabisi (athritis), tezi dume na upungufu wa nguvu za kiume. Katika kuboresha upatikanaji wa huduma jumuishi za tiba asili nchini, Wizara ilifanya usimamizi shirikishi katika hospitali sita (6) za rufaa za mikoa (Singida, Morogoro, Tanga, Arusha, Mwananyamala na Temeke) na kiwanda cha NIMR – Mabibo.

***"Tunapothibitisha tiba asili kwa sayansi, tunageuza urithi wa mababu zetu kuwa tiba salama ya leo, fursa ya uchumi wa kesho, na nguzo ya kujitegemea kwa Taifa".***

**Huduma za Matibabu ya Ubingwa na Ubingwa Bobezi**

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini kwa lengo la kusogeza huduma hizo kwa

wananchi na kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia tiba utalii. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla wa wagonjwa 4,202,137 walipatiwa huduma katika hospitali ngazi za rufaa. Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa wa nje walikuwa 3,709,432 na wa kulazwa walikuwa 492,705. Aidha, baadhi ya huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na kupandikiza mimba kwa wateja kumi (10), upandikizaji wa figo kwa wagonjwa 24, upandikizaji wa vifaa vya usikivu wagonjwa 16, huduma ya kuweka puto tumboni kwa ajili ya kupunguza uzito kwa wagonjwa tisa (9), upandikizaji wa meno kwa wagonjwa 26, kubadilisha goti au nyonga kwa wagonjwa 58 na upandikizaji uloto kwa wagonjwa nane (8). Kutolewa kwa huduma hizo za kibobezi nchini kumepelekea kuokoa takribani Shilingi bilioni 3.67 endapo wagonjwa hawa wangehudumiwa nje ya nchi.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali za

rufaa za mikoa zimeendelea kuimarisha huduma za ubingwa kwa kuanzisha huduma mpya za ubingwa katika fani za magonjwa ya macho, mfumo wa mkojo, afya ya akili, masikio, pua na koo, kuchuja damu, magonjwa ya ngozi, saratani, magonjwa ya mfumo wa chakula, upasuaji wa mifupa, radiolojia, huduma za dawa za usingizi na ganzi, patholojia na magonjwa ya dharura ambapo wagonjwa 17,409 walihudumiwa. Hospitali za rufaa za mikoa zilizoanzisha huduma mpya ni Geita, Katavi, Ligula, Maweni, Mawenzi, Mount Meru, Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere, Sekou Toure, Shinyanga, Songea, Songwe na Tumbi.

***145. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Madaktari Bingwa wa Dkt. Samia imetoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa wagonjwa 55,300 katika halmashauri zote 184 nchini. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizotolewa ni pamoja na magonjwa ya ndani, magonjwa ya wanawake na uzazi, huduma za watoto, huduma za upasuaji

bingwa wa mifupa na majeruhi, huduma za kinywa na meno na huduma za upasuaji wa magonjwa mbalimbali. Baadhi ya wananchi wenye magonjwa ya muda mrefu waliweza kupata huduma za upasuaji karibu na makazi yao na hivyo kuwapunguzia adha na gharama, mfano mgonjwa aliyeondolewa uvimbe wa kilo 20 tumboni. Aidha, jumla ya wataalam 5,585 waliopo katika vituo vya kutolea huduma za afya wamejengewa uwezo wakati wa utoaji wa huduma kutoka kwa madaktari hao.

***146. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum na taifa ilitoa huduma mkoba nchini zilizoweza kuwafikia jumla ya wagonjwa 77,118 na kati yao 6,807 walifanyiwa upasuaji. Aidha, kupitia tiba utalii jumla ya wagonjwa 3,018 raia wa kigeni walipatiwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi. Madaktari bingwa na bobezi kutoka hospitali za JKCI na Benjamin Mkapa walikwenda nje ya nchi na kutoa huduma kwa wagonjwa 4,363 katika nchi za Zambia, Comoro na

Burundi kwa lengo la kuendelea kutangaza huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zinazopatikana nchini, kuvutia tiba utalii na kukuza diplomasia ya afya.

***"Huduma za kibingwa zinaposogezwa karibu na wananchi, Taifa haliponyi wagonjwa pekee; linapunguza hofu, linarejesha matumaini, linajenga uwezo wa wataalam, na linatangaza ubora wa Tanzania ndani na nje ya mipaka yake."***

**Hospitali ya Taifa Muhimbili – Upanga**

***147. Mheshimiwa Spika,*** hospitali ya Taifa ya Muhimbili - Upanga imetoa huduma kwa wagonjwa 373,176 kati ya wagonjwa hao wakulazwa ni 28,881 na wagonjwa wa nje ni 344,295. Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi kwa kutoa huduma za kupandikiza mimba ambapo hadi Machi, 2026 jumla ya wateja kumi (10) walipata huduma hiyo. Aidha, huduma nyingine zilizoendelea kutolewa ni pamoja

na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa saba (7) hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 88 tangu huduma ilipoanzishwa mwaka 2017; upandikizaji wa vifaa vya usikivu wagonjwa 16, hivyo kufanya jumla ya wagonjwa kufikia 86 tangu huduma hiyo ilipo anzishwa mwaka 2017. Vilevile, katika kukuza tiba utalii nchini, jumla ya wagonjwa 833 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Mauritius na Zambia walipatiwa huduma.

***148. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali ya Taifa Muhimbili imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 6,802,647,947 kwa wagonjwa 36,414 ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 10,640,269,858 kwa wagonjwa 42,714 kwa kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na kuchuja damu, huduma za ICU, huduma za vipimo vya CT scan, MRI na huduma za dawa.

**149. *Mheshimiwa Spika***, katika kuendelea kuboresha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini, Serikali ilifanya tathmini ya utoaji wa huduma katika hospitali ya Taifa Muhimbili na kubaini mapungufu mbalimbali. Mapungufu hayo ni pamoja na uchakavu wa miundombinu na kutawanyika kwa mpangilio wa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na ukarabati wa mara kwa mara na mazingira yasiyoruhuru maboresho ya huduma za ubobezi na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Dhamira ya Serikali ni kufanya mapinduzi na kujenga Muhimbili mpya itakayotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi ili kufikia viwango vya kimataifa na kuiwezesha kutoa huduma kwa wananchi na wageni kutoka nje ya nchi na hivyo kuimarisha tiba utalii.

**150. *Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa Muhimbili mpya utapunguza idadi ya rufaa za matibabu nje ya nchi, itaongeza maeneo ya kutolea huduma, itapunguza kero ya kusubiri huduma kwa muda mrefu, itaboresha

mazingira ya kazi kwa watumishi, itaingiza fedha za kigeni na kuimarisha uchumi wa nchi. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miaka mitano (5) na kugharimu Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa majengo, mifumo, ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali. Naomba nifafanue kwa kifupi kuwa mchango wa Serikali katika mradi huo kwa sehemu kubwa si fedha taslimu bali ni gharama za maandalizi ya eneo la ujenzi, msamaha wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa bidhaa na vifaa vitakavyoingizwa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya ulinganifu wa gharama za ujenzi wa hospitali mpya ya Muhimbili kwa kulinganisha na miradi mingine 16 kutoka nchi 15 tofauti za barani Afrika, Ulaya na Asia kwa kuangalia ukubwa wa hospitali, gharama kwa mita za mraba, kiwango cha huduma zinazotarajiwa

na mwaka wa ujenzi wa mradi. Matokeo ya ulinganifu huo yameonesha kuwa mradi wa ujenzi wa Muhimbili mpya una gharama nafuu ikilinganishwa na miradi kutoka nchi nyingine. Kati ya hospitali zote zilizolinganishwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili ina eneo kubwa la ujenzi kuliko miradi mingine (mita za mraba 115,000), na gharama za ujenzi katika nchi hizo zinakadiriwa kati ya Dola za Marekani 3,000 hadi 7,000 kwa mita za mraba wakati mradi wa Muhimbili mpya utagharimu Dola za Marekani 1,819 kwa mita za mraba. Kwa ulinganifu huu ina maana kwamba, wakati baadhi ya nchi zinalipa mara mbili au zaidi kwa kila mita za mraba, gharama kwa nchi yetu itakuwa chini kwa wastani wa asilimia 42. Tanzania inakwenda kupata hospitali kubwa kwa gharama nafuu na huu si ushahidi wa matumizi mabaya bali ni uwekezaji wa busara na wa thamani nzuri ya fedha za umma.

### Hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila

**152.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ya Taifa Muhimbili – Mloganzila iliendelea kushuhudia ongezeko la utoaji wa huduma ikilinganishwa na mwaka uliopita. Katika kipindi hiki, jumla ya wagonjwa 229,281 walihudumiwa. Kati yao, wagonjwa wa nje ni 215,295 na wagonjwa 13,986 ni wa kulazwa.

**153.** ***Mheshimiwa Spika***, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi ambazo ni pamoja na upandikizaji wa figo kwa wagonjwa tisa (9) na kufanya jumla ya wagonjwa 24 tangu huduma hii ilipoanzishwa mwaka 2023. Gharama ya upandikizaji wa figo kwa mgonjwa ni Shilingi 37,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 120,000,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma ya kuweka puto tumboni kwa wagonjwa tisa (9) hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliohudumiwa

tangu huduma hiyo kuanza mwaka 2022 kufikia 192. Gharama ya huduma hiyo ni Shilingi 5,500,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shillingi 26,565,000 kama mgonjwa angetibiwa nje ya nchi. Hospitali imeendelea kutoa huduma ya upandikizaji wa meno kwa wagonjwa 26 na kufanya idadi ya wagonjwa kufikia 55 tangu huduma hii ilipoanzishwa mwaka 2024/2025. Vilevile, huduma za kubadilisha goti na nyonga zilitolewa kwa wagonjwa 58, upasuaji rekebishi wagonjwa wanne (4) na upasuaji wa kupunguza ukubwa wa tumbo la chakula kwa wagonjwa watatu (3).

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 43,705 vya Radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo, *MRI* 3,141, *CT Scan* 3,400, *x-ray* 16,441, *Mammograph* 231, *Ultrasound* 16,149 na *x-ray* maalum za uchunguzi wa magonjwa ya kinywa na meno 2,127. Pia, jumla ya vipimo vya maabara 456,918

vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa. Kwa ujumla, huduma za uchunguzi zimeendelea kutoa matokeo sahihi na ya wakati kwa ajili ya kusaidia matibabu.

**155.** ***Mheshimiwa Spika*****,** hospitali imetoa huduma za mkoba katika hospitali ya rufaa ya Ndanda – Mtwara kwa wagonjwa 2,064 na kati yao 29 walifanyiwa upasuaji. Aidha, katika kutekeleza sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali ilitoa misamaha ya huduma yenye thamani ya Shilingi 3,499,697,791 kwa wagonjwa 12,350. Kwa upande wa Tiba Utalii, wagonjwa 240 kutoka nchi jirani za Uganda, Sudan, Kenya, Comoro, Malawi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo walihudumiwa.

## Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI)

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imetoa huduma kwa wagonjwa 169,313 kati ya wagonjwa hao, waliolazwa ni 25,441 na wagonjwa wa nje ni

143,872. Taasisi imeweza kufanya huduma ya kuchunguza mishipa ya miguu kwa wagonjwa 59 na kuzibua mishipa ya miguu kwa wagonjwa 14. Kutibu shinikizo la juu sugu kupitia tundu dogo (Renal Denervation) kwa wagonjwa 6 pamoja na kutibu magonjwa ya moyo kwa njia ya *Transcatheter Aortic Valve Implantation* kwa mgonjwa mmoja (1). Huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni uchunguzi wa mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 967, kufunga vifaa visaidizi vya moyo kwa wagonjwa 129, kuzibua mishipa ya damu ya moyo kwa wagonjwa 217, kutibu hitilafu ya mfumo wa umeme wa moyo kwa wagonjwa 37, kuziba matundu ya moyo kwa watoto wagonjwa 192 na kuchunguza matatizo ya moyo kwa watoto wagonjwa 111.

**157. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu kwa

wagonjwa 339 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 8,927 tangu kuanza kwa huduma hiyo mwaka 2015. Gharama ya kufanya upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua na mishipa ya damu ni wastani wa Shilingi 15,450,000 kwa mgonjwa mmoja ndani ya nchi ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 50,800,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi. Vilevile, Taasisi imefanikiwa kufanya upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo kwa wagonjwa 1,974 na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliopatiwa huduma hii kufikia 38,739 tangu huduma hizo zilipoanza kutolewa. Gharama ya kufanya upasuaji huo ni wastani wa Shilingi 6,000,000 kwa mgonjwa mmoja ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 20,000,000 kwa mgonjwa mmoja akitibiwa nje ya nchi.

***158. Mheshimiwa Spika***, Taasisi ilitoa msamaha kwa wagonjwa 880 wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu zenye thamani ya Shilingi 1,350,858,947 katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi

2026, ikilinganishwa na gharama ya Shilingi 825,762,214 kwa wagonjwa 710 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Huduma zilizoongoza kuolewa misamaha ni pamoja na vipimo vya maabara, upasuaji wa moyo kwa njia ya tundu dogo na malazi kwa upande wa wagonjwa mahututi.

***159.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ya moyo ambapo vipimo vya ECHO vilikuwa 19,931 *Holter* vilikuwa 2,368, *Stress ECG* vilikuwa 2,971 *Dobutamine* vilikuwa 46, *Stress ECHO* vilikuwa 12 na *Sparkle Traching ECHO* vilikuwa 1,086, *Transosophageal ECHO* vilikuwa 26, *X-Ray* vilikuwa 18,066, *Ultra Sound* vilikuwa 17,854, *ECG* vilikuwa 17,699 *Ultra Functional Test* vilikuwa 281, *Lung functional test* vilikua 60 na *ABP* vilikuwa 1,980. Aidha, jumla ya vipimo vya maabara 512,066 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa ikilinganishwa na vipimo 405,258 kipindi kama hicho mwaka 2024/2025.

**160. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza *Dkt. Samia Cardiac Outreach Program,* Taasisi imeendelea kutoa huduma za mkoba katika Mikoa ya Dar es Salaa, Geita na Arusha ambapo jumla ya wagonjwa 6,870 walifikiwa na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliopatiwa huduma tangu taasisi imeanza kutoa huduma za mkoba mwaka 2015 kufikia 54,192. Jumla ya wagonjwa 14,119 walipatiwa vipimo vya *ECHO* na *ECG* kupitia huduma hizo za mkoba na wagonjwa wapya 4,602 sawa na asilimia 33 waligundulika kuwa na magonjwa ya moyo.

**161. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 234 waliofika nchini na wagonjwa 3,163 walipatiwa huduma katika nchi za Comoro na Zambia na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliotibiwa kufikia 3,360. Wagonjwa waliotibiwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete walitoka nchi za Msumbiji, Misri, Comoro, Malawi, Zambia, Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. Vilevile, kutokana na kuimarika kwa huduma

za ubingwa za upasuaji wa moyo, Taasisi imezijengea uwezo nchi za Malawi, Rwanda na Zambia.

**Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI)**

**162.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Taasisi imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 224,715 kati yao wagonjwa wa kulazwa ni 9,882 na wagonjwa wa nje ni 214,833. Aidha, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, Taasisi imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 5,169,995,385.26 kwa wagonjwa 19,190 na huduma zilizoongoza kwa msamaha ni pamoja na upasuaji, uchunguzi wa mionzi, kulazwa, vipimo vya maabara pamoja na dawa.

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupanua wigo wa huduma zinazotolewa, Taasisi imeanzisha huduma mpya zifuatazo; upasuaji wa ubongo bila kufungua fuvu, upasuaji wa mgongo kwa kufungua eneo

dogo, upasuaji wa kunyoosha mgongo uliopinda, upasuaji wa kuondoa uvimbe kwenye ubongo kupitia tundu la pua, huduma ya kutibu maumivu sugu ya mgongo, kuweka tiba sementi kwenye pingili za mgongo, upasuaji rekebishi wa viungo vilivyopooza, huduma ya upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu. Aidha, huduma zingine za ubingwa bobezi zimendelea kutolewa kwa jumla ya wagonjwa 5,836 walihudumiwa kwa mafanikio makubwa na kuwezesha Serikali kuokoa Shilingi bilioni 318 ambazo zingetumika iwapo wagonjwa hao wangepewa rufaa kwenda kutibiwa nje ya nchi.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 74,809 vya radiolojia vilifanyika, Kati ya hivyo vipimo vya *MRI* vilikuwa 12,070, *CT scan* vipimo 7,850, *X-Ray* vipimo 50,633 na *ultrasound* vipimo 4,256. Aidha, jumla ya vipimo vya maabara 163,023 vilifanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

***165. Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeendelea kutoa huduma mkoba, ambapo jumla ya wagonjwa 13,204 walihudumiwa, kati yao wagonjwa 1,245 walifanyiwa upasuaji. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 365 kutoka nchi za Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji, Burundi, Sudani Kusini, Uganda na Rwanda. Wananchi wa mataifa mengine wamekuwa na imani kubwa na tiba zetu kutokana na kuimarika na kuaminika kwa huduma za ubingwa bobezi hapa nchini.

**Taasisi ya Saratani Ocean Road**

***166. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Taasisi ilihudumia jumla ya wagonjwa 62,976 kati yao, wagonjwa wa nje ni 60,840 na wagonjwa wa kulazwa ni 2,136. Huduma za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na tiba mionzi bobezi, tiba ya mionzi ya ndani (3D brachytherapy) na tiba bobezi kupitia dawa za

*Immunotherapy*. Jumla ya wagonjwa 396 walitibiwa kwa tiba ya mionzi bobezi, wagonjwa 4,978 walitibiwa kwa tiba mionzi ya ndani na jumla ya wagonjwa 2,132 walipata tiba za immunotherapy. Vilevile, Taasisi imekamilisha usimikaji wa mashine tatu (3) mpya za kisasa ikiwemo moja (1) ya *Linear Accelerator - LINAC* itakayowezesha utoaji wa huduma za tiba mionzi bobezi (*Volumetric Arch Therapy* na *Stereotactic Body Radiotherapy) na* mashine 2 za tiba mionzi za cobalt 60*.* Uwepo wa mashine hizo umepunguza kwa kiasi kikubwa muda wa wagonjwa kupata matibabu. Pia, huduma za upasuaji mdogo wa magonjwa ya saratani ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 3,249 walifanyiwa upasuaji.

***167. Mheshimiwa Spika*,** Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba mionzi (3D-CRT) ambapo kwa kipindi hiki, tiba mionzi 173,786 zimetolewa ikilinganishwa na tiba mionzi 151,946 zilizotolewa katika kipindi kama hicho kwa 2024/2025. Tiba mionzi ya 3D-CRT ilianza mwaka 2019 ambapo hadi sasa

jumla ya tiba mionzi 1,497,542 zimetolewa. Aidha, Taasisi imetoa tiba kemia 28,279 ikilinganishwa na tiba kemia 25,754 katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Hadi sasa jumla ya tiba kemia 527,842 zimetolewa tangu kuanzishwa kwa huduma hii mwaka 2017. Pia, Taasisi imeendelea kutoa huduma za tiba shufaa kwa wagonjwa 46,551 ikilinganishwa na wagonjwa 35,715 kwa mwaka 2024/2025.

**168. *Mheshimiwa Spika*,** Huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali zimeendelea kuimarika ambapo jumla ya vipimo vya maabara 192,294 vimefanyika ikilinganishwa na vipimo 171,930 katika kipindi cha mwaka 2024/2025. Kwa upande wa radiolojia, vipimo 20,053 vimefanyika ikilinganishwa na vipimo 18,694 vilivyofanyika kipindi kama hicho cha mwaka 2024/2025. Kati ya vipimo hivyo, vipimo 6,552 ni vya *X-Ray*, 7,722 vya *ultrasound*, 3,268 vya *CT scan*, 2,050 vya *MRI*, 193 vya *mammograph* na 268 *Interventional Radiology*.

**169. *Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi wa *PET - CT* scan ambao ulihusisha ujenzi wa *bunkers* na ununuzi na usimikaji wa mashine za PET - CT scan na Cyclotron umekamilika na huduma zinaendelea kutolewa. Huduma za uchunguzi kwa PET – CT scan kwa kutumia kitendanishi cha Gallium zilianza kutolewa Julai 2024 na jumla ya wagonjwa 574 wamechunguzwa. Vilevile, Serikali imewezesha kupatikana kwa Shilingi bilioni 2.1 kwa ajili ya mafunzo ya wataalam na ununuzi wa malighafi za uzalishaji kitendanishi cha *FluoroDeoxyGlucose* (FDG). Mashine ya Cyclotron imeanza uzalishaji wa FDG - 18 mwezi Machi 2026 na hivyo kuongeza idadi ya wagonjwa wanaochunguzwa kupitia mashine ya *PET - CT* scan kutoka wagonjwa watano (5) hadi wagonjwa 20 kwa siku.

**170. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha, wagonjwa 26,808 walipewa msamaha wa jumla ya Shilingi 13,461,853,093.86. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni tiba mionzi, tiba za

kibaiolojia, dawa za tiba kemia, uchunguzi wa maabara, radiolojia na huduma za kulazwa. Aidha, Taasisi imetoa huduma mkoba katika mikoa saba (7) ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani, Tanga, Geita, Mara, na Dodoma na kuhudumia jumla ya wateja 6,825. Huduma zilizotolewa ni pamoja na uchunguzi wa saratani ya matiti, saratani ya mlango wa kizazi, ngozi, utumbo mpana, tezi dume na utoaji wa elimu.

**171.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, jumla ya wagonjwa 533 kutoka nje ya nchi walipatiwa huduma za uchunguzi na tiba ya saratani ikilinganishwa na wagonjwa 607 waliopata huduma hiyo kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Malawi, Kenya, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Msumbiji, Sudani ya Kusini, Zambia, Marekani, Rwanda, Burundi na Uganda.

## Hospitali ya Benjamin Mkapa

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** hospitali imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 224,645. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 11,061 na wagonjwa wa nje ni 213,584. Hospitali imeendelea kuimarisha huduma za ubingwa bobezi za upasuaji wa moyo kwa watu wazima na watoto ambapo wagonjwa 12 wamenufaika. Gharama ya kumtibu mgonjwa mmoja wa upasuaji wa moyo ni wastani wa Shilingi 70,000,000 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 210,000,000 iwapo matibabu hayo yangefanyika nje ya nchi.

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa na hospitali ni pamoja na upandikizaji wa uloto kwa wagonjwa tisa (9) na hivyo kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia 30 toka huduma ilipoanzishwa mwaka 2023. Pia, hospitali imefanikiwa kupandikiza figo wagonjwa nane (8) na kufanya idadi ya wagonjwa waliofanyiwa huduma hii kufikia

wagonjwa 58 tangu kuanzishwa 2018. Hospitali ilifanikiwa kufanya huduma ya uvunjaji wa mawe kwenye mfumo wa mkojo kwa wagonjwa 173. Huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upasuaji wa nyonga na magoti kwa wagonjwa 180, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kwa wagonjwa 405 na upasuaji wa moyo na huduma zitolewazo kwa kutumia mtambo maalum wa *cathlab* kwa wagonjwa 252. Katika kuimarisha wigo wa huduma, hospitali imeanzisha huduma mpya ikiwemo kurefusha miguu kwa wagonjwa 11 pamoja na huduma ya upasuaji wa kifundo cha mguu kwa wagonjwa wawili (2).

***174. Mheshimiwa Spika,*** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 75,059 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya vipimo hivyo *MRI* 4,841, *CT scan* vipimo 4,976, *X-Ray* vipimo 24,561, *fluoroscopy* 1,341, *mammography* 436 na *ultrasound* vipimo 38,904. Aidha, jumla ya vipimo vya maabara

398,296 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

***175. Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 448,917,605.50 kwa wagonjwa 1,894. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni pamoja na uchujaji damu, vipimo vya maabara, kitengo cha wagonjwa mahututi, huduma za upasuaji, kumuona daktari na dawa.

**Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe**

***176. Mheshimiwa Spika***, hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kipimo cha umeme wa Ubongo *EEG* kilifanyika kwa wagonjwa 71, *ECHO* wagonjwa 615, *ECG* wagonjwa 684, *X-Ray* wagonjwa 3,159, na *ultrasound* wagonjwa 2,541. Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya vipimo vya maabara 37,851 vimefanyika kwa

kutumia vifaa vya kisasa. Vilevile, hospitali ilitoa huduma mkoba zilizolenga huduma za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia katika mikoa ya Dodoma, Manyara na Ruvuma ambapo jumla ya wateja 915 walihudumiwa.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** hospitali imeendelea kutoa huduma za matibabu ya afya ya akili kwa wananchi, mahabusu na wafungwa kwa mujibu wa Sheria. Vilevile, hospitali inatoa huduma za matibabu kwa waraibu wa aina mbalimbali ikiwemo waathirika wa dawa za kulevya. Hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 64,868, kati yao wagonjwa wa nje ni 63,195 na wagonjwa wa kulaza ni 1,673. Aidha wagonjwa 13,063 sawa na asilimia 20 ni wagonjwa wa akili na wagonjwa 51,805 sawa na asilimia 80 ni wagonjwa wa magonjwa mengine. Kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa akili wahalifu waliothibitishwa na vyombo vya kisheria wanaotibiwa sehemu ya Isanga, ambapo jumla ya wagonjwa 474 walithibitishwa na wanaendelea na matibabu.

***178. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza sera ya msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya shilingi 571,868,514.7 kwa wagonjwa 8,976. Huduma zilizotolewa msamaha ni pamoja na matibabu, chakula, mavazi na malazi.

**Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto**

***179. Mheshimiwa Spika,*** hospitali Maalum ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto imeendelea kutoa huduma za tiba, kinga na tafiti. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 21,242. Kati ya wagonjwa waliohudumiwa, wagonjwa wa nje ni 20,484 na wagonjwa wa kulazwa ni 758. Aidha, kati ya wagonjwa 21,242 waliohudumiwa, wagonjwa wa kifua kikuu walikuwa 506 (kifua kikuu cha kawaida 408 na kifua kikuu sugu 98), wagonjwa wa UKIMWI 908 na magonjwa mengine 19,828.

**180. *Mheshimiwa Spika,*** kati ya wagonjwa wa kulazwa 758, wagonjwa wa Kifua Kikuu sugu walikuwa 98 ambao ni rufaa kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ambao hulazwa kwa muda wa wastani wa miezi sita (6) wakipatiwa matibabu, chakula, chakula dawa kwa wenye utapiamlo mkali na mahitaji mengine muhimu ya kijamii. Idadi ya wagonjwa waaliolazwa kutokana na mapafu kuathirika na vumbi la silica kutoka maeneo ya migodini walikuwa 50 ambao wanakuwa tegemezi wa hewa tiba ya oksijeni maisha yao yote. Kwa wastani hospitali hutumia mitungi 60 kwa siku kuhudumia wagonjwa hao.

**181. *Mheshimiwa Spika,*** hospitali ina maabara ya Afya ya Jamii ya usalama wa kibaiolojia daraja la tatu yenye ithibati ya kimataifa ISO:15189 yenye vifaa vya kisasa vya uchunguzi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya vipimo vya uchunguzi wa maabara vilivyofanyika ni 33,286. Kati ya hivyo vipimo vya radiolojia 3,583 (X-Ray 2,444, *Ultrasound* 593, ECHO 388, Doppler

Ultrasound 22 na CT scan vipimo 136). Aidha, katika kutekeleza sera ya msamaha, hospitali ilihudumia wagonjwa 1,147 kwa msamaha kwa gharama ya Shilingi 786,048,490. Huduma zinazoongoza kutolewa msamaha ni huduma ya hewa tiba hasa kwa wagonjwa wa silicosis, huduma za dawa, kumuona daktari, uchunguzi wa maabara na radiolojia.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Ziwa Bugando**

***182. Mheshimiwa Spika,*** hospitali imetoa huduma kwa wagonjwa 286,934. Kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 21,206 na wagonjwa wa nje ni 286,934. Hospitali imeendelea kutoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi, ambazo ni matibabu ya magonjwa ya figo, kisukari, damu, njia ya chakula, ngozi, watoto, saratani, mfumo wa upumuaji, afya ya akili, huduma za dharura na ajali na huduma ya tiba viungo na utengemano.

**183. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi za upasuaji kwa wagonjwa 8,750 katika maeneo ya nyonga, magoti, kinywa na meno, mdomo sungura kwa watoto, macho, masikio, pua na koo, kifua, moyo, ubongo, mishipa ya fahamu na uti wa mgongo, mfumo wa mkojo, upasuaji sanifu, upasuaji maalum wa watoto, upasuaji wa matundu madogo na huduma ya viungo tiba na vifaa tiba saidizi. Aidha, kati ya waliofanyiwa upasuaji wagonjwa 8,290 walifanyiwa upasuaji mkubwa na wagonjwa 460 walifanyiwa upasuaji mdogo.

**184. *Mheshimiwa Spika*,** wagonjwa 12,820 wamepatiwa huduma ya matibabu ya saratani kati yao, wagonjwa 12,072 ni wagonjwa wa nje 748 ni wagonjwa wa kulazwa, wagonjwa 6,913 walipatiwa tiba kemia ya saratani na wagonjwa 3,346 walipatiwa tiba kwa kutumia mionzi. Aidha, utoaji wa huduma hizo umepunguza adha ya wagonjwa kufuata huduma hizo katika Taasisi ya Saratani Ocean Road.

**185. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo katika kipindi hiki vipimo 46,501 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya MRI 2,236, CT-Scan 5,355, X-Ray 18,367, *ultrasound* 19,661, *mammography* 137, *fluoroscopy* 502 na *Interventional radiology* 1,052. Katika kipindi hiki, jumla ya vipimo vya maabara 887,550 vimefanyika kwa kutumia vifaa vya kisasa.

**186. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeendelea kutoa huduma za mkoba kwa vituo 19 ambapo wagonjwa 13,702 walipatiwa huduma na kati yao 157 walifanyiwa Upasuaji. Aidha, katika kutekeleza Sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 1,739,468,790 kwa wagonjwa 6,647. Huduma zinazoongoza kutolewa misamaha ni pamoja na, mionzi tiba, utoaji wa dawa za mionzi, magonjwa ya akili, huduma za matibabu ya watoto wachanga, mama wajawazito, huduma ya

kuchuja damu na huduma kwa wazee wasiojiweza. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia wagonjwa 82 raia wa nchi za Kenya, Uganda, Rwanda na Zambia.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya**

***187. Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuhudumia jumla ya wagonjwa 193,823 ambapo kati yao, wagonjwa wa kulazwa ni 60,223 na wagonjwa wa nje ni 133,600. Aidha, huduma zilizoendelea kutolewa ni pamoja na upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, matibabu ya mfumo wa chakula na ini, huduma ya mfumo wa upumuaji pamoja na huduma ya upasuaji kwa watoto wachanga. Jumla ya wagonjwa wapatao 1,644 wamepatiwa huduma za ubingwa bobezi.

**188. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo jumla ya vipimo 55,547 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo *MRI* ni 590, *CT scan* 3,423, *X-ray* 13,921 *fluoroscopy* 12,702 na *utrasound* 24,911. Vipimo vya maabara 191,900 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa.

**189. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 1,111,678,330 kwa wagonjwa 31,766. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni pamoja na kumuona daktari, kulazwa pamoja na upasuaji kwa wajawazito wa kumtoa mtoto tumboni. Katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 190 kutoka nchi za Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Zambia na Msumbiji.

**190. *Mheshimiwa Spika*,** kwa kutumia wataalam wa ndani, Hospitali imebuni

mfumo wa kudhibiti joto “automatic temperature control” katika chumba cha watoto wachanga na watoto njiti. Pia, mfumo wa e-Medical unaotumika katika shughuli mbalimbali za hospitali ikiwemo kuona wagonjwa umebuniwa na wataalam wetu na umefungwa katika baadhi ya hospitali za kanda, taifa na hospitali binafsi. Wabunifu hao wametambuliwa na kupewa hati za ufanyakazi hodari na **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani mwaka 2025.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini – KCMC**

**191.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 193,379. Kati ya hao wagonjwa wa nje ni 178,688 na wagonjwa wa ndani ni 14,691. Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa bobezi ambapo jumla ya wagonjwa 7,998

wamefanyiwa upasuaji katika fani za upasuaji wa ubongo, upasuaji wa ubingwa katika njia ya mkojo, upasuaji wa mgongo na uti wa mgongo, upasuaji wa ubingwa wa kinywa na meno, macho, masikio, pua na koo na upasuaji wa utumbo mpana.

**192. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi ambapo wagonjwa 2,211 walifanyiwa kipimo cha *MRI, CT scan* 4,651, *ultrasound* 12,444, *X-Ray* 20,292, *mamography* 222. Kwa upande wa vipimo vya maabara, Taasisi ilifanya jumla ya vipimo 208,798. Aidha, Hospitali imetoa huduma za msamaha kwa wagonjwa 1,786 wenye thamani ya Shilingi 1,897,185,255. Huduma zilizoongoza kutolewa msamaha ni matibabu ya Saratani, Dawa, Vipimo na Kulazwa. Vilevile, hospitali imeendelea kutoa huduma mkoba, katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ambapo zaidi ya wagonjwa 2,500 walipatiwa huduma za saratani, macho na VVU/UKIMWI

**193. *Mheshimiwa Spika,*** katika dhana ya kuendeleza tiba utalii nchini, hospitali imeimarisha ubora wa huduma kwa kuweka mikakati ya kuvutia wateja wa kimataifa. Katika kipindi hiki hospitali imehudumia wateja 399 kutoka nchi mbalimbali, zikiwemo za Afrika Mashariki (Kenya, Uganda, Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, na Sudan kusini) pamoja na raia wa mataifa nje ya Afrika. Huduma hizo zimechangia kuongeza mapato ya Shilingi 335,679,733. Aidha, katika hatua nyingine ya kuongeza vyanzo vya mapato na ubora wa huduma, hospitali imeanzisha huduma za kliniki binafsi ambapo hadi sasa imehudumia zaidi ya wagonjwa 1,466 tangu kuanzishwa kwake mwezi Oktoba 2025.

## Hospitali ya Rufaa ya Kanda Chato

**194. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, hospitali imetoa huduma kwa jumla ya wagonjwa 46,252 ikiwa wagonjwa wa nje ni 43,168 na wagonjwa wa kulazwa ni 3,084. Hospitali

imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika fani za mifupa, ubongo na mishipa ya fahamu ambapo jumla ya wagonjwa 6,184 walihudumiwa. Aidha, hospitali imeanzisha kliniki ya ubingwa ya selimundu ambapo jumla ya wagonjwa 4,198 wamehudumiwa. Vilevile, hospitali inaendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi za magonjwa ya moyo kwa kushirikiana na Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete ambapo kwa kipindi hiki jumla ya wagonjwa 8,324 wamehudumiwa.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa magonjwa mbalimbali ambapo vipimo 13,669 vya radiolojia vilifanyika. Kati ya hivyo vipimo vya *MRI* vilikuwa 268, *CT Scan* 487, *X-Ray* 3,343, *Dental X-Ray* 149, *ultrasound* 4,674, *ECHO* 3,099 na *ECG* 1,649. Jumla ya vipimo vya maabara 44,586 vimefanyika kwa kutumia mashine za kisasa.

**196.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza sera ya kutoa msamaha kwa wagonjwa

wasio na uwezo wa kumudu gharama, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye gharama ya Shilingi 222,797,016 kwa wagonjwa 1,063. Katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali ilihudumia wagonjwa 21 raia wa nchi za Uganda, Rwanda na Burundi.

**Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini – Mtwara**

***197. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali rufaa ya kanda Mtwara ili kuiwezesha kuwa na uwezo wa kutoa huduma nyingi za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo hospitali imehudumia jumla ya wagonjwa 36,550. Kati yao, wagonjwa wa nje ni 34,329 na wagonjwa wa kulazwa ni 2,221. Hospitali ilifanikiwa kutoa huduma za ubingwa kwa wagonjwa 20,706 katika fani za upasuaji, magonjwa ya moyo, magonjwa ya wanawake na uzazi, magonjwa ya ndani, magonjwa ya masikio pua na koo na magonjwa ya watoto.

**198. Mheshimiwa Spika,** hospitali imeendelea kutoa huduma za uchunguzi wa ubingwa ambapo imefanikiwa kusimika mashine ya C-Arm kwa ajili ya uchunguzi wa radiolojia na kuanzisha kitengo cha uchunguzi wa vinasaba. Kwa upande wa vipimo vya radiolojia, wagonjwa 399 walifanyiwa kipimo cha *MRI, CT-scan* wagonjwa 681, *ultrasound* wagonjwa 4531, *X-ray* wagonjwa 4740 na vipimo vya maabara 68,061.

**199. Mheshimiwa Spika,** hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa za mkoba katika mkoa wa Mtwara kwa ajili ya matibabu ya pua masikio na koo, macho, ngozi, watoto na meno ambapo jumla ya wagonjwa 1,684 walipatiwa matibabu, kati yao 61 walifanyiwa upasuaji. Katika kutekeleza sera ya kutoa huduma ya msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu, hospitali imetoa msamaha wenye thamani ya Shilingi 25,116,331 kwa wagonjwa 308. Aidha, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii nchini,

hospitali ilihudumia jumla ya wagonjwa 248 kutoka nchi za jirani.

**Hospitali ya Kanda ya Mashariki – CCBRT**

***200. Mheshimiwa Spika,*** hospitali imeendelea kutoa huduma mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ambapo jumla ya wagonjwa 85,178 walihudumiwa ikilinganishwa na wagonjwa 88,808 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kati yao wagonjwa wa nje ni 81,104 na wagonjwa wa ndani ni 4,074. Aidha, wagonjwa wenye ulemavu waliohudumiwa ni 10,672 ikilinganishwa na wagonjwa 9,557 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Hospitali imeendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika fani za upasuaji rekebishi kwa wagonjwa 98, upasuaji kwa njia ya matundu madogo kwa wagonjwa 52, kutoa uvimbe kwenye tezi za uzazi kwa wagonjwa saba (7), kufunga mirija ya uzazi kama njia ya uzazi wa mpango wagonjwa 10, upasuaji wa ndani ya kizazi kwa njia ya kamera mgonjwa mmoja

(1) na huduma ya uchunguzi kwa njia ya matundu madogo wagonjwa 14, kuweka lensi kwenye mboni wagonjwa 196 na upasuaji wa makengeza kwa watoto 20.

**201. *Mheshimiwa Spika*,** huduma nyingine za ubingwa na ubingwa bobezi ziliendelea kutolewa ambapo jumla ya wagonjwa 5,233 walifanyiwa upasuaji wa macho, fistula itokanayo na uzazi, mifupa, mdomo sungura na miguu kifundo. Aidha, wagonjwa 747 walipata viungo saidizi. Vilevile, hospitali kupitia kituo cha huduma za utengemao kilichopo Moshi ilitoa huduma ya utengemao kwa wagonjwa 3,338 katika maeneo ya upasuaji wa macho, upasuaji wa mtoto wa jicho kwa njia ya vitundu vidogo, upasuaji wa pazia la jicho, makengeza na upasuaji wa nyonga na goti bandia. Huduma hizo zimeboresha maisha ya watu ambao wangeweza kuwa walemavu wa macho au viungo vingine.

**202. *Mheshimiwa Spika*,** hospitali imeimarisha huduma za uchunguzi zinazoendana na

huduma za ubingwa na ubingwa bobezi kwa kuimarisha utendaji wa vifaa vya maabara ambapo jumla ya vipimo 54,435 vilitolewa. Kwa upande wa vipimo vya radiolojia, wagonjwa 237 walifanyiwa kipimo cha *CT - Scan*, wagonjwa 4,742 *ultrasound* na wagonjwa 4,737 *X-Ray*. Pia, hospitali imenunua mashine ya kisasa ya *ultrasound* ya macho kwa ajili ya upimaji wa kibobezi wa pazia la nyuma ya jicho.

**203. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza sera ya kutoa huduma ya msamaha kwa wagonjwa wasioweza kumudu gharama za matibabu, hospitali imetoa huduma za msamaha zenye thamani ya Shilingi 2,100,180,013.52 kwa wagonjwa 3,976. Aidha, hospitali imeendelea kutoa huduma mkoba kwa wagonjwa 5,819 kupitia vituo vya utengemao vilivyoko kwenye jamii na huduma za majumbani. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya tiba utalii, hospitali imetoa huduma za matibabu ya afya ya macho, vifaa saidizi vya macho, mifupa na fistula ya uzazi kwa raia wa nchi jirani

ambapo jumla ya wagonjwa 374 walihudumiwa.

## Hospitali za Rufaa za Mikoa

**204.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 hospitali 28 za rufaa za mikoa zimehudumia wagonjwa 2,789,223 kati yao wa kulazwa ni 366,027 na wa nje ni 2,423,196 ikilinganishwa na wagonjwa 2,628,784 waliohudumiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, katika kutekeleza sera ya msamaha kwa wagonjwa wasio na uwezo wa kumudu matibabu, hospitali zilitoa msamaha kwa wagonjwa 116,117 wenye thamani ya Shilingi 2,735,855,307 ikilinganishwa na misamaha ya Shilingi 2,630,043,203 kwa wagonjwa 134,145 iliyotolewa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

**205.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa hospitali zote za rufaa za mikoa zinakuwa na uwezo wa kutoa huduma za ubingwa katika fani nane (8) ambapo kwa

sasa hospitali 18 kati ya 28 zimeweza kufikisha lengo ikilinganishwa na hospitali 15 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Sanjari na lengo hilo, Wizara inaendelea kutekeleza mkakati wa kuongeza idadi ya fani za ubingwa kufikia 17 katika hospitali zote za rufaa za mikoa. Fani hizo ni magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, afya ya watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, afya ya macho, magonjwa ya ngozi, huduma za dharura, utoaji wa dawa za usingizi na ganzi, radiolojia, magonjwa ya damu, magonjwa ya saratani na patholojia. Aidha, idadi ya madaktari bingwa imeongezeka katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka 402 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 hadi kufikia madaktari 497 Machi, 2026.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** hospitali zimetoa huduma mkoba kwa wagonjwa 41,657 ambapo kati yao 2,259 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 68,058

waliohudumiwa na 5,121 waliofanyiwa upasuaji kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Huduma zilizotolewa ni magonjwa ya kinamama na afya ya uzazi, magonjwa ya ndani, watoto, afya ya akili, upasuaji, upasuaji wa mifupa, magonjwa ya njia ya mkojo, afya ya kinywa na meno, masikio, pua na koo, macho, ngozi, utoaji wa dawa za usingizi, ganzi na radiolojia. Uanzishwaji wa huduma mpya na utoaji wa huduma mkoba umewezesha wananchi kupata huduma kwa haraka katika mikoa yao, kupunguza gharama za matibabu na kupunguza msongamano katika hospitali za rufaa za kanda, maalum na taifa.

**207. *Mheshimiwa Spika,*** jumla ya vipimo vya radiolojia 410,797 vilifanyika. Kati ya hivyo *CT scan* 35,025, *Ultra Sound* 193,365 na *X-ray* 181,406. Aidha, jumla vya vipimo 2,317,017 vya maabara vilifanyika. Vilevile, katika kuendeleza dhana ya tiba utalii nchini, hospitali za rufaa za mikoa na hasa zilizopo pembezoni mwa mipaka ya nchi, zilihudumia wagonjwa 616 kutoka nchi jirani za Malawi,

Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo, Burundi, Kenya, Uganda na Msumbiji.

### Huduma za Uuguzi na Ukunga

**208.** ***Mheshimiwa Spika*****,** uuguzi na ukunga umeendelea kuwa muhimili muhimu katika utoaji wa huduma bora za afya nchini ambapo asilimia 80 ya huduma hutolewa na kada hiyo. Kulingana na takwimu zilizopo zinaonesha kuwa sehemu kubwa ya vifo vya wajawazito hutokea wakati wa uchungu, kujifungua na baada ya kujifungua. Katika kukabiliana na hali hiyo, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wauguzi na wakunga ili kuimarisha ufuatiliaji wa uchungu wa mama mjamzito wakati na baada ya kujifungua kwa kutumia chati uchungu iliyoboreshwa.

**209.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya wakunga 1,850 kutoka mikoa saba (7) ya Mbeya, Njombe, Rukwa, Arusha, Morogoro, Pwani na Kilimanjaro walipatiwa mafunzo. Hii imeongeza idadi ya wakunga waliopatiwa mafunzo hayo kufikia 9,093 ikilinganishwa

na 7,243 kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, hadi sasa, jumla ya vituo vya kutolea huduma 5,884 katika mikoa 22 vinatumia chati uchungu iliyoboreshwa pamoja na kutoa mafunzo kwa wakufunzi 90 wa vyuo vya afya na kujumuisha maudhui ya chati uchungu kwenye mitaala ya vyuo vikuu mbalimbali ikiwemo Bugando, Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, KCMC, Mwanza University, Kairuki, St. John, Aga Khan na Chuo kikuu cha Dodoma.

***210. Mheshimiwa Spika***, jumla ya vituo vya kutolea huduma 1,244 vimeanza kutoa huduma ya mama mwambata (birth companionship) ikilinganishwa na vituo 847 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kupitia huduma hii mama mjamzito anaruhusiwa kuwa na mwenza au ndugu wa karibu aliyemchagua yeye wakati wa kujifungua. Hatua hii imechangia kuongeza ufanisi wa ufuatiliaji wa akina mama wakati wa uchungu na baada ya kujifungua, pamoja na kuboresha huduma zinazotolewa.

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika juhudi za kuhakikisha huduma za afya zinatolewa kwa kuzingatia utu, heshima na staha, Wizara imetengeneza bango kitita ili kuongoza watumishi kutoa huduma staha na mawasiliano madhubuti. Kupitia juhudi hizo wauguzi na wakunga 3,500 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Katavi, Kigoma, Songwe, na Mtwara wamejengewa uwezo na kufanya idadi yao kufikia 15,700 ikilinganishwa na wauguzi na wakunga 12,000 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 30.8. Sanjari na mafunzo hayo, jumla ya vituo vya kutolea huduma 413 vimeanzisha madawati ya huduma kwa mteja ili kuongeza ufanisi wa kushughulikia kero za wananchi yaliyosaidia kuimarisha mawasiliano kati yao na watoa huduma.

212. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha utoaji wa huduma za afya unazingatia miongozo na kuimarisha ubora kwa kutekeleza zoezi la ukaguzi wa kimatibabu katika utoaji wa huduma za

uuguzi na ukunga. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, vituo vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam vilifanyiwa ukaguzi wa kimatibabu. Matokeo ya ukaguzi huo yalionesha kuendelea kuimarika kwa ubora wa huduma za Uuguzi na Ukunga na kufikia wastani wa asilimia 68 ikilinganishwa na asilimia 60 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, katika kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji na kutoa huduma bora, Wizara imewajengea uwezo wa kufanya ukaguzi wa ndani wauguzi na wakunga 456 kutoka halmashauri 162. Hatua hii inalenga kuhakikisha kuwa ukaguzi unakuwa endelevu na sehemu ya utendaji wa kila siku wa watoa huduma.

**213.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usimamizi wa ndani, Wizara imetoa mafunzo kwa wauguzi viongozi 67 kutoka hospitali za rufaa za mikoa 28 na hospitali 11 za binafsi zenye hadhi ya hospitali za rufaa za mikoa nchini kuhusu uwajibikaji na namna bora ya

kusimamia huduma za uuguzi na ukunga. Aidha, wauguzi na wakunga 241 kutoka vituo 14 vya kutolea huduma wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya hewa tiba ya oksijeni, hivyo kufanya idadi ya wauguzi na wakunga waliopatiwa mafunzo kufikia 1,001. Vilevile, katika kuimarisha usimamizi wa ubora wa huduma, Wizara imeandaa viashiria 24 vya kupima utoaji wa huduma za uuguzi na ukunga ambapo wauguzi viongozi 256 wamejengewa uwezo wa kufuatilia na kutumia viashiria hivyo.

***"Muuguzi aliyefundishwa amekuwa moja ya baraka kuu za ubinadamu! Muuguzi anatoa faraja, huruma, na huduma". Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.***

**Uhakiki Ubora wa Huduma za Afya**

**214.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya afya ili kukidhi mahitaji ya sasa, kukua kwa

teknolojia, mipango ya kitaifa na kimataifa na Dira ya Taifa 2050. Katika kutekeleza hilo, Wizara inafanya mapitio ya Sera ya Afya ya Mwaka 2007 ambapo pamoja na mambo mengine itaweka mkazo katika maboresho ya mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini hususan kwa makundi maalum na rasimu ya sera hiyo ipo katika hatua mbalimbali za maamuzi. Vilevile, maandalizi ya Sheria ya Afya yanaendelea ili kuweka msingi wa kisheria katika usimamizi na utoaji wa huduma za afya ikiwemo; uvunaji na upandikizaji wa viungo, uanzishwaji wa taasisi ya udhibiti wa gharama na huduma za afya, Taasisi ya Ithibati, uanzishwaji wa Ofisi ya Mganga Mkuu wa Serikali na Bodi za taaluma za afya na sayansi shirikishi.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kufuatilia na kuimarisha ubora wa huduma za afya kwa kutumia takwimu katika kufanya maamuzi na kuimarisha uwajibikaji katika ngazi zote za utoaji huduma ikiwemo kufanya uchambuzi wa takwimu kutoka mfumo wa kidijitali wa usimamizi shirikishi

wa AfyaSS, unaotumika kufuatilia utekelezaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, Wizara imefanya tathmini ya uhakiki ubora wa maeneo ya upimaji VVU ili kuona kama yanakidhi viwango vya ubora katika maeneo 240 kutoka vituo 156 vya kutolea huduma katika mikoa mitatu (3) ambayo ni Mtwara, Morogoro na Lindi. Kati ya maeneo yaliyofikiwa, maeneo 209 sawa na asilimia 87 yalipata daraja la nne la ubora na hivyo kukidhi viwango vya ubora vya upimaji VVU.

***216. Mheshimiwa Spika***, Wizara iliendesha zoezi la usimamizi shirikishi kwa kutumia mfumo wa kidijitali wa AfyaSS. Zoezi hilo lilihusisha ufuatiliaji wa ubora wa huduma za afya, usimamizi wa mnyororo wa dawa, tathmini ya ubora wa takwimu na tathmini ya uwepo na ufanisi wa timu za uimarishaji ubora pamoja na timu ya uchakataji wa taarifa za bidhaa za afya. Kazi hii ilitekelezwa katika mikoa nane (8) ambayo ni Kilimanjaro, Tabora, Arusha, Tanga, Dar es salaam, Pwani, Morogoro na Geita kwa

dhumuni la kuimarisha matumizi ya mfumo wa usimamizi shirikishi katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia shughuli za ubora wa huduma katika ngazi ya mkoa na halmashauri, sambamba na kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa rasilimali na huduma.

**217. *Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea na mchakato wa uanzishaji wa taasisi ya ithibati ya ubora wa huduma za afya ili kuwezesha usimamizi wa ubora wa huduma za Afya nchini. Aidha, hospitali zimeanza taratibu za kupata ithibati ya ubora wa huduma za kimataifa kama ISO, JCI, SafeCare na COHSASA. Jitihada hizi zinalenga kuhakikisha huduma zinazotolewa na Taasisi za afya nchini zinakuwa na viwango vinavyokubalika kimataifa. Wizara itatumia ithibati ya ubora katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuhakikisha wananchi wanaojiunga na bima ya afya wanapokea huduma zinazostahili na zenye viwango vinavyoridhisha.

## Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa

218. ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa na matengenezo ya vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kuwekeza kwenye maeneo makuu ya uchunguzi ambayo ni huduma za maabara, radiolojia, matengenezo ya vifaa tiba pamoja na Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

## Huduma za Maabara

219. ***Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kuna ongezeko la maabara 12 zilizopata ithibati ya kimataifa na hivyo kufanya jumla ya maabara zenye ithibati kutoka 90 hadi kufikia 102. Kati ya maabara hizo, 72 ni za umma, 24 zinamilikiwa na mashirika ya dini na maabara sita (6) ni za binafsi. Kati ya maabara hizo, maabara tatu (3) ziko katika ngazi ya taifa, sita (6) katika ngazi ya hospitali maalum, saba (7) ngazi ya Kanda, 36 ngazi ya rufaa za mikoa, 37 ngazi ya

wilaya, tisa (9) katika vituo vya afya na maabara nne (4) katika vituo vya tafiti.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeweza kujengea uwezo maabara tano (5) za usalama wa vimelea ngazi ya tatu (Biosafety level 3 – BSL 3). Maabara hizo ni Maabara ya Taifa ya Afya ya Jamii - Kibong'oto, maabara kuu ya Kifua Kikuu Muhimbili (CTRL), maabara ya hospitali ya Kanda Mbeya, Maabara ya Tafiti Kilimanjaro (KCRI) na Wakala ya Maabara ya Magonjwa ya Wanyama (TVLA). Kufuatia kukidhi vigezo vya kimaabara katika ngazi ya tatu ya usalama kwa viwango vya kimataifa, Maabara ya Tafiti Kilimanjaro imetambuliwa na Umoja wa Afrika kama maabara yenye uwezo wa kufanya kazi na vimelea hatarishi. Utambuzi huu una maana kuwa maabara hiyo inakidhi viwango vya juu vya ubora wa huduma za uchunguzi, inalinda usalama wa watumishi na sampuli dhidi ya maambukizi, na inaongeza uaminifu wa matokeo ya vipimo kitaifa na kimataifa. Aidha, hadhi hii huwezesha nchi kushiriki tafiti za kimataifa,

kubadilishana taarifa za kisayansi, na kuimarisha utayari wa kukabiliana na milipuko ya magonjwa hatarishi.

## Huduma za Radiolojia

***221. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imefanikisha upatikanaji wa huduma za radiolojia na radiolojia tiba, zikiwemo *PET CT-Scan, MRI, CT-Scan* na huduma nyingine za radiolojia katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Aidha, katika kipindi hiki Wizara imefanya usimamizi shirikishi pamoja na kuandaa miongozo mbalimbali ya vipimo vya radiolojia ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia. Vilevile, Wizara imewezesha wataalam 125 kupata mafunzo ya matumizi bora ya mashine ya *ultrasound* kutoka vituo vya kutolea huduma na vyuo vya radiografia/radiolojia pamoja na wataalam 46 wa ufundi wa vifaa tiba.

**Matengenezo ya Vifaa Tiba**

***222. Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha huduma za matengenezo ya vifaa na vifaa tiba, Wizara imeandaa miongozo ya usimamizi wa mitambo ya uzalishaji wa hewa tiba ya oksijen pamoja na kufanya usimamizi shirikishi kwa mitambo 25 ya uzalishaji wa hewa tiba ya oksijen katika vituo 25 vya kutolea huduma ya afya nchini. Vituo vilivyotembelewa ni Hospitali ya taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete, Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mtwara, Hospitali ya maalum ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto, Hospitali ya Rufaa ya Kanda - Mbeya, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tumbi, Mwananyamala, Temeke, Bombo, Mawenzi, Mt. Meru, Singida, Iringa, Bukoba pamoja na hospitali saba (7) za Halmashauri za Mafia, Ulanga, Ngara, Nzega, Mafinga, Ukerewe na Kahama.

***223. Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya matumizi, ukarabati na usimamizi wa vifaa tiba, mitambo ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni na mashine

125 za *Utrasound* zilizosimikwa katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na vyuo vya afya. Aidha, wataalam 125 wa ufundi wa vifaa tiba wamepatiwa mafunzo ya msingi ya utunzaji na matengenezo ya mashine hizo.

**Huduma za Damu Salama**

***224. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kuhakikisha uwepo wa damu salama ya kutosha nchini. Jumla ya chupa za damu 273,105 zilikusanywa ambazo ni sawa na asilimia 82 ya lengo la kukusanya chupa 332,747 kwa mwaka 2025/2026. Makusanyo hayo yamewezekana kutokana na uwekezaji katika uhamasishaji wa jamii kuhusu kuchangia damu kwa hiari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, madhehebu ya dini, timu za ukusanyaji damu za halmashauri pamoja na timu za hospitali za rufaa za kanda na mikoa. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha ubora wa huduma za damu nchini ambapo kanda sita (6) za damu salama zimeendelea kushikilia ithibati za kimataifa, kanda mpya ya Dodoma

imependekezwa kupatiwa ithibati baada ya kufanyiwa ukaguzi mwezi Februari 2026. Ithibati hizi zina maana kuwa huduma za damu zinakidhi viwango vya kimataifa vya ubora na usalama, hivyo kupunguza hatari ya maambukizi kupitia damu na kuongeza ufanisi wa huduma za afya. Vilevile, huongeza hadhi ya nchi kimataifa kwa kuonesha uwezo wa kutoa huduma salama na zinazoaminika, na kuvutia ushirikiano wa kitaalamu na uwekezaji katika sekta ya afya.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutoa huduma za damu salama nchini, Mpango wa taifa wa damu salama ulifanyiwa tathmini ya kipimo cha uhakiki ubora kwa mujibu wa kiwango cha kimataifa cha ISO 17043. Kupitia tathmini hiyo, Mpango wa taifa wa damu salama umefanikiwa kupata ithibati na cheti kutoka South Africa National Accreditation System – SANAS hatua inayothibitisha ubora na uaminifu wa huduma za maabara nchini. Hatua hizo zinaendelea kuimarisha mifumo ya ubora na usalama wa huduma za damu na hivyo

kuongeza imani ya wananchi na wadau katika huduma hizo muhimu.

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama umefanikiwa kutengeneza mazao ya damu chupa 627 na kusambaza katika hospitali zinazotumia mazao hayo kama hospitali ya taifa, hospitali maalum na hospitali za kanda ikilinganishwa na chupa 614 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imefanikiwa kuandaa sampuli za kuhakiki ubora wa upimaji wa makundi ya damu na kusambaza katika hospitali 302 ili kuhakiki ubora wa huduma za damu zinazotolewa.

***"Damu haiwezi kutengenezwa, inapatikana tu kutoka kwa watu wenye moyo wa ukarimu. Huhitaji kuwa daktari ili kuokoa maisha bali hata kwa kuwa mchangiaji tu wa damu. Niwasihi wananchi wenzangu kujitokeza kwa wingi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wengi".***

## Maabara Kuu ya Taifa ya Afya ya Jamii

**227. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Maabara imefanikiwa kupima jumla ya sampuli 80,111 za magonjwa mbalimbali ya milipuko. Sampuli hizo zinahusisha uchunguzi wa magonjwa yakiwemo Mpox, murburg, mafua makali ya influenza, kipindupindu, surua, rubella, kimeta, dengue, kichaa cha mbwa, matende, rotavirus, Human Papilloma Virus, wingi wa virusi vya UKIMWI, na utambuzi wa maambukizi ya VVU kwa watoto wachanga. Maabara hii inaendelea kuwa kituo cha taifa cha ufuatiliaji wa magonjwa pamoja na kuendelea kuwa kituo cha umahiri cha ufundishaji wa usalama, upimaji na udhibiti wa vimelea hatarishi vya magonjwa yanayoweza kusababisha mlipuko na majanga.

## Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA)

**228. *Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ni taasisi iliyopo chini ya Wizara ya Afya,

iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Sura 177 yenye majukumu makuu ya kufanya uchunguzi wa Kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo, utoaji ushahidi wa kitaalam mahakamani na usimamizi na udhibiti wa kemikali za viwandani na majumbani.

***229. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kufanya uchunguzi wa kisayansi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo nchini, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu iliendelea kutoa huduma ya uchunguzi wa kimaabara wa sampuli mbalimbali na vielelezo ambapo jumla ya sampuli 152,130 zilipokelewa. Kati ya sampuli hizo, sampuli 142,085 zilifanyiwa uchunguzi sawa na asilimia 73 ya lengo la kuchunguza sampuli 194,310. Mwelekeo wa sampuli zilizochunguzwa umeongezeka kutoka 132,737 hadi kufikia sampuli 142,085 sawa na ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Uchunguzi huo umeisaidia

Serikali na mamlaka nyingine kufanya maamuzi stahiki katika kulinda afya za wananchi na mazingira pamoja na utoaji wa haki kwa wananchi na katika vyombo vya maamuzi.

***230. Mheshimiwa Spika***, maabara tano (5) za mamlaka zenye ithibati ya kimataifa ambazo ni maabara ya mazingira, chakula, maikrobaiolojia, vinasaba vya binadamu na sayansi jinai, zilifanyiwa ukaguzi wa umahiri wa uchunguzi wa kimaabara kwa mujibu wa matakwa ya ithibati (ISO 17025:2017) kutoka taasisi ya ithibati ya Southern African Development Community Accreditation Services (SADCAS) na kuendelea kushikilia hadhi hiyo. Aidha, ukaguzi wa umahiri wa uchunguzi kwa mara ya kwanza kwa Maabara ya Sayansi Jinai Kemia ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kimataifa (ISO 17025:2017) na kufanikiwa kupendekezwa kupewa ithibati ya kimataifa. Hii ina maana kuwa maabara hizi zina uwezo wa kutoa matokeo sahihi, ya kuaminika na yanayotambulika kimataifa. Ithibati hii ni

muhimu katika kulinda afya ya wananchi kupitia uchunguzi sahihi wa chakula, mazingira na vinasaba, pamoja na kuimarisha ushahidi wa kisayansi katika masuala ya kisheria (forensic). Aidha, huongeza uaminifu wa nchi katika biashara na usafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, kwani matokeo ya maabara yanatambulika kimataifa bila kuhitaji uthibitisho wa ziada.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchangia utoaji wa haki katika vyombo vya maamuzi Mamlaka ilitoa ushahidi wa kitaalam mahakamani kwa mashauri 621 sawa na asilimia 80 ya mashauri 778 yaliyopokelewa. Aidha, kulikuwa na kupungua kwa asilimia 23 ikilinganishwa na mashauri 811 yaliyotolewa ushahidi mahakamani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Mamlaka ilisajili wadau 1,301 wanaojishughulisha na biashara ya kemikali sawa na asilimia 52 ya lengo la kusajili wadau 2,496 kwa mwaka. Lengo la kusajili wadau hao ni kuendelea na juhudi za kulinda

afya, mazingira na usalama wa nchi dhidi ya kemikali hatarishi na bashirifu zinazotumika kutengeneza dawa za kulevya au silaha za kemikali. Pia, Mamlaka ilitoa mafunzo kuhusu usafirishaji salama wa kemikali nchini kwa wadau wa kemikali 1,914. Mafunzo hayo yamesaidia kuwapa uelewa wa namna bora ya kujilinda, kulinda afya ya watu wengine pamoja na kulinda mazingira wakati wa usafirishaji wa kemikali hizo. Aidha, Mamlaka ilitoa jumla ya vibali 68,885 sawa na asilimia 76 ya lengo la kutoa vibali 90,700 kwa mwaka. Vilevile, jumla ya maghala 2,804 ya kuhifadhi kemikali yalikaguliwa, sawa na asilimia 78 ya maghala 3,585 yaliyopangwa kukaguliwa kwa mwaka.

***233. Mheshimiwa Spika,*** Katika kuhakikisha Mamlaka inakuwa na vifaa vya kutosha kulingana na mahitaji na teknolojia ya kisasa, Serikali imeiwezesha Mamlaka kununua na kusimika mtambo wa *Seq Studio Genetic Analyser na fire suppression system* na kuanza kufanya kazi katika maabara ya

vinasaba vya binadamu Dodoma, mtambo wa *Real Time PCR* katika maabara ya vinasaba vya binadamu Dar es Salaam na mitambo midogo 85 katika ofisi ya makao makuu na ofisi za kanda. Mitambo hiyo ya maabara imewezesha matokeo ya uchunguzi wa kimaabara kutoka kwa wakati baada ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

### Huduma za Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi

***234. Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kutoa kipaumbele katika upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya zenye ubora, ufanisi na zilizo salama kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara kupitia Bohari ya Dawa (MSD) imeendelea kununua, kutunza na kusambaza aina mbalimbali za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Katika kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya, Serikali imeendelea kutoa fedha za ruzuku kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya ununuzi wa

bidhaa za afya kupitia MSD, ambapo jumla ya Shilingi bilioni 275 zimetolewa.

### Hali ya Upatikanaji wa Dawa na Bidhaa Muhimu za Afya

**_235. Mheshimiwa Spika_**, Wizara imeimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi ambapo upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele aina 382, umeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 88.8 katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na wastani wa asilimia 86.2 kwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Hali ya upatikanaji wa dawa kwenye zahanati ni asilimia 79.5, vituo vya afya asilimia 82.8, hospitali za halmashauri asilimia 83.8, hospitali za rufaa za mikoa asilimia 95.9 na hospitali za kanda, maalum na taifa asilimia 97.7. Aidha, upatikanaji wa dawa muhimu za kipaumbele 382 katika Bohari ya Dawa umeimarika kutoka wastani wa asilimia 68 mwaka 2025 hadi kufikia asilimia 73 mwezi Machi 2026.

**236. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia MSD huagiza zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa za afya kutoka nje ya nchi wakati chini ya asilimia 20 ya bidhaa za afya huzalishwa na viwanda vya ndani. Hali hii inaonesha umuhimu wa kuchukua hatua za kimkakati ili kupunguza utegemezi wa bidhaa za afya kutoka nje, kuimarisha usalama wa afya wa Taifa, kuongeza uzalishaji wa ndani, kukuza ajira na kujenga uwezo wa nchi kujibu dharura za kiafya bila kutegemea masoko ya nje. Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara imeanzisha kikosi kazi maalum kiitwacho Pharmaceutical Investment Acceleration Taskforce (PIAT) chenye jukumu la kuratibu, kuwezesha na kuharakisha uwekezaji katika uzalishaji wa dawa, vifaa tiba na bidhaa nyingine za afya nchini. Kupitia kikosi kazi hicho, Wizara imefanya mikutano maalum minne (4) na wadau wa uwekezaji wa ndani na nje ya nchi, ambapo wawekezaji 64 wameonesha nia ya kuwekeza nchini.

**237. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuwezesha uwekezaji huo, Serikali imetenga eneo lenye

jumla ya ekari 400 lililopo Mloganzila kwa ajili ya uendelezaji wa Kongani Maalum ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba, yaani Mloganzila Pharmaceutical and Medical Devices Special Economic Zone. Aidha, tarehe 8 Mei, Serikali ilianza rasmi hatua za uendelezaji wa eneo hili maalum, ikiwa ni alama muhimu ya mageuzi ya sekta ya afya kutoka katika utegemezi wa kuagiza bidhaa kutoka nje, kuelekea uzalishaji wa ndani, uhamishaji wa teknolojia, utafiti, ubunifu na biashara ya bidhaa za afya ndani na nje ya nchi. Kongani hii itakuwa kitovu cha uzalishaji wa dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine muhimu za afya, na hivyo kuiweka Tanzania katika nafasi bora ya kuwa kituo cha kikanda cha uzalishaji na usambazaji wa bidhaa za afya.

**238.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali pia katika Bajeti hii imetenga fedha kwa ajili ya kujenga maabara yenye hadhi ya Bio-Equivalent Laboratory. Maabara hii ni muhimu sana kwa kuwa itawezesha kufanya tathmini za kisayansi za ubora, usalama na

ufanisi wa dawa zinazozalishwa nchini pamoja na zile zinazoingizwa kutoka nje. Uwepo wa maabara hii utaimarisha uwezo wa nchi kuthibitisha kuwa dawa zinazozalishwa ndani zinafanya kazi kwa kiwango sawa na dawa rejea, hivyo kuongeza imani ya wananchi, wataalam, MSD na masoko ya kikanda katika bidhaa zinazozalishwa nchini. Aidha, maabara hii itapunguza utegemezi wa kufanya vipimo nje ya nchi, itapunguza gharama na muda wa usajili wa dawa, na itachochea ukuaji wa viwanda vya ndani kwa kuwawezesha wazalishaji kupata uthibitisho wa ubora ndani ya nchi.

***239. Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha dhamira hii inakwenda sambamba na teknolojia ya kisasa, Serikali imesaini makubaliano na kampuni ya Sartorius kutoka Ujerumani kuwa mbia wa teknolojia katika eneo la biopharmaceuticals. Ushirikiano huu utasaidia kujenga uwezo wa nchi katika uhamishaji wa teknolojia, mafunzo ya wataalam, uanzishaji wa

miundombinu ya uzalishaji wa bidhaa za kibayoteknolojia, pamoja na kushirikiana na Serikali katika kuendeleza uzalishaji wa chanjo muhimu. Hatua hii ni ya kimkakati kwa sababu chanjo, dawa na bidhaa za kibayoteknolojia si bidhaa za kawaida; ni sehemu ya usalama wa afya, usalama wa Taifa na uwezo wa nchi kujilinda dhidi ya magonjwa ya mlipuko na majanga ya kiafya.

**240.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, hatua hizi zinaonesha kuwa Serikali haijengi viwanda vya dawa kwa mtazamo wa kibiashara pekee, bali inajenga msingi wa uhuru wa kiafya wa Taifa. Kupitia PIAT, Kongani Maalum ya Mloganzila, maabara ya Bio-Equivalent, na ushirikiano wa kimkakati na wabia wa teknolojia kama Sartorius, Tanzania inaweka misingi ya kujitosheleza kwa bidhaa za afya, kukuza uchumi wa viwanda, kuongeza ajira za wataalam, kuvutia uwekezaji na kulinda maisha ya wananchi. Huu ni mwelekeo mpya unaotafsiri kwa vitendo maono ya Serikali ya kujenga Taifa lenye uwezo wa kuzalisha,

kuthibitisha, kusambaza na kutumia bidhaa zake za afya kwa usalama, ubora na uhakika.

**Mapambano ya Usugu wa Vimelea vya Magonjwa dhidi ya Dawa.**

**241.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara imefanya tathmini ya uanzishwaji wa timu za usimamizi na ufuatiliaji wa Usugu wa Vimelea vya Magonjwa Dhidi ya Dawa (UVIDA) katika hospitali nane (8) Tanzania Bara ambapo vituo vinne (4) kati ya hivyo vilipata zaidi ya asilimia 50 ikionesha vinahitaji kuwezeshwa kwa kiasi kidogo ili kuanza kutekeleza afua za UVIDA. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Taifa ya Mapambano Dhidi ya UVIDA inayofanya kazi chini ya mwamvuli wa Afya Moja iliandaa maadhimisho ya Kanda ya Afrika yanayojulikana kama *"Continental World Antimicrobial Resistance Awareness Week"*. Maadhimisho hayo yalifanyika nchini kuanzia tarehe 02 hadi 05 Desemba, 2025 yakiwa yamebeba ujumbe wa *"Act Now, protect our present, Secure our future",* yaani "Chukua

hatua sasa, linda leo yetu, hakikisha kesho yetu". Maadhimisho hayo yalifanyika sambamba na Kongamano la Kisayansi lililolenga kushirikisha wadau mbalimbali katika kujadili utekelezaji wa afua za UVIDA nchini.

**Bohari ya Dawa (MSD)**

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bohari ya Dawa (MSD) ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1993 kwa mujibu wa Sheria ya Bohari ya Dawa Na.13 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2021 ikiwa na majukumu manne (4); uzalishaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa bidhaa za afya kwenda kwenye vituo vya umma na binafsi vilivyoidhinishwa na Wizara. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya vinavyohudumiwa na MSD vimeongezeka na kufika vituo 8,893 kutoka vituo 8,619 mwezi Machi 2025 sawa na ongezeko la vituo 274.

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bohari ya Dawa huagiza zaidi ya asilimia 80 ya bidhaa za afya kutoka nje ya nchi ambapo bidhaa zenye

mikataba, hutumia miezi mitatu (3) tangu uagizaji hadi upokeaji wa shehena na kwa bidhaa zisizo na mikataba hutumia hadi miezi sita (6) au zaidi. Vilevile, kwa baadhi ya bidhaa ambazo huhitaji uzalishaji baada ya kuagiza, huweza kuchukua hadi miezi tisa (9) tangu uagizaji hadi upokeaji wa bidhaa hizi kutoka kwa wazalishaji.

**244. *Mheshimiwa Spika*,** Bohari ya Dawa imeendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kuhakikisha uwepo wa mikataba ya muda mrefu ambapo mpaka sasa tuna mikataba 479 yenye jumla ya bidhaa 1,354 kati ya bidhaa 1,725 zinazopaswa kununuliwa, kutunzwa na kusambazwa na MSD kwa muda wote. Kwa upande wa bidhaa za afya za kipaumbele aina 382, bidhaa 361 sawa na asilimia 94.5 zina mikataba ya kudumu na bidhaa nyingine zilizosalia zipo katika hatua mbalimbali za zabuni. Vilevile, katika kulinda viwanda vya ndani, MSD imenunua bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi bilioni 62.5 ikiwemo maji tiba kutoka kwa wazalishaji wa

ndani ili kuvutia wawekezaji na kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya.

**_245. Mheshimiwa Spika,_** hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za kipaumbele 382 kwenye maghala ya MSD umefikia asilimia 71 kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya mwezi mmoja na zaidi ikilinganishwa na asilimia 65 iliyorekodiwa mwezi Desemba, 2025. Aidha, upatikanaji wa bidhaa za dawa pekee umefika asilimia 72 ikilinganishwa na asilimia 64 iliyorekodiwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 kwa kiwango kinachokidhi mwezi mmoja na zaidi. Vilevile, hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya za Miradi Msonge umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 81 mwaka 2024/2025 hadi kufikia asilimia 87 Machi, 2026. Pia, hali ya utimizaji wa mahitaji ya vituo vya kutolea huduma za afya umeendelea kuimarika na kufikia asilimia 83.

**_246. Mheshimiwa Spika,_** Bohari ya Dawa imeendelea kufanya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba vinavyohitajika katika vituo vya kutolea huduma za afya kuanzia ngazi ya

msingi hadi vituo vinavyotoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi nchini. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine za kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo, mashine za mionzi kwa ajili ya kinywa na meno, mashine za usingizi, *ultrasound*, *Digital X-Ray*, majokofu ya kuhifadhia miili na jenereta vyenye thamani ya Shilingi bilioni 116.4.

**247. *Mheshimiwa Spika*,** Bohari ya Dawa inamiliki maghala yenye mita za mraba 48,254 sawa na asilimia 48 ya mahitaji yake ya miundombinu baada ya kukamilisha ujenzi wa maghala ya kisasa katika kanda ya Dodoma na Mtwara yenye jumla ya mita ya mraba 12,000 yaliyogharimu kiasi cha Shilingi bilioni 42. Katika kukabiliana na changamoto ya uhaba wa maghala, Bohari ya Dawa imekodi mita za mraba 20,605 kutoka taasisi binafsi, hivyo kufikisha jumla ya mita za mraba 68,859 sawa na asilimia 68.9 ya mahitaji kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa za afya. Pamoja na jitihada za kukodi kutoka Sekta binafsi, bado maghala hayo hayakidhi viwango vya uhifadhi kwa

kuzingatia nafasi na uhifadhi salama wa bidhaa husika hivyo kuhatarisha ubora na usalama wa bidhaa husika. Aidha, mahitaji halisi ya kutosheleza utunzaji wa bidhaa za afya ni mita za mraba 100,000 zinazoendana na kasi ya uwekezaji wa Serikali katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na ongezeko la idadi ya watu nchini. Kwa sasa Bohari ya Dawa inaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ghala katika Mkoa wa Geita – Chato uliofikia asilimia 40 ya utekelezaji na hadi kukamilika kwake utagharimu kiasi cha Shilingi bilioni 19.

***248. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, uhakiki mali umefanyika kwa Kanda zote na bidhaa za afya zipo sawa kama ilivyo kwenye mfumo wa ERP epicor10. Kiasi cha bidhaa za afya za kundi la kawaida ilikuwa na thamani ya Shilingi bilioni 235.7, bidhaa za miradi msonge Shilingi bilioni 313.1, na bidhaa maalum Shillingi bilioni 13.1. Kwa Bohari ya Dawa kuwa na bidhaa za thamani hii kunatoa uhakika wa usalama wa afya katika

kipindi cha kawaida na pale ambapo majanga yakitokea.

***249. Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Bohari ya Dawa imeendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kutekeleza mpango wa usambazaji wa mizunguko sita kwa mwaka, ambapo vituo hupatiwa bidhaa kila baada ya miezi miwili, tofauti na mfumo wa awali wa mizunguko minne kwa mwaka. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Bohari ya Dawa imefanikiwa kusambaza bidhaa za afya zenye thamani ya Shilingi bilioni 317 nchi nzima. Aidha, utekelezaji wa usambazaji huo ulifanyika kwa kuzingatia muda uliopangwa kwa wastani wa asilimia 98, hatua iliyochangia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya wakati wote. Katika kipindi hiki, Taasisi imefanya usambazaji wa vifaa tiba katika maeneo yote muhimu ikiwa ni pamoja na vifaa vya huduma za mama na mtoto, mashine za kuchuja damu na huduma za kinywa na meno.

**250. *Mheshimiwa Spika*,** katika kuboresha afya ya mama na mtoto Bohari ya Dawa ilipokea mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.9 kupitia mradi wa *Safer Birth Bundle of Care (SBBC) PLUS* kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa bidhaa za uzazi salama kwa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya. Hadi kufikia Machi 2026, bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 2.5 zilikuwa tayari zimesambazwa sawa na utekelezaji wa asilimia 83.1. Kwa vituo vilivyo chini ya OWM-TAMISEMI, Bohari ya Dawa ilipokea mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 10.3 ambapo bidhaa zenye thamani ya Shilingi bilioni 7.9 sawa na asilimia 77 zilikuwa tayari zimenunuliwa na kusambazwa. Aidha, hadi kufikia Machi 2026, kwa upande wa huduma za dharura kwa akinamama na watoto wachanga (CEmONC) vifaa tiba vyenye thamani ya Shilingi bilioni 27.1 kati ya mahitaji yenye thamani ya Shilingi bilioni 27.9 sawa na asilimia 97.3 vimesambazwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bohari ya Dawa imeendelea kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa ajili ya huduma ya kuchuja damu kwa wagonjwa wa figo zinakuwepo kwa gharama nafuu ambapo kwa sasa gharama ya mzunguko mmoja imepungua kutoka shilingi 250,000.00 hadi 150,000.00. Kwa kipindi hiki Bohari ya Dawa imesambaza jumla ya mashine 145 za kuchuja damu katika hospitali 16, ambapo hospitali 13 kati ya hizo tayari zinaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa. Aidha, kwa sasa Bohari ya Dawa ina mashine 19 za kuchuja damu, viti 22 vya kuchuja damu na mashine 21 za kuchanganya dawa kiautomatiki zilizopo kwenye maghala.

**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA)**

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilianzishwa kupitia Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219 ikiwa na jukumu kuu la kulinda afya ya jamii kwa kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa

dawa, vifaa tiba, vitendanishi na bidhaa nyingine.

**253.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa dawa na vipukusi, kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipokea jumla ya maombi 917 ya usajili wa dawa za binadamu, ambapo maombi 826 sawa na asilimia 90 yalifanyiwa tathmini. Aidha, maombi 643 sawa na asilimia 78 ya maombi yaliyofanyiwa tathmini yaliidhinishwa na kusajiliwa. Vilevile, maombi 179 ya usajili wa dawa za mifugo yalipokelewa, ambapo maombi 169 sawa na asilimia 94 yalifanyiwa tathmini kati ya hayo maombi 67 sawa na asilimia 40 yalikidhi vigezo na kusajiliwa.

**254.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilipokea maombi 605 ya usajili wa maeneo ya biashara zinazohusiana na dawa na vipukusi ambapo maombi 463 sawa na asilimia 77 yalifanyiwa tathmini na maombi 453 kati ya hayo sawa na asilimia 98 yalikidhi

vigezo vya usajili na hivyo kupewa vibali vya biashara. Aidha, Mamlaka ilifanya ukaguzi wa viwanda 80 (76 vya nje ya nchi na vinne (4) vya ndani ya nchi) na matokeo ni kwamba, viwanda 41 vya nje ya nchi na vitatu vya ndani ya nchi vilikidhi vigezo na kiwanda kimoja (1) cha ndani ya nchi na viwanda 35 vya nje ya nchi havikukidhi vigezo kutokana na mapungufu mbalimbali. Vilevile, maeneo 8,058 ya biashara ya dawa na vipukusi yalikaguliwa ambapo maeneo 7,066 sawa na asilimia 88 yalikidhi vigezo.

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ilipokea jumla maombi ya vibali 3,441 vya dawa, vipukusi na malighafi za bidhaa hizo vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi ambapo maombi 3,334 ni ya kuingiza nchini na 107 ni ya kusafirisha nje ya nchi. Kati ya vibali vilivyoombwa, vibali 3,281 vilitolewa kati ya hivyo 3,186 ni vya kuingiza bidhaa nchini na 95 ni vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Kati ya vibali 3,281 vilivyotolewa, vibali 2,519 vilikaguliwa katika vituo vya forodha ambapo vibali 2,487 ni vya kuingiza bidhaa

nchini na 32 ni vya kusafirisha bidhaa nje ya nchi. Vilevile, jumla ya tani 257.7 za dawa zenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 15.2 ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

***256. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha usalama, ubora na ufanisi wa vifaa tiba na vitendanishi, Mamlaka imepokea jumla ya maombi 531 ya usajili wa vifaa tiba na vitendanishi (Vifaa tiba 347 na vitendanishi 184), kati ya hayo maombi 488 (Vifaa tiba 314 na vitendanishi 174) sawa na asilimia 92 yalifanyiwa tathmini na maombi 217 (vifaa tiba 135 na vitendanishi 82) yaliidhinishwa. Aidha, maombi 489 ya usajili wa maeneo ya biashara ya vifaa tiba na vitendanishi yalifanyiwa tathmini na maeneo 465 sawa na asilimia 95 yalikidhi vigezo na kusajiliwa.

***257. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mamlaka ilikagua viwanda 41 (34 vya nje ya nchi na saba (7) vya ndani ya nchi) na maeneo 901

yanayojihusisha na biashara za vifaa tiba na vitendanishi ambapo maeneo 886 sawa na asilimia 98 na viwanda saba (7) vya ndani ya nchi vilikidhi vigezo. Pia, viwanda vya nje vitano (5) vilikidhi vigezo na viwanda vya nje 29 havikukidhi vigezo kutokana na upungufu mbalimbali.

**_258. Mheshimiwa Spika,_** katika kipindi hicho, Mamlaka ilipokea maombi 5,166 ya vibali vya kuingiza nchini na kusafirisha nje ya nchi vifaa tiba, vitendanishi na malighafi za vifaa tiba, ambapo vibali 4,762 vilitolewa. Aidha, jumla ya tani 180 za vifaa tiba na vitendanishi zenye thamani ya takribani Shilingi bilioni 15 ziliteketezwa kutokana na kutokidhi vigezo vya ubora na usalama na hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu. Vilevile, jumla ya sampuli 415 za bidhaa za dawa, vifaa tiba, vitendanishi na vipukusi vilichunguzwa na vilikidhi vigezo. Hii inaashiria uwepo wa ubora na usalama wa bidhaa ambazo zimedhibitiwa na Mamlaka katika soko.

## Huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto

259. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi, Mama, Mtoto na vijana ambapo katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wanawake 4,626,300 sawa na asilimia 40 ya walengwa walipatiwa huduma za kisasa za uzazi wa mpango, kati yao 856,488 walipatiwa huduma hiyo baada ya kujifungua. Vilevile, watoa huduma 219 kutoka mikoa 11 ya Lindi, Ruvuma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Shinyanga, Geita, Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam walipata mafunzo ya uzazi wa mpango. Aidha, jumla ya vituo 53 vya kutolea huduma za afya vimeboreshwa kufanya upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni na kufikia idadi ya vituo 630 ikilinganishwa na 577 katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025.

260. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya kinamama wajawazito 2,218,640 walihudhuria kliniki na kupatiwa huduma za afya wakati wa ujauzito

na kati yao asilimia 73.3 walihudhuria angalau mara nne. Aidha, kinamama 1,892,998 walijifungua na kati yao asilimia 98 walijifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya na waliojifungua kwa njia ya upasuaji ni asilimia 11. Kutokana na matokeo ya tafiti mbalimbali duniani asilimia 60 ya vifo vitokanavyo na uzazi hutokea baada ya kujifungua. Katika jitihada za kupunguza vifo hivyo, jumla ya kinamama 1,758,507 sawa na asilimia 93 ya walengwa na watoto wachanga 1,764,093 sawa na asilimia 93 ya walengwa, walipata huduma ndani ya saa 24 baada ya kujifungua. Aidha, jumla ya vizazi hai 1,917,647 vilitolewa taarifa kutoka vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Takwimu zinaonesha kuwa watoto wachanga 112,336 sawa asilimia 5.9 walizaliwa na uzito pungufu. Aidha, asilimia 94.8 ya watoto hawa walianza kunyonyeshwa ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa.

***261. Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani, vifo vya watoto

wachanga vinaweza kupungua kwa zaidi ya asilimia 50 ikiwa kila halmashauri itaanzisha wodi maalumu kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu (Neonatal Care Unit - NCU). Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya NCU 76 zimeanzishwa na kufikia 438 ikilinganishwa na 362 kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa NCU kubwa na ya kisasa katika hospitali ya Wilaya ya Kwimba na imeanza ujenzi wa NCU nyingine kubwa za kisasa 35 (15 ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa na 20 hospitali za wilaya). Aidha, vifaa mbalimbali kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu vimenunuliwa na kusambazwa; vikiwemo CPAP 1,350, *Phototherapy* mashine 182, *Radiant warmer* 495 na mashine ya kuzalisha oksijeni 252.

**262.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imenunua na kusambaza bidhaa za afya ya uzazi kwenye vituo vya kutolea huduma za

afya, bidhaa hizo ni; depo provera dozi 1,766,340 sawa na asilimia 85 ya lengo, vidonge vya uzazi wa mpango 1,643,623 sawa na asilimia 84 ya lengo, vipandikizi aina ya implanon NXT 358,084 sawa na asilimia 79 ya lengo, vitanzi aina ya copper T 123,377 sawa na asilimia 83 ya lengo. Aidha, bidhaa nyingine ni; dawa ya sindano ya oxytocin ya kuzuia kupotea kwa damu baada ya kujifungua chupa 3,148,130 sawa na asilimia 97 ya lengo, sindano ya magnesium sulphate ya kuzuia na kutibu kifafa cha mimba chupa 234,170 sawa na asilimia 94 ya lengo, vidonge vya misoprostol 340,083 sawa na asilimia 93 ya lengo. Vilevile, dawa za watoto; vidonge myeyuko vya amoxycilin 41,039,930 kwa matibabu ya homa ya mapafu (nimonia) sawa na asilimia 96 ya lengo, pakiti za ORS na zinki zilizofungashwa pamoja 650,690 kwa matibabu ya kuharisha sawa na asilimia 87 ya lengo.

***263. Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma rafiki ya uzazi kwa vijana, vituo 69 vya kutoa huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa

vijana vimeongezeka na kufikia 1,630 ikilinganishwa 1,561 vilivyokuwepo kipindi kama hiki 2024/2025. Lengo ni kupunguza mimba katika umri mdogo, maambukizi ya VVU na kuimarisha huduma za masuala ya jinsia. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya vituo jumuishi 15 vya kutoa huduma kwa waathirika wa matukio ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto vimeongezeka na kufikia vituo 46. Vilevile, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya waathirika 137,146 walipatiwa huduma na kati yao asilimia 13 walikuwa wamefanyiwa ukatili wa kingono, asilimia 35 walikuwa wamefanyiwa ukatili wa kimwili na asilimia 27 ya waathirika walikuwa ni watoto.

**264.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, vituo vya uchunguzi wa matiti vimeongezeka kufikia 1,700 kutoka 1,375 sawa na asilimia 23. Aidha, jumla ya wanawake 2,443,392 walifanyiwa uchunguzi wa matiti na kati yao asilimia 0.3 walibainika kuwa na dalili za awali za saratani ya matiti na kupewa rufaa

kwa ajili ya matibabu zaidi. Vilevile, jumla ya wanawake 501,615 walifanyiwa uchunguzi wa awali wa saratani ya mlango wa kizazi na kati yao asilimia 2.5 walihisiwa kuwa na saratani ya mlango wa kizazi, asilimia 1.1 walikuwa na mabadiliko ya awali ya saratani ya mlango wa kizazi na walipatiwa matibabu. Katika kuimarisha huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani ya mlango wa kizazi, Wizara imenunua na kusambaza mashine tiba joto 392 za kutibu mabadiliko ya saratani ya mlango wa kizazi.

***265. Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kuimarisha huduma za afya ya uzazi mama na mtoto nchini, kikao cha Marais wa Umoja wa Afrika kilichofanyika mwezi Februari 2026, kilimpa heshima na kumtambua **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kama kinara wa kuongoza juhudi za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto barani Afrika.

## Rasilimali Watu katika Sekta ya Afya

***266. Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya, kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 5,000 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na kufanya jumla ya watumishi katika sekta ya afya kufikia 182,430. Kati ya watumishi hao, 142,794 sawa na asilimia 78 wapo katika ngazi ya afya ya msingi na 34,047 sawa na asilimia 19 wanafanya kazi katika ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum na taifa. Watumishi 5,589 wapo kwenye mashirika, vyuo vya mafunzo, wakala na idara zilizopo chini ya Wizara ya Afya sawa na asilimia 3.0. Vilevile, jumla ya wataalam 9,039 waliajiriwa kwa utaratibu wa ajira za mikataba ya muda mfupi kwa kutumia mapato ya ndani. Kati yao, watumishi 3,717 wameajiriwa kwenye hospitali za rufaa za mikoa, kanda, maalum

na hospitali ya taifa Muhimbili na watumishi 5,322 wameajiriwa ngazi ya afya ya msingi.

**267.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara imeendelea kusimamia uendeshaji wa mafunzo katika vyuo vya afya vya umma, binafsi na vinavyomilikiwa na taasisi za dini ili kuhakikisha vinazalisha wataalam mahiri na wenye weledi. Kwa mwaka wa masomo 2025/2026, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi lilifanya uchaguzi wa wanafunzi 39,698 sawa na asilimia 88.7 ya waombaji 44,760 waliotuma maombi ya kujiunga na programu mbalimbali za kada za kati za afya. Kati ya waliochaguliwa, wanafunzi 5,057 sawa na asilimia 12.7 walipangiwa vyuo vya Serikali, na wanafunzi 34,641 sawa na asilimia 87.3 walipangiwa vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi na taasisi za dini.

**268.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iliratibu mitihani ya kitaifa ya muhula wa pili kwa kada za kati za afya na jumla ya wanafunzi

85,959 kutoka vyuo vyenye programu za mafunzo ya afya ngazi ya kati walishiriki kwenye mitihani hiyo. Kati yao, wanafunzi 42,511 sawa na asilimia 49.5 walifaulu mitihani ambapo kati ya waliofaulu, wanafunzi 14,401 walikuwa wa programu za Stashahada (NTA Level 6) wakiwa ni asilimia 89.6 ya wanafunzi wote wa ngazi hiyo. Aidha, katika kuimarisha uwezo wa wakufunzi wa vyuo vya afya katika mbinu za ufundishaji na upimaji wa wanafunzi, Wizara iliratibu na kufanikisha mafunzo mahsusi kwa wakufunzi 33 kutoka vyuo vya mafunzo ya kada za kati. Vilevile, ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa mafunzo katika vyuo vya afya vya umma, Wizara iliratibu uendeshashaji wa mafunzo ya uongozi na usimamizi ambayo yalihusisha washiriki 60 wakiwemo wakuu wa vyuo na makamu wakuu wa vyuo vya afya.

**269.** ***Mheshimiwa Spika*****,** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara kupitia ufadhili wa masomo wa *Samia Health Super-Specialization Program* umewezesha ufadhili

wa masomo kwa wataalam wapya wa Sekta ya Afya 498 na kufanya jumla ya wataalam wanaofadhiliwa kusomea fani mbalimbali za ubingwa na ubingwa bobezi ndani na nje ya nchi kufikia 1,483. Kati ya wataalam wapya waliopata ufadhili, 442 wamepata ufadhili wa kusoma vyuo vikuu vya ndani na watalaamu 56 wamepata ufadhili wa kusoma nje ya nchi. Aidha, hospitali na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya zimeweza kutoa ufadhili wa masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi kwa jumla ya watumishi 132 kwa kutumia mapato yao ya ndani.

**270.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Wizara kupitia Mabaraza ya Kitaaluma imeendelea kuhakikisha mafunzo endelevu kwa watumishi wa Sekta ya Afya yanatolewa kwa wataalam wanaofanya kazi katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Jumla ya watumishi 84,351 walifanikiwa kukamilisha mafunzo na kutunukiwa vyeti. Haya ni matokeo chanya kutokana na Wizara kuendelea kuimarisha na kusisitiza matumizi

ya mfumo maalum wa mafunzo kwa njia ya kielektroniki unaojulikana kama *National e-Learning Platform for Health*. Aidha, katika kipindi hiki watumiaji wapya waliosajiliwa kwenye mfumo ni 12,088 hivyo kufanya jumla ya watumishi waliosajiliwa hadi sasa kufikia 143,156.

***"Hakuna mfumo wa afya unaoweza kufanya kazi bila wataalam waliopata mafunzo, wenye motisha na wanaopata stahiki zao ipasavyo".*** **Tedros Adhanom Ghebreyesus, Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO).**

**Matumizi ya TEHAMA**

***271. Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza agizo la **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** la kuhakikisha mifumo ya kielektroniki iliyopo katika Sekta ya Afya inakuwa michache na inayosomana, Wizara inaendelea na maboresho ya mifumo ya TEHAMA na kuiunganisha na mifumo mingine ya Serikali. Hatua hiyo ni nguzo muhimu kwa ufanisi wa utoaji wa huduma,

hususan wakati huu Wizara inapoendelea kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote. Wizara imeweka eneo hili kuwa kipaumbele cha kimkakati, ambapo mapitio ya mifumo yote iliyopo yanafanyika ili kuwezesha kuwa na mfumo wa kitaifa wa afya unaosomana (end-to-end health care management system) utakaotumika katika ngazi zote. Mfumo huo utawezesha upatikanaji wa takwimu sahihi kwa wakati, kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa gharama za matibabu, kuzuia udanganyifu na mianya ya upotevu wa mapato, kusaidia kuthibitisha kwa ushahidi huduma zilizotolewa, kupanga na kufanya maamuzi ya kimkakati.

***272. Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafanya mapitio ya sera, kanuni na sheria ili kuhakikisha matumizi ya mfumo huu ni ya lazima, dawa zote zitaandikwa kwa njia ya kielektroniki (e-prescription), madai na malipo kufanyika kupitia mfumo huo. Hatua hizi ni muhimu ili kulinda uendelevu wa Bima ya Afya kwa Wote na kuimarisha ubora wa huduma kwa wananchi kwa kuhakikisha

dawa zinazoandikwa zinapatikana ndani ya vituo vya kutolea huduma, kupunguza gharama kwa wagonjwa, kuondoa marudio ya vipimo vilivyofanyika na kuwezesha wataalam kuona taarifa za mgonjwa na mwendelezo wa matibabu yake kutoka kituo kimoja hadi kingine alichohudumiwa.

**273. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa sasa imefanikiwa kutengeneza mfumo wa "Health Data Universal Application Programming Interface (HDU API)" ambao utawezesha kupokea, kutuma, kutunza kutoa rufaa kidigitali na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kwenye mifumo mingine inayohitaji taarifa za wagonjwa kutoka hospitali za umma na binafsi. Mfumo huo utaunganisha mifumo mingine ya Afya eHMS, GOTHOMIS, mfumo wa dharura za Afya (NEMS), mfumo jumuishi wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii (UCS), Mfumo wa Taarifa za Watumishi wa Sekta ya Afya (HRHIS), Mfumo wa Uhasibu na Utoaji wa Taarifa za Fedha ngazi ya Kituo (FFARS), Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE), Mfumo wa taarifa za

usajili wa wataalam wa kada za afya (HPRS), mfumo wa taarifa za chanjo (VIMS), mfumo wa taarifa za utoaji wa huduma za afya (DHIS2) na Mfumo wa taarifa za wanaopata huduma za chanjo (TIMR). Aidha, kufikia Machi, 2026 mfumo wa Afya eHMS unatumika katika hospitali zote 28 za rufaa za mikoa na mfumo wa GOTHOMIS unatumika katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya ngazi ya msingi kwa asilimia 96.

***274. Mheshimiwa Spika,*** uunganishaji huo utawezesha wagonjwa kufungua jalada kwa njia ya mtandao, kupata namba ya malipo ya huduma zote za awali bila kulazimika kufika katika kituo cha kutolea huduma na kuandikiwa cheti cha dawa cha kidigitali baada ya kupata huduma. Kukamilika kwa mfumo huo kutapunguza msongamano, matumizi ya karatasi, muda wa kusubiri huduma na kuongeza ufanisi wa vituo vya kutolea huduma ikiwemo kupunguza mianya ya upotevu wa mapato.

**Ufuatiliaji na Tathmini**

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuandaa na kutoa takwimu mbalimbali za Sekta ya Afya kwa wakati ambazo hutumika kwa ajili ya kuandaa mipango na kufanya maamuzi. Katika kipindi hiki, Wizara imekamilisha taarifa nne (4) muhimu za kitakwimu ambazo ni *Annual Health Statistical Bulletin Second Edition, Annual Health Sector Performance Profile, Health Statistical Table and Figure, National Health Facility Atlas na Health Facility's Annual Mortality Statistics Report.* Taarifa hizi zinapatikana katika tovuti ya Wizara na tovuti ya Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali – NBS.

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imenunua na kusambaza jumla ya kompyuta 2,758 katika mikoa yote 26 nchini kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa takwimu zenye ubora na kwa wakati katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kompyuta hizo zitawezesha vituo vya kutolea huduma za afya kufanya uchambuzi wa takwimu kwa kutumia

mifumo ya kidigitali badala ya matumizi ya sasa ya karatasi, hivyo kupunguza nguvu kubwa na muda mrefu katika uchambuzi.

**277.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza maelekezo ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge, Uratibu na wenye Ulemavu kwa kuimarisha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ndani ya Sekta ya Afya. Katika kuhakikisha taaluma ya ufuatiliaji na tathmini inawafikia wataalam wengi zaidi nchini katika Sekta ya afya, Wizara kwa kushirikiana na chuo cha CEDHA imeandaa mtaala maalum wa muda mfupi wa ufuatiliaji na tathmini katika Sekta ya Afya na kuanzisha mafunzo.

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2026, jumla ya wataalam wa afya 756 wamepata mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kupitia mtaala huo, ikijumuisha baadhi ya waganga wakuu wa mikoa, halmashauri, timu za uendeshaji wa huduma za afya za mikoa na halmashauri na watumishi kutoka katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, Wakurugenzi na wataalam kutoka

katika Taasisi za Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Saratani Ocean Road, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI), Hospitali ya kanda ya ziwa Bugando, Hospitali maalum ya Taifa ya Afya ya Akili - Mirembe pamoja na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT) wamepata mafunzo hayo. Vilevile, hospitali za rufaa za mikoa nane (8) zilifikiwa na mafunzo ambazo ni hospitali ya rufaa ya mkoa ya Ligula, Tumbi, Mwananyamala, Dodoma, Manyara, Maweni, Geita na Hospitali ya Kumbukukumbu ya Mwalimu Nyerere – Mara.

**Ugharamiaji wa Huduma za Afya**

***279. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuwezesha wananchi kupata huduma bora za afya kwa kuzingatia Sera ya Afya ya Mwaka 2007. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini na kuhakikisha mpango wa bima ya afya kwa wote unatekelezwa kwa ufanisi.

**280. *Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha Shilingi trilioni 3.1 kimetengwa kwa ajili ya kugharamia vipaumbele mbalimbali katika Sekta ya Afya ikiwemo ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika ngazi zote, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, stahiki za watumishi na kuendelea kugharamia mafunzo ya wataalam katika ngazi mbalimbali kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi trilioni 2.54 kilichotengwa mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 22.

**281. *Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari zitokanazo na mabadiliko ya sera za kimataifa katika ufadhili wa huduma za afya, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa rasilimali fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia huduma za afya nchini, ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya kugharamia bidhaa za afya imeongezeka hadi kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 398.2 kutoka Shilingi bilioni 200 zilizotengwa

mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 99. Ongezeko hili limewezesha ununuzi na upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya VVU (ARVs) pamoja na dawa nyingine muhimu nchini, ambapo hadi kufikia Machi 2026 kiasi cha Shilingi bilioni 275 sawa na asilimia 69 ya fedha zilizotengwa kimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa dawa hizo.

***282. Mheshimiwa Spika*,** Serikali inaendelea kutekeleza ahadi ya **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** ya kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa Awamu. Awamu ya kwanza ya utekelezaji ilianza rasmi tarehe 26 Januari, 2026 ambayo imehusisha usajili wa kaya 276,004 zisizo na uwezo ikiwa ni pamoja na wazee 235 na watoto 255 wanaoishi katika makazi maalum yanayomilikiwa na Serikali. Wanufaika wote katika awamu hii watagharamiwa na Serikali ambapo tayari kiasi cha Shilingi bilioni 48.8 kimetolewa. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya kaya

172,297 kati ya 276,004 sawa na asilimia 62 zimefikiwa na kufanya idadi ya wanufaika kuwa 463,228 sawa na asilimia 38 ya lengo la kusajili wananchi 1,206,319 ambapo kwa sasa wanufaika wameanza kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, katika zoezi la uhakiki na usajili ilibainika kuwa wananchi 15,747 walipoteza sifa za kugharamiwa bima ya afya na Serikali kutokana na sababu za kuimarika kiuchumi au kufariki na wananchi 192,208 hawakujitokeza wakati zoezi linatekelezwa. Kwa muktadha huo, jumla ya wananchi 671,183 sawa na asilimia 55 wamefikiwa kwa lengo la usajili wa wananchi 1,206,319 na usajili unaendelea ili kufikia wananchi 535,136 waliobaki.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** katika zoezi la usajili wa makundi maalumu, kati ya wazee 235, wazee 141 wamepatiwa kadi za bima ya afya, 16 wamefariki, 33 hawakuwepo katika vituo vya kulelea wazee na 45 taarifa zao zilikosewa. Aidha, kwa upande wa watoto, kati ya watoto 255, watoto 205 wamekutwa

wana kadi za bima ya afya zilizo hai, 49 hawakuwepo katika vituo vya kulelea watoto na mtoto mmoja (1) taarifa yake ilikosewa. Marekebisho ya taarifa zilizokosewa yanaendelea kufanyika ili wahusika waweze kusajiliwa na kupatiwa kadi za bima. Aidha wananchi wote ambao wamesajiliwa na kupatiwa kadi, wanaendelea kupata huduma.

***284. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na OWM- TAMISEMI, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania inaendelea kutoa elimu kwa wananchi na kuhamasisha kuhusu umuhimu wa bima ya afya. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 makundi ya kimkakati yaliyofikiwa ni pamoja na viongozi wa ngazi za Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na wahariri na waandishi wa habari wa vyombo vyote nchini. Dhamira ya Wizara kufikia makundi hayo kwanza ni kujenga uelewa wa pamoja, kuwawezesha kuelewa kwa kina malengo ya Serikali, mwelekeo wa kisera na

dhana ya bima ya afya kwa wote, ili wawe washirika wa maendeleo katika kuifikisha sera hii kwa wananchi. Vilevile, jumla ya vipindi 10 vya televisheni, 108 vya redio za kitaifa, 20 vya redio jamii na makala tano (5) kwenye magazeti matano (5) na mitandao ya kijamii zimetolewa. Aidha, jukumu la kuelimisha wananchi ni endelevu lenye lengo la kufikia wananchi wote ikiwa ni pamoja na kubadilisha fikra, mtazamo na tabia za wananchi ambao wengi wao hawana uelewa mzuri wa dhana ya bima ya afya.

## Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

***285. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ni taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Sura 395 kwa lengo la kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watumishi wa umma na wategemezi wao kupitia bima ya afya. Kufuatia marekebisho ya Sheria ya Bima ya Afya ya mwaka 2009, Mfuko unajumuisha watumishi katika sekta ya

umma, wafanyakazi kutoka katika sekta binafsi na makundi mbalimbali katika sekta zisizo rasmi. Majukumu ya kisheria ya Mfuko ni pamoja na kuandikisha wanachama, kukusanya michango na kuitunza, kusajili watoa huduma na kufanya malipo kwa watoa huduma za afya. Majukumu mengine ni kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma, kufanya tathmini ya uhai wa Mfuko na kutoa elimu kwa umma.

***286. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umesajili wanachama 763,793 sawa na asilimia 68 ya lengo la kusajili wanachama 1,129,929. Asilimia 92 ya wanachama waliosajiliwa ni kutoka sekta binafsi na asilima 8 ni kutoka sekta ya umma. Idadi ya wanachama waliosajiliwa imewezesha Mfuko kuwa na wanachama 1,640,646 wenye jumla ya wanufaika 6,904,539 sawa na asilimia 10.5 ya watanzania wote. Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kuendelea kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha

wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

**287. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko umekusanya mapato jumla ya Shilingi bilioni 697.4 sawa na asilimia 74.3 ya lengo la mwaka. Kati ya fedha zilizokusanywa, kiasi cha Shilingi bilioni 625.6 kimetokana na michango ya wanachama, kiasi cha Shilingi bilioni 66.4 kimetokana na mapato yatokanayo na uwekezaji na kiasi cha Shilingi bilioni 5.4 kimetokana na mapato kutoka vyanzo vingine kama vile maombi ya mikopo, usajili wa vituo na usimamizi wa huduma za ziada.

**288. *Mheshimiwa Spika*,** Mfuko umechakata jumla ya madai 47,502 na jumla ya Shilingi bilioni 399.3 zimelipwa sawa na asilimia 90 ya madai yaliyowasilishwa. Madai hayo yalichakatwa kwa wastani wa siku 51 ikilinganishwa na siku 58 kipindi kama hicho mwaka 2024/2025. Vilevile, asilimia 40 ya malipo yalilipwa kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma vya Serikali na asilimia 60 kwenda vituo vya kutolea huduma vya

binafsi na vituo vinavyomilikiwa na mashirika ya dini. Aidha, Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi, 2026 Mfuko umesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 2,259. Kati ya vituo hivyo, vituo 420 ni usajili wa mara ya kwanza na vituo 1,839 ilikuwa ni kwa sababu nyingine zikiwemo kuhuisha usajili, kubadilishiwa hadhi, kuongeza huduma, kubadilishiwa umiliki pamoja na kubadilisha eneo.

**289.** ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko umeendelea kupambana na kudhibiti udanganyifu kutoka kwa watoa huduma, waajiri binafsi, wanufaika wa huduma na watumishi kwa kutekeleza mikakati mbalimbali. Mikakati hiyo imelenga kudhibiti na kuibua vitendo vya udanganyifu kutoka kwa watoa huduma na wanufaika, kuibua maeneno yenye upungufu katika shughuli za uendeshaji na kuchukua hatua stahiki. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umefanikiwa kufanya chunguzi 115 ambapo

kufuatia chunguzi hizo kiasi cha Shilingi bilioni 2.1 kilibainishwa kwa ajili ya kurejeshwa.

**_290. Mheshimiwa Spika_**, katika kuongeza kiwango cha kuridhishwa na huduma za Mfuko kwa wateja, mikakati mbalimbali ya uimarishaji wa huduma imefanyika ikiwemo Mfuko kuanzisha kituo cha huduma kwa wateja kwa ajili ya kuhakikisha wanachama wanapata msaada wakati wote. Katika kipindi husika, kituo cha huduma kwa wateja kilishughulikia simu 206,351 kati ya 283,536 zilizopigwa sawa na asilimia 73. Aidha, asilimia 97 ya malalamiko yaliyowasilishwa kwa njia ya barua pepe na masanduku ya maoni yalijibiwa na kupatiwa ufumbuzi na kupandisha kiwango cha wateja kuridhika na huduma kufikia asilimia 94.

**_291. Mheshimiwa Spika,_** Mfuko umeendelea kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima ya afya na kuimarisha mahusiano na wadau kwa njia mbalimbali kama vile runinga, redio, mitandao ya kijamii, maonesho,

majukwaa mbalimbali na tovuti ya Mfuko. Aidha, elimu kuhusu Vifurushi vya NHIF, elimu ya Bima ya Afya kwa Wote na mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa/udanganyifu pamoja na matumizi ya Self Service Portal ilitolewa.

**292.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mfuko umeendelea kusisitiza matumizi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake hususan kuwezesha mchakato wa ulipaji madai kwa kutumia mifumo inayojiendesha (inayotumia akili unde - AI); kuboresha mfumo wa usajili wa wanachama kwa kuunganisha pamoja na mifumo ya Serikali kwa ajili ya utambuzi mfano: TASAF; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum; Wizara ya Afya; Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA); kuboresha mfumo wa uandikishaji na kumwezesha mwanachama kujiandikisha na kujihudumia bila kulazimika kufika katika ofisi za Mfuko.

**Utekelezaji wa Majukumu ya Mabaraza na Bodi za Kitaaluma**

***293. Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wa Sekta ya Afya katika vituo vya kutolea huduma nchini. Katika kutekeleza ilo, mabaraza ya kitaaluma na bodi za usajili wa vituo binafsi ziliundwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kusimamia maadili ya kitaaluma, kusajili wataalam na kusimamia ubora wa huduma zinazotolewa na wataalam wa kada mbalimbali za afya.

***294. Mheshimiwa Spika***, Wizara ina jumla ya mabaraza ya kitaaluma nane (8) na bodi za usajili mbili (2), ambazo ni pamoja na; Baraza la Madaktari Tanganyika, Baraza la Afya Mazingira, Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala, Baraza la Uuguzi na Ukunga, Baraza la Famasia, Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria), Baraza la Wataalam wa Radiolojia, Baraza la Wataalam wa Maabara, Bodi ya Maabara Binafsi za Afya na Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi.

**295. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, mabaraza ya kitaaluma yalisajili jumla ya watalaam 14,310, usajili wa maduka ya dawa 330, usajili wa watarajali 3,004, mashauri ya kinidhamu yaliyofanyiwa kazi ni 30, mafunzo endelevu ya kitaaluma (CPD) yametolewa kwa watalaam 102,066 (84,351 kupitia mfumo wa National e-Learning Platform for Health na 17,715 nje ya mfumo), ukaguzi wa vituo binafsi vya kutolea huduma za afya 654 na usajili wa vituo vya kutolea huduma 3,643. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, Bodi na Mabaraza ya Kitaaluma yametekeleza majukumu yake kama ifuatavyo: -

## Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC)

***296. Mheshimiwa Spika***, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania lina mamlaka ya kisheria ya kusimamia taaluma na wanataaluma wa uuguzi na ukunga Tanzania. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya wauguzi na wakunga 4,658 walisajiliwa sawa na asilimia 77.6 ya lengo la kusajili wataalam 6,000 kwa mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na wataalam 4,506 waliosajiliwa katika kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Idadi hiyo inafanya jumla ya wataalam waliosajiliwa na Baraza kufikia 59,257. Aidha, wauguzi na wakunga 741 wamepewa usajili wa awali na wanaendelea na mafunzo ya utarajali katika vituo 37 zikiwemo hospitali ya taifa, hospitali za rufaa za kanda na hospitali za rufaa za mikoa. Aidha, jumla ya wauguzi na wakunga 4,382 waliohitimu mafunzo yao kwa ngazi mbalimbali walifanya mtihani wa usajili na leseni. Idadi hiyo ilijumuisha watahiniwa 673 sawa na asilimia 15 ngazi ya shahada, watahiniwa

3,683 sawa na asilimia 84 ngazi ya stashahada na watahiniwa 26 sawa na asilimia 1 ngazi ya astashahada. Katika kipindi hiki, vyuo viwili (2) vimesajiliwa kuendesha mafunzo ya stashahada ya uuguzi na ukunga. Vilevile, Baraza lilipokea na kuhakiki jumla ya maombi 485 ya wanafunzi waliodahiliwa vyuoni ambao waliomba usajili wa awali.

***297. Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuimarisha uendelezaji wa wataalam ambapo jumla ya moduli 20 za mafunzo ya kujiendeleza zenye maudhui mbalimbali zilipokelewa, kuhakikiwa na kupewa ithibati. Vilevile, jumla ya mashauri 12 ya tuhuma za uvunjifu wa maadili yalipokelewa kutoka Mkoa wa Tabora, Arusha na Dodoma ambapo ufuatiliaji wa awali umefanyika. Kati ya hayo, mashauri 10 yamekamilika na kuwasilishwa kwenye kikao cha 225 cha Baraza na kujadiliwa ambapo wauguzi na wakunga 17 walihusishwa. Aidha, maamuzi kwa tuhuma zilizosikilizwa yalikuwa kama ifuatavyo; wauguzi watano (5) walipewa

onyo, sita (6) walisimamishwa kutoa huduma mwaka mmoja kwa kila mtaaluma, wawili (2) walisimamishwa kutoa huduma miezi sita, watatu (3) walisimamishwa kutoa huduma miezi mitatu (3) na mmoja (1) hakukutwa na hatia.

**Baraza la Madaktari Tanganyika**

***298. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, majukumu ya msingi yaliyoendelea kutekelezwa na Baraza kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ni pamoja na kusimamia usajili, utendaji na maadili ya wataalam na taaluma ya udaktari. Katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 2,252 walisajiliwa ikilinganishwa na wataalam 3,794 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na kufanya jumla ya wataalam wote waliosajiliwa mpaka sasa kufikia 43,405. Aidha, jumla ya wataalam 1,978 wamepatiwa leseni kwa mara ya kwanza na wataalam 5,561 wamehuisha leseni zao na hivyo kufanya jumla ya wataalam

waliopatiwa leseni na kuhuisha leseni kufikia 7,539.

**299. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya maombi ya mtihani wa kabla ya utarajali yaliyopokelewa yalikuwa 1,510 ambapo watahiniwa wa udaktari walikuwa 1,324, udaktari wa meno walikuwa 57, fiziotherapia walikuwa 69 na wataalam wa tiba ya chakula na lishe 60. Aidha, kwa mitihani ya baada ya mafunzo ya utarajali iliyofanyika Desemba, 2025 jumla ya maombi yaliyopokelewa yalikuwa 1,425 kati ya hayo watahiniwa wa udaktari walikuwa 1,290, udaktari wa meno 59, fiziotherapia 41 na wataalam wa tiba ya chakula na lishe 35.

**300. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Baraza lilifuatilia ukiukwaji wa maadili ya kitaaluma ambapo jumla ya malalamiko mapya 14 yalipokelewa. Kati ya hayo malalamiko sita (6) yamechunguzwa na Kamati ya Uchunguzi wa Mashauri ya Kimaadili. Uchunguzi wa awali unaendelea

dhidi ya malalamiko nane (8). Aidha, mashauri 11 yaliyokuwa yamechunguzwa kipindi cha 2024/2025 dhidi ya wataalam waliotuhumiwa kwenda kinyume na maadili ya kitaaluma yalisikilizwa na Baraza. Maamuzi ya mashauri hayo yalihusisha madaktari 11 ni pamoja na madaktari wawili (2) kupewa onyo; watatu (3) kupewa onyo kali; mmoja (1) kufungiwa leseni ya kutoa huduma kwa muda wa miezi sita (6); wawili (2) kufungiwa leseni ya kutoa huduma kwa muda wa mwaka mmoja (1); mmoja (1) kufutiwa leseni ya kutoa huduma na wawili (2) hawakukutwa na hatia hivyo kuachiwa huru.

**301.** ***Mheshimiwa Spika***, Baraza limeendelea kusimamia mafunzo endelevu kwa wanataaluma ambapo kwa kipindi hiki, Baraza limetoa ithibati kwa watoa mafunzo endelevu 79 na kozi za mafunzo endelevu 290. Aidha, Baraza limefanya usimamizi shirikishi kwenye vituo vitano (5) vya kutolea mafunzo endelvu, pia limejengea uwezo hospitali za wilaya na vituo vya afya 25 ili

kuweza kutoa mafunzo endelevu kwa wanataaluma. Vilevile, limefanya uhamasishaji unaohusu mafunzo endelevu, weledi na maadili ya kitaaluma katika mikutano mitatu (3) ya vyama vya kitaaluma ambavyo ni Chama cha Madaktari Bingwa wa Watoto, Chama cha Fiziotherapia Tanzania na Chama cha Viungo Tiba na Vifaa Saidizi Tanzania.

**Baraza la Famasi**

***302. Mheshimiwa Spika,*** Baraza la Famasi lina majukumu ya kusimamia taaluma na wataalam wa dawa, utendaji wake pamoja na usajili na kutoa vibali katika maeneo yanayotoa huduma za dawa na kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi ya dawa. Baraza limesajili jumla ya wafamasia 216, fundi sanifu dawa 1,001 wameandikishwa na fundi sanifu dawa wasaidizi 30 wameorodheshwa na kufikisha jumla ya wanataaluma 15,943 wanaotambuliwa hadi sasa. Kati ya hao, wafamasia ni 4,256; fundi sanifu dawa ni 10,512 na fundi dawa wasaidizi ni 1,175.

**303. *Mheshimiwa Spika*,** Katika kipindi hiki, majengo ya biashara ya famasi 487 yamesajiliwa kutoa huduma ya dawa nchini, hivyo kufanya jumla ya majengo ya biashara ya famasi kuwa 3,718. Vilevile, katika kipindi hiki jumla ya wafamasia 3,159, fundi dawa sanifu 5,305 na fundi dawa wasaidizi 324 wamefanya mafunzo endelevu na moduli 17 za mafunzo hayo zimeidhinishwa.

**Baraza la Wataalam wa Radiolojia**

**304. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Baraza lilipitia maombi ya usajili wa wataalam wa radiolojia kwa kada mbalimbali na kufanya usajili wa awali, usajili wa kudumu, usajili wa muda, uandikishaji na uorodheshaji kwa wataalam waliokidhi vigezo. Katika kipindi hiki, jumla ya wataalam 258 wamesajiliwa, kuorodheshwa na kuandikishwa, hivyo kufikia jumla ya wataalam 2,473 waliosajiliwa hadi sasa. Aidha, jumla ya wataalam 1,554 wamehuisha leseni zao kati

ya wataalam 2,083 wanaotegemewa kuhuisha leseni kwa mwaka 2025/2026 ikiwa ni sawa na asilimia 74.6.

**305.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Baraza limeendelea kusimamia watarajali wa kada za radiolojia nchini ambapo jumla ya watarajali 94 walipewa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili na kupangiwa vituo vya utarajali kwa njia ya mfumo. Aidha, katika kipindi hiki, Baraza lilitoa mafunzo juu ya sheria, kanuni, miiko na maadili kwa wataalam wapatao 450 katika makongamano ya wanataaluma wa radiolojia. Vilevile, Baraza limepokea Shauri moja (1) la uvunjifu wa maadili ya taaluma ambalo limejadiliwa kwenye kikao cha baraza na kwa sasa lipo hatua ya ofisi ya mwanasheria kwa hatua zaidi.

**Baraza la Wataalam wa Macho (Optometria)**

**306.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Baraza lina jukumu la usimamizi na udhibiti wa wataalam wa kada ya optometria, kliniki za optometria,

wasambazaji wa vifaa na miwani na kuhakikisha kliniki zote zinazotoa huduma za optometria zinasajiliwa na kupatiwa leseni. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Baraza limesajili jumla ya wataalam 80 kwa usajili wa kudumu ikilinganishwa na wataalam 40 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kwa usajili wa kudumu kufikia 520. Vilevile, jumla ya wahitimu 40 ngazi ya stahashada ya optometria kutoka vyuo mbalimbali ndani na nje ya nchi wamepewa usajili wa awali na kupangiwa vituo vya mafunzo chini ya usimamizi wa wataalam wazoefu kwa muda wa mwaka mmoja (1), ambapo mara baada ya mafunzo hayo watapewa usajili wa kudumu. Baraza limefanikiwa kusajili kliniki ishirini na mbili (22) zinazotoa huduma za optometria na kuwapangia watarajali wanne (4) kwa ajili ya kupata mafunzo kwa vitendo.

**307. *Mheshimiwa Spika,*** Wataalam wa huduma za optometria takribani 342 wamefanya mafunzo ya kujiendeleza (CPD)

kwa njia tofauti tofauti ikiwemo kwa njia ya mtandao, semina mbalimbali za kujengewa uwezo, na tafiti mbalimbali. Aidha, Baraza lilifanya usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za optometria katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Pwani, Songwe, Iringa, Mbeya na Njombe kwa lengo la kuwajengea uwezo waratibu ngazi ya mikoa (RHMTs) na halmashauri (CHMTs) ili wataalam na wamiliki wa vituo hivyo viweze kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo. Kati ya vituo 116 vilivyokaguliwa, vituo 51 vilibainika kuwa na changamoto mbalimbali na baadhi vilishauriwa namna bora ya kuendesha huduma za optometria, na vingine vilichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ya optometria ya mwaka 2007.

***308. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Baraza lilifanya ukaguzi wa vyuo vitatu (3) vinavyotoa elimu ya optometria ambavyo ni Chuo cha Sayansi Kishiriki Mvumi, Hospitali ya CCBRT na Chuo cha City ndaki ya Mwanza ambapo Taasisi ya

CCBRT inatarajia kuanza kutoa mafunzo ya kada ya optometria ngazi ya stashahada. Aidha, Baraza lilifanya tathmini ya majaribio kwa wataalam wenye usajili wa awali wenye lengo la kutambua uwezo wa wataalam hao katika vituo vyao vya kujifunzia. Katika zoezi hilo jumla ya wataalam 25 ngazi ya stashahada na watarajali watano (5) walitembelewa katika Mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza.

**Baraza la Wataalam wa Maabara**

***309. Mheshimiwa Spika*****,** Baraza lina jukumu la kuhakikisha wataalam wa maabara wamesajiliwa, wameandikishwa, kufuata miiko na maadili ya taaluma ya Maabara pamoja na kusimamia utekelezaji wa mitaala ya mafunzo ya maabara ya afya. Katika kipindi hiki cha Julai 2025 hadi Machi, 2026, Baraza limesajili wataalam 1,987 ikilinganishwa na Wataalam 1,221 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/25. Kati yao, wataalam 787 walisajiliwa kwa usajili wa kudumu, wataalam 75 walipata usajili wa

kuandikishwa na wataalam 1,127 walipata usajili wa awali na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa hadi sasa kufikia 17,390. Wataalam walioweza kuhuisha leseni zao kwa kipindi hiki walikuwa 9,354. Aidha, jumla ya leseni 313 zimetolewa kwa wapimaji wa VVU wasio wataalam wa maabara. Vilevile, katika kipindi hiki mashauri mawili (2) ya kimaadili yalishughulikiwa na hatua za ufuatiliaji wa awali zinaendelea.

***310. Mheshimiwa Spika,*** Baraza liliendesha mitihani ya usajili kwa kada ya maabara ngazi ya astashahada, stashahada na shahada, ambapo jumla ya wataalam 2004 walifanya mitihani na waliopata alama ya ufaulu walikuwa 1,424 sawa na asilimia 71.1. Katika kipindi hiki, Baraza liliendelea kuwasimamia watarajali wa maabara 436 katika vituo 25 vya kutolea mafunzo. Vilevile, Baraza limetoa mafunzo endelevu kwa wataalam wa maabara 7,766 ambao walipata alama.

**311. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi hiki, Baraza lilifanya ukaguzi wa maabara ya hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Njombe, Katavi, Songwe na Kagera kwa ajili ya kupatiwa watarajali wa maabara. Kati ya maabara hizo, maabara ya hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Katavi na Kagera zilifikia vigezo. Vilevile, Baraza limefanya ukaguzi katika chuo cha "Military College of Heath Lugalo" na Chuo cha Teofili Kisanji, University mkoani Mbeya kwa ajili kuanzisha kozi ya maabara. Pia, Baraza liliweza kufanya usimamizi shirikishi katika mikoa tisa (9) ambayo ni Rukwa, Mbeya, Songwe, Iringa, Ruvuma, Njombe, Singida, Dodoma na Arusha. Jumla ya wataalam waliofikiwa katika zoezi hili walikuwa 667 ambapo kati yao, 656 sawa na asilimia 98.8 walikuwa na usajili wa Baraza.

**Baraza la Wataalam wa Afya Mazingira**

**312. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza linasimamia usajili wa wataalam wa afya mazingira ili

kulinda na kusimamia nidhamu na maadili katika taaluma ya afya mazingira. Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi 2026, idadi ya wataalam wapya waliosajiliwa na Baraza la Afya Mazingira ni 730 ikilinganishwa na wataalam 448 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/25 na hivyo kufanya jumla ya wataalam waliosajiliwa kufikia 5,599, kati ya hao, wenye usajili kamili ni 2,159, usajili wa kuorodheshwa ni 2,677, usajili wa kuandikishwa ni 581 na usajili wa muda ni 182. Aidha, Baraza linaendelea na utaratibu wa kusajili wataalam kwa njia ya kielektroniki (hprs.moh.go.tz) ambapo jumla ya wataalam 4,735 wamesajiliwa kupitia mfumo huo.

**313.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Baraza liliendelea kuratibu mafunzo ya utarajali ambapo, jumla ya watarajali 181 wanaendelea na mafunzo katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na vyuo sita (6) vinavyotoa mafunzo ya afya mazingira ngazi ya stashahada ambapo watarajali 144 wamehitimu mafunzo hayo katika kipindi

hiki. Aidha, ufuatiliaji wa usajili, uhuishaji wa leseni na watarajali umefanyika katika mikoa ya Arusha, Manyara, Singida, Ruvuma, Lindi, Kigoma, Njombe, Mbeya, Kilimanjaro, Morogoro na Mwanza na katika vyuo vya afya mazingira vya Mpwapwa na MUHAS. Vilevile, Baraza linaendelea kuhamasisha na kufanya ufuatiliaji kwa wanataaluma wote kujisajili na kuhuisha leseni ili kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria.

**Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala**

***314. Mheshimiwa Spika*,** Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala lilianzishwa kwa lengo la kusimamia, kudhibiti na kuendeleza shughuli za tiba asili na tiba mbadala nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya waganga, wasaidizi wa waganga, wauza dawa wa tiba asili na tiba mbadala wapatao 3,098 wamesajiliwa sawa na asilimia 69 ya lengo la kusajili wataalam 4,500 ikilinganishwa na wataalam 6,713 waliosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025 na kufanya jumla ya wataalam

waliosajiliwa na Baraza kufikia 67,783. Vilevile, Baraza limesajili vituo vya tiba asili sita (6) na kufanya kuwa na jumla ya vituo 154 vinavyotambulika kisheria.

***315. Mheshimiwa Spika,*** Baraza linaendelea na utoaji wa elimu, usajili wa wauza dawa na wamiliki wa maduka ya tiba asili katika Mkoa wa Dar es salaam ambapo hadi kufikia Machi 2026 limesajili wataalam 529 kwa mchanganuo ufuatao: wataalam wa tiba mbadala wawili (2); waganga 147; wasaidizi wa waganga 20; wasaidizi tiba mbadala watatu (3); vilinge vitatu (3); vituo vya masaji vitatu (3); kliniki tiba asili 56; maduka ya dawa 66; wauza dawa 104; na kuhuisha waganga 125.

**Bodi ya Maabara Binafsi za Afya**

***316. Mheshimiwa Spika,*** Bodi hii ina jukumu la kusajili, kusimamia na kuhakikisha kuwa huduma bora za maabara binafsi hapa nchini zinatolewa kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya (zahanati, vituo vya afya,

hospitali pamoja na maabara zote zinazojitegemea). Katika kipindi Julai 2025 hadi Machi, 2026, Bodi ilisajili vituo 287 ikilinganishwa na vituo 317 vilivyosajiliwa kipindi kama hiki mwaka 2024/2025. Kati ya vituo hivyo, vituo 127 vinajitegemea na 160 vipo ndani ya vituo vya kutolea huduma za afya na kufanya jumla ya maabara binafsi nchini kufikia 4,640.

**317.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Katika kipindi hiki, Bodi imefanya ufuatiliaji wa huduma zitolewazo kwenye maabara binafsi za afya 1,117 katika Mikoa 10 ya Kagera, Shinyanga, Simiyu, Morogoro, Dar es Salaam, Singida, Dodoma, Mwanza, Geita na Tabora. Matokeo ya ufuatiliaji yanaonesha maabara zinazingatia vigezo vya mfumo wa udhibiti ubora ambapo uhakiki wa ubora wa ndani wa vipimo (IQC) uliongezeka kutoka asilimia 55 hadi 58 na matengenezo kinga ya mashine yalipanda kutoka asilimia 45 hadi 47.

## Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi

***318. Mheshimiwa Spika***, Bodi ya Ushauri wa Hospitali Binafsi ina jukumu la msingi la kusajili na kusimamia vituo vyote vya kutolea huduma za afya binafsi. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Bodi imesajili jumla ya vituo 3,653. Aidha, kati ya vituo hivyo, vituo vinavyofanya kazi ni 3,422, Vituo vilivyofungwa moja kwa moja ni 98 na vituo 133 vimefungwa kwa muda kutokana na sababu mbalimbali. Pia, kati ya vituo hivyo, hospitali ni 231, vituo vya afya 324, zahanati 2,146, kliniki 278, *polyclinics* 396, kliniki za kusafisha damu 25 na vituo vya uchunguzi ni 22.

***319. Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, jumla ya vituo binafsi 191 vilisajiliwa, kati ya vituo hivyo, 151 vilikuwa vituo vipya, 27 vilikuwa vituo vinavyoomba kubadilishwa daraja na vituo 21 vilikuwa vituo vinavyohuisha usajili. Vilevile, jumla ya vituo 300 viliwasilisha maombi ya usajili, kati ya vituo hivyo, 191 sawa na asilimia 64 vilikidhi vigezo vya kusajiliwa, na vituo 109 sawa na

asilima 36 vilikuwa na mapungufu mbalimbali yaliyohitaji kuboreshwa. Kati ya vituo 191 vilivyosajiliwa, hospitali ngazi ya mkoa tatu (3), hospitali ngazi ya wilaya tisa (9) na hospitali ngazi ya kanda moja (1), vituo vya afya 12, zahanati 103 na kliniki 63.

**320. *Mheshimiwa Spika*,** Bodi kwa kushirikiana na waratibu ngazi za mikoa na wilaya ilifanya ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma za afya binafsi katika mikoa 13 ya Mwanza, Kilimanjaro, Kagera, Kigoma, Songwe, Mbeya, Morogoro, Shinyanga, Njombe, Manyara, Mtwara, Ruvuma na Dar es Salaam, ambapo baadhi ya vituo vilikutwa na mapungufu mbalimbali kama vile, uhaba wa watumishi, miundombinu chakavu na kutozingatia miongozo ya kukinga na kudhibiti maambukizi. Vilevile, baadhi ya vituo havikuwa na usajili na vingine vilikuwa vimeacha kutoa huduma.

**Miradi ya Maendeleo**

321. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususani katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Wizara pamoja na kuendelea na ujenzi lakini pia imefanya ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi 40 ambapo, kati yake, miradi 27 inatekelezwa katika hospitali za rufaa za mikoa, miradi 13 inatekelezwa katika hospitali ya taifa, maalum na kanda. Utekelezaji wa miradi hiyo upo katika hatua mbalimbali mathalani miradi saba (7) imefikia zaidi ya asilimia 90 ikiwemo ujenzi wa jengo la huduma za mionzi, wagonjwa wa nje, damu salama, ujenzi wa jengo la dharura na wagonjwa mahututi katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Manyara; ujenzi wa hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kwangwa - Mara awamu ya nne; ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje awamu ya kwanza katika hospitali ya rufaa

ya mkoa wa Kigoma - Maweni; ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Kilimanjaro – Mawenzi; ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika hospitali ya rufaa ya mkoa wa Simiyu; na ujenzi wa jengo la huduma ya tiba ya mionzi katika hospitali ya kanda ya KCMC. Aidha, miradi nane (8) imefikia wastani wa asilimia 70, mradi mmoja (1) umefikia wastani wa asilimia 45 na miradi 24 iko hatua za awali.

***322. Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Mifupa Muhimbili imeendelea na ujenzi wa jengo jipya la kuhudumia wagonjwa wa nje ili kupunguza msongamano kwa wagonjwa ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 54 na ukarabati wa kituo cha kliniki ya Tumaini ambao umefikia asilimia 99. Aidha, Wizara kupitia Taasisi ya Saratani Ocean Road imeendelea na ujenzi wa jengo la huduma jumuishi za saratani ambao umefikia asilimia 37 pamoja na ujenzi wa kituo cha Saratani Mbeya uliofikia wastani wa asilimia 40 ya utekelezaji. Wizara imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya

kutolea huduma za afya katika hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe ikiwemo maabara ya kisasa, ujenzi wa kituo cha utengamao kwa ajili ya waraibu wa dawa za kulevya. Vilevile, Wizara inaendelea kufanya ukarabati wa jengo la utawala katika Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto ambapo hadi sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 80.

***323. Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na ukarabati wa jengo la kliniki ya wagonjwa wa nje lenye jumla ya vyumba 30 ambalo litatumika katika kuboresha huduma za matibabu na kuendelea kukamilisha ujenzi wa jengo la kutolea mafunzo ya huduma za dharura na majanga ambalo limeanza kutoa huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda Bugando. Aidha, Wizara kupitia hospitali ya kanda KCMC, imeendelea na ujenzi wa jengo la upasuaji uliofikia wastani wa asilimia 89, mabweni ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa wa saratani ambao umefikia wastani wa asilimia 94, maabara jumuishi

umefikia asilimia 90 na jengo la huduma ya magonjwa ya moyo umefikia asilimia 55.

***324. Mheshimiwa Spika***, Serikali imefanya tathmini ya utoaji wa huduma katika hospitali ya Taifa Muhimbili na kubaini mapungufu ya uchakavu wa miundombinu, kutawanyika kwa mpangilio wa majengo, gharama kubwa za uendeshaji na ukarabati wa mara kwa mara na mazingira yasiyoruhusu maboresho ya huduma za ubobezi na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa, Serikali inakusudia kujenga Muhimbili mpya ambayo itapunguza idadi ya rufaa za matibabu nje ya nchi, itaongeza maeneo ya kutolea huduma, itapunguza kero ya kusubiri huduma kwa muda mrefu, itaboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na ndugu wa wagonjwa, itaingiza fedha za kigeni na kuimarisha huduma za ubobezi nchini.

***325. Mheshimiwa Spika***, mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miaka

mitano (5) na kugharimu Shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa majengo, mifumo, ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 908.6 ni mkopo wenye masharti nafuu na Shilingi bilioni 292 ni mchango wa Serikali. Naomba nifafanue kwa kifupi kuwa mchango wa Serikali katika mradi huo kwa sehemu kubwa si fedha taslimu bali ni gharama za maandalizi ya eneo la ujenzi, msamaha wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa bidhaa na vifaa vitakavyoingizwa nchini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi.

326. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imefanya ulinganifu wa gharama za ujenzi wa hospitali mpya ya Muhimbili kwa kulinganisha na miradi mingine 16 kutoka nchi 15 tofauti za barani Afrika, Ulaya na Asia kwa kuangalia ukubwa wa hospitali, gharama kwa mita za mraba, kiwango cha huduma zinazotarajiwa na mwaka wa ujenzi wa mradi. Matokeo ya ulinganifu huo yameonesha kuwa mradi wa ujenzi wa Muhimbili mpya una gharama nafuu ikilinganishwa na miradi kutoka nchi

nyingine. Kati ya hospitali zote zilizolinganishwa, Hospitali ya Taifa Muhimbili ina eneo kubwa la ujenzi kuliko miradi mingine (mita za mraba 115,000) na gharama za ujenzi katika nchi hizo zinakadiriwa kati ya Dola za Marekani 3,000 hadi 7,000 kwa mita za mraba wakati mradi wa Muhimbili mpya utagharimu Dola za Marekani 1,819 kwa mita za mraba. Kwa ulinganifu huu ina maana kwamba, wakati baadhi ya nchi zinalipa mara mbili au zaidi kwa kila mita za mraba, gharama kwa nchi yetu itakuwa chini kwa wastani wa asilimia 42. Tanzania inakwenda kupata hospitali kubwa kwa gharama nafuu na huu si ushahidi wa matumizi mabaya bali ni uwekezaji wa busara na wa thamani nzuri ya fedha za umma. Maboresho hayo yatawezesha hospitali ya taifa Muhimbili kutoka ngazi ya tatu kwenda ngazi ya nne ya utoaji wa huduma za afya kulingana na vigezo vya kimataifa.

**327. *Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa hospitali ya taifa ya kisasa si uwekezaji wa sekta ya afya

pekee, bali ni uwekezaji wa kimkakati katika uchumi wa nchi. Katika ushindani wa kuvutia Makao Makuu ya Mashirika ya Kimataifa, kampuni za kimataifa, taasisi kubwa za kikanda, ubora wa huduma za afya ni moja ya vigezo muhimu vinavyozingatiwa. Wakati mwingine nchi yetu inaweza kukosa kuchaguliwa kuwa makao makuu au kituo cha kikanda cha taasisi na kampuni hizo kwa sababu nchi jirani zina hospitali za kisasa zaidi zinazotoa uhakika wa huduma bora, za haraka na za kibobezi kwa watumishi, familia zao na wageni wa kimataifa. Hivyo, kuwa na hospitali ya taifa ya kiwango cha juu kama Muhimbili mpya kutajenga imani kwa wawekezaji na mashirika ya kimataifa, kutasaidia upanuzi wa biashara na kufunguliwa kwa ofisi za kikanda nchini, kutapunguza hitaji la rufaa za matibabu nje ya nchi, na kunaweza pia kuchangia kupunguza gharama za bima na malipo ya hatari kwa mashirika hayo. Aidha, uwepo wa huduma za afya za kibobezi na teknolojia ya kisasa utaifanya Tanzania kuwa eneo lenye ushindani zaidi katika kuvutia vipaji adimu

vya kitaalamu vinavyohitajika kusaidia sekta mbalimbali za uchumi wetu, zikiwemo viwanda, madini, nishati, fedha, utalii, teknolojia na huduma za kitaalamu. Kwa msingi huo, mradi wa Muhimbili mpya ni sehemu ya miundombinu ya msingi ya uchumi wa kisasa na kichocheo muhimu cha kuongeza nafasi ya Tanzania kama kitovu cha biashara, uwekezaji na huduma za kimataifa na kikanda.

## SEHEMU YA VI: VIPAUMBELE VYA MPANGO NA BAJETI, MAPATO NA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA MAENDELEO VYA WIZARA YA AFYA, KWA MWAKA 2026/2027.

***328. Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele na mpango wa Wizara ya Afya kwa mwaka 2026/2027 vimezingatia mipango ya kitaifa na kisekta ikiwemo, Dira 2050, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Awamu ya Nne, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025-2030, hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kufungua Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sera ya Afya na Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya.

***329. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa, Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza Vipaumbele 11 vya kimkakati pamoja na afua zake zinazolenga kuleta maboresho makubwa katika Sekta ya Afya kama ifuatavyo: -

i. Kuimarisha ubora wa huduma za afya

zinazotolewa ili kukidhi viwango vya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuvijengea uwezo vituo vya kutolea huduma za afya wa kufanya tathmini ya ubora wa huduma zinazotolewa kwa lengo la kufikia viwango na kupata ithibati za taasisi za ndani na nje ya nchi.
b. Kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa taasisi ya ndani ya kutoa ithibati ya ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.
c. Kuhakikisha huduma bora zenye staha na utu zinatolewa kwa wananchi kwa kuendelea kusimamia maadili, usajili wa wataalam, mashauri ya kinidhamu na kitaaluma, ukaguzi na usimamizi shirikishi wa vyuo na vituo vya kutolea huduma za afya.
d. Kuimarisha huduma kwa mteja ikiwemo kupunguza muda wa kusubiri huduma husika, lugha ya mawasiliano, haki na wajibu wa mteja, mfumo wa kushughulikia malalamiko na kutoa mrejesho

pamoja na usalama wa huduma zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

ii. Kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini ikiwa ni pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuimarisha ugharamiaji wa huduma za afya nchini kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani.
b. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili wananchi kutoka kaya zisizo na uwezo na zenye uwezo.
c. Kuendelea kutoa elimu kwa jamii ili wajiunge na bima ya afya.
d. Kuimarisha ushirikiano na Sekta binafsi katika kugharamia huduma za afya nchini.
e. Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera, Ilani ya Chama Tawala (CCM mwaka 2025-2030), Mpango Mkakati wa Muda wa Kati, mipango ya

mwaka, programu na miradi kwa kuzingatia Mipango wa kitaifa, majukumu ya Wizara ili kuweka mipango ya ugharamiaji wa huduma za afya inayotekelezeka.

iii. Kuwezesha na kuharakisha uwekezaji wa viwanda vya ndani ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa bidhaa za afya na kupunguza utegemezi kutoka nje ya nchi kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

   a. Ujenzi wa maabara ya kisasa ya Utafiti wa Dawa na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya uwekezaji katika viwanda vya dawa nchini.
   b. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya virusi vya UKIMWI kwa kuwekeza katika uzalishaji wa dawa katika kiwanda cha TPI pamoja na kuvutia wawekezaji wengine wa viwanda vya dawa.
   c. Kuendelea kuimarisha upatikanaji wa bidhaa za afya kwa kuboresha mifumo ya maoteo, ugharamiaji, ununuzi, utunzaji na usambazaji wa dawa na bidhaa nyingine katika ngazi

zote za utoaji wa huduma za afya.

d. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka nyingine itaendelea kuratibu uwekezaji wa viwanda vya dawa nchini ikiwemo kuandaa majukwaa mbalimbali na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.
e. Kuimarisha ufuatiliaji, uratibu na udhibiti wa usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kusimamia uingizaji wa dawa nchini na matumizi sahihi ya *antibiotics*.

iv. Kuimarisha mifumo na matumizi ya TEHAMA ili kuhakikisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya kwa kutekeleza yafuatayo:

a. Kuendelea kuimarisha mifumo katika vituo vya kutolea huduma za afya ili kuweza kusomana na kubadilishana taarifa.
b. Kuimarisha afya mtandao ikiwemo *teleradiology, teleconsultation* na elimu ya afya kwa umma.
c. Kuhakikisha mifumo inayotumika

katika Sekta ya Afya inapeleka taarifa kwenye kituo kikuu cha kukusanyia na kuhifadhi taarifa (*Central Data Repository)*.

d. Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ili kuondokana na matumizi ya karatasi katika kukusanya, kuchakata, kusambaza na kutumia takwimu ili kuwa na taarifa zenye ubora zitakazosaidia kuweka mipango ya kisera yenye uhalisia.
e. Kuimarisha matumizi ya akili unde (AI) katika utoaji wa huduma za afya nchini.

v. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza magonjwa ya kuambukiza, magonjwa ya mlipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, pamoja na kuimarisha afua za lishe na usafi wa mazingira kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuhamasisha jamii kupima na kutambua mapema hali za afya zao na kuchukua

hatua stahiki.

b. Kuimarisha ufuatiliaji na udhibiti wa magonjwa ya mlipuko na utoaji wa taarifa kwa wakati kabla hayajasambaa na kusababisha madhara makubwa.

c. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha Umahiri wa Elimu ya afya kwa Umma na kusimika mitambo ya kisasa ya TEHAMA na uchapaji ili kuboresha utoaji wa elimu na hamasa za afya kwa umma.

d. Kuendelea na utekelezaji wa Mpango Jumuishi wa Wahudumu wa afya ngazi ya Jamii ikiwemo kuwajengea uwezo na kutoa nafasi 8,000 za ajira mpya nchini.

e. Kuendelea kuboresha na kuhamasisha utoaji wa huduma za chanjo kwa kuweka mfumo wa kielektroniki katika vituo vya kutolea huduma za afya, ununuzi wa majokofu na ufungaji wa vifaa vya kufuatilia mwenendo wa jotoridi kwenye majokofu ya kuhifadhia chanjo.

f. Kuimarisha huduma za kinga tiba dhidi ya magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Halmashauri 19 kwa ugonjwa wa trakoma, matende na mabusha pamoja

na kutoa huduma za utengamao kwa walioathirika.

g. Kuendelea kutekeleza afua za lishe kwa kuelimisha wananchi kutumia vyakula vilivyoongezwa virutubishi ili kupambana na utapiamlo.

h. Kuimarisha huduma ya udhibiti wa magonjwa mipakani kwa kujenga miundombinu ya kuwatenga wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza na ya mlipuko.

vi. Kuimarisha tafiti na matumizi ya matokeo ya tafiti za afya, ubunifu na teknolojia kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuratibu tafiti katika vituo vya kutolea huduma za afya, taasisi, pamoja na vyuo kufanya tafiti zinazolenga kutatua changamoto za afya nchini.

b. Kutoa huduma za afya kwa kuzingatia ushahidi wa kisayansi unaotokana na tafiti.

c. Kukamilisha tafiti zinazoendelea na kuanza tafiti mpya katika maeneo ya huduma za kinga, tiba, utengamao, mafunzo, huduma za dawa na mifumo ya afya.

vii. Kuimarisha huduma za ukunga, afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vya watoto wachanga na vitokanavyo na uzazi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na bidhaa nyingine za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kuchochea juhudi za Serikali za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vifo vya watoto wachanga.
b. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto kwa kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa huduma za watoto wachanga wagonjwa na waliozaliwa na uzito pungufu, vituo vya huduma za kujifungua na vituo vya huduma rafiki ya afya ya uzazi kwa vijana.
c. Kuendelea kuimarisha huduma za ukunga kwa kusisitiza na kusimamia matumizi ya chati uchungu iliyoboreshwa sambamba na kuboresha vyumba vya kujifungulia ili kuwezesha huduma ya mwambata.

viii. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi kwa kutekeleza yafuatayo: -

a. Kuongeza programu za mafunzo ya ubingwa na ubingwa bobezi katika kada mbalimbali za afya kwenye maeneo ya kipaumbele kwa utaratibu wa mafunzo ya muda mrefu na SETI kwa kuzingatia sera za kitaifa za utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi.
b. Kusimamia ubora wa mafunzo kwa wanafunzi katika vyuo vya afya vya umma na binafsi pamoja na mafunzo kwa vitendo kwa watarajali.
c. Kuendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya afya ya kada za kati katika vyuo vya afya.
d. Kuendelea kuajiri watumishi wa kada za afya katika Sekta ya Afya kwa ajira ya kudumu na mkataba.
e. Kuendelea na uimarishaji na utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu katika vyuo vya afya.

ix. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa afua za tiba asili na tiba mbadala kwa kutekeleza afua zifuatazo.

   a. Kuwajengea uwezo wataalam wa kada za afya ili kuimarisha utoaji wa huduma jumuishi za tiba asili katika vituo vya kutolea huduma za afya.
   b. Kuongeza wigo wa huduma za tiba asili ikiwemo kujumuisha dawa na huduma nyingine kwenye mfumo rasmi wa afya.
   c. Kuanzisha na kuendeleza mashamba ya miti dawa kwa kila kanda ili kuhamasisha uzalishaji endelevu wa dawa za tiba asili.
   d. Kununua eneo la kujenga miundombinu ya kituo cha umahiri wa huduma na mafunzo ya tiba asili mkoani Dodoma.
   e. Kuendelea kushirikiana na Mataifa na Taasisi nyingine za kimataifa zilizopiga hatua kwenye matumizi ya teknolojia na tiba asili na mbadala.

x. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa na kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi na kuvutia tiba utalii nchini kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

   a. Kuendelea kutoa huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika hospitali ngazi ya rufaa ya mkoa, kanda, maalum na taifa.
   b. Kuanzisha huduma mpya za kibobezi katika hospitali za rufaa ngazi ya kanda, maalum na taifa ili kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia tiba utalii.
   c. Kuendeleza kituo cha umahiri cha Afrika Mashariki cha matibabu ya magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, upandikizaji figo, upandikizaji wa uloto na kuanzisha kituo cha umahiri cha matibabu ya magonjwa ya kinywa na meno.
   d. Kuongeza idadi ya huduma za ubingwa katika hospitali za rufaa za mikoa kutoka nane (8) hadi 17 na kuanzisha huduma tano (5) za

ubingwa kwenye hospitali za Halmashauri.

e. Kuimarisha huduma za uchunguzi kwa kuhakikisha uwepo wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wa kada za uchunguzi.

f. Kuimarisha huduma za damu salama ikiwemo ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kuwajengea uwezo watumishi pamoja na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuchangia damu ili kuokoa maisha.

g. Kuimarisha huduma za uhandisi na matengenezo ya vifaa tiba kwa kuwaendeleza na kuwajengea uwezo wataalam wa fani hizo.

h. Kuendelea na uimarishaji wa miundombinu ya utoaji huduma katika hospitali za rufaa za mikoa, hospitali za kanda, hospitali maalum na hospitali ya Taifa.

xi. Kuimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao hususan kwa watoto, wazee na watu wenye ulemavu kwa kutekeleza afua zifuatazo: -

a. Kuandaa mpango mkakati wa afya ya akili, msaada wa kisaikolojia na kijamii utakaotoa mwelekeo wa utoaji huduma za afya ya akili katika eneo la kinga, tiba na utengamao.
b. Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi wa Sekta ya Afya ili kukuza usalama wa kazi na ustawi wa kiakili kwa watumishi wa afya.
c. Kuendelea kuimarisha huduma za afya ya akili na huduma za kisaikolojia nchini.
d. Kuimarisha huduma za utengamao na huduma za wazee katika vituo vya kutolea huduma za afya.

## SEHEMU YA VII: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027

### Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2026/2027

***330.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara, Taasisi na hospitali zilizo chini yake inakadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi 747,200,091,299.81**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 76,195,850,735.53** zinatarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya ndani vya Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 165,804,149,264.47** kutoka Hospitali za Rufaa za Mikoa na kiasi cha **Shilingi 505,200,091,299.81** kutoka Taasisi, Hospitali ya Taifa, Maalum na Kanda*.*

### Matumizi ya Kawaida

***331.*** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha **2026/2027**, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 652,236,871,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 36 ya bajeti iliyotengwa, ambapo kiasi cha **Shilingi 516,323,356,000.00** ni mishahara ya

watumishi wa Wizara, hospitali na taasisi zilizo chini yake na kiasi cha **Shilingi 135,913,515,000.00** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Miradi ya Maendeleo**

***332. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha **2026/2027**, Wizara imepanga kutumia kiasi cha **Shilingi 1,148,025,187,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia **64** ya bajeti iliyotengwa. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ni kiasi cha **Shilingi 789,458,609,000.00** na fedha za nje ni kiasi cha **Shilingi 358,566,578,000.00**.

**_333. Mheshimiwa Spika,_** jumla ya fedha zote zinazoombwa na Wizara ni kiasi cha **Shilingi 1,800,262,058,000.00** ili kuweza kutekeleza malengo na vipaumbele iliyojiwekea.

| **Na** | **Fungu** | **Matumizi ya Kawaida** | **Miradi ya Maendeleo** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 52 | 652,236,871,000.00 | 1,148,025,187,000.00 | 1,800,262,058,000.00 |

**_334. Mheshimiwa Spika,_** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Afya _www.moh.go.tz_.

**_335. Mheshimiwa Spika,_** naomba kutoa hoja.




*Waziri Mkuu **Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba** akipokea tuzo ya shukrani ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka kwa Waziri wa Afya **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)** katika hafla ya kuazimisha miaka 30 ya Taasisi ya Saratani Ocean Road.*




Waziri wa Afya, **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)** akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa Kongani ya Viwanda vya Dawa na Vifaa Tiba Mloganzila.



*Naibu Waziri wa Afya **Mhe. Dkt. Florence Samizi** akiwajuli hali wagonjwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro.*



*Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mhe. Dkt. Johannes Lukumay, ilipotembelea mradi wa ujenzi wa Jengo la OPD katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI)*



*Waziri wa Afya, **Mhe. Mohamed Mchengerwa (Mb)**, Naibu Waziri wa Afya **Mhe. Dkt. Florence Samizi (Mb)**, Katibu Mkuu **Dkt. Seif Shekalaghe** pamoja na Mganga Mkuu wa Serikali **Dkt. Grace Magembe** wakiwa katika moja ya vikao vya Kamati ya Bajeti.*



*Waziri wa Afya, **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)** alipotembelea kiwanda cha kuzalisha dawa za kufubaza makali ya virusi vya ukimwi Tanzania Pharmaceutical Industry (TPI) Arusha.*




*Waziri wa Afya* ***Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa*** *(Mb) akifanya ukaguzi wa vifaa tiba katika Taasisi ya Saratani Ocean Road kabla ya kuzindua Bodi ya Taasisi hiyo Januari 5, 2026 Jijini Dar es Salaam.*




*Katibu Mkuu Wizara ya Afya* ***Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe*** *akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua hali ya utoaji wa huduma katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Mwananyamala*



*Naibu Katibu Mkuu **Ndugu. Ismael Rumatila** akiwa na Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru **Dkt. Alex Ernest** na Viongozi wa Wizara wakitembelea Hospitali hiyo.*



*Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia masuala ya dawa na vifaa tiba **Ndugu. Emmanuel Daud Tayari** akiwa na Mwenyekiti wa Umoja wa Wamiliki wa Viwanda vya Kuzalisha Dawa **Ndugu. Bashir Haroon** ambapo walijadili njia bora za kuongeza kasi ya uzalishaji wa dawa.*



*Mganga Mkuu wa Serikali **Dkt. Grace Magembe** akitoa chanjo ya polio ya matone kwa watoto chini ya miaka 10 mkoani Mwanza.*



*Madaktari bingwa wa Rais **Samia Suluhu Outreach Program** wakifanya upasuaji wa kibingwa bobezi katika Hospitali ya Rufaa wa mkoani wa Tabora – kitete.*



Waziri wa Afya **Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa (Mb)** akishiriki katika mazoezi ya kujenga afya ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa




Watumishi wa Mfuko wa taifa wa Bima ya Afya (NHIF) wafikisha bendera ya Bima ya Afya kwa wote katika kilele cha Mlima Kilimanjaro ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa Jamii kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote.




*Bohari ya Dawa ikiendelea na usambazaji wa dawa ili kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za Afya kote nchini vinapata Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi kwa wakati.*



*Moja ya wodi za kisasa za wagonjwa mahututi (ICU) katika hospitali, ikiwa na vitanda vya kisasa na vifaa tiba vya hali ya juu kwa uangalizi maalum wa wagonjwa.*



*Muonekano mpya wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili utakavyokua baada ya kukamilika kwa ujenzi*



*Jengo la huduma ya mama na mtoto la Meta lililo chini ya Hospitali ya Rufaa ya nyanda za juu kusini Mbeya*